

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Saba – Tarehe 12 Aprili, 2021

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Saba. Natumaini mlikuwa na *weekend* njema Waheshimiwa Wabunge, ingawaje *weekend* ilikuwa na mambo yake hii.

Jana nilimtafuta Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa mambo yetu haya ya Bunge kuhusiana na uchangiaji wa Mpango wa Maendeleo akaniambia Mheshimiwa Spika tafadhali niache. Aah! Sasa nakuacha kuna nini tena? Anasema nina *stress*. Kumbe matokeo ya juzi yamempa *stress*. *(Makofi/Kicheko)*

Pole sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, na Wanayanga wote poleni sana. Taarifa tulizonazo ni kwamba wachezaji wana njaa, hali yao kidogo, maana yake wamelegealegea hivi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge baadaye tunaweza tukafanya mchango kidogo tuwasaidie Yanga ili wachezaji... *(Kicheko)*

Katibu, tuendele. *(Kicheko)*

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA NA VIJANA) (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza linaelekea TAMISEMI na litaulizwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge kutoka kule Ruvuma.

Na. 49

Hitaji la Vituo vya Afya – Tunduru

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya katika Kata za Tinginya, Muhimba, Kalulu, Mindu, Nalasi Magharibi na Nalasi Mashariki Wilayani Tunduru?

SPIKA: Majibu ya Serikali kuhusu ujenzi wa vituo vya afya Ruvuma na nchi nzima, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya katika ngazi zote nchini ikiwemo Wilaya ya Tunduru. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi 2020 Serikali imejenga na kukarabati Vituo vinne (4) vya Afya vya Mkasale, Matemanga, Mchoteka na Nakapanya Wilayani Tunduru kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha maboma manne (4) ya zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya ni mengi nchini, ikiwemo Wilaya ya Tunduru. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikiwemo vituo vya afya kwenye Kata za Tinginya, Muhimba, Kalulu, Nalasi Magharibi na Nalasi Mashariki katika Wilaya ya Tunduru kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani ameridhika, tunaendelea na Wabunge wengine. Ahaa, amesimama mwenyewe; Mheshimiwa Jacqueline, swali la nyongeza.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Tunduru, na kwa Kata hizi zilizotajwa; Tinginya, Malumba, Kalulu, Mindu, Narasi Mashariki na Narasi Magharibi, ni kata ambazo hazina vituo vya afya. Lakini pia zinazungukwa na *Selous Game Reserve*. Wakati mwingine unakuta wale akinamama wanaokwenda kujifungua, haja ya kujifungua inawapata wakati wa usiku ambapo sasa kutoka maeneo waliyopo mpaka kufika kwenye hospitali ya wilaya pana zaidi ya

takribani kilometa 80 mpaka 100 na wakati mwingine sasa wamekuwa wakipata majanga ya kuvamiwa na tembo, wanyama wakali kama simba na chui.

SPIKA: Swali.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa wananchi hawa kujengewa vituo vya afya ili waweze kuondokana na adha hiyo?

(b) Mheshimiwa Spika, maeneo hayo yote niliyoyataja yana zahanati tu, na zahanati zao wakati mwingine unakuta hazina watumishi wa kutosha. Zahanati moja ina mtumishi mmoja na kwamba akiumwa huyo mtumishi ni wiki nzima hakuna huduma ya afya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba zahanati hizo zinapelekewa wahudumu wa afya ili waweze kupata huduma inayostahili? Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu vituo vya afya na watumishi wa Sekta hiyo ya Afya tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga vituo vya afya katika maeneo hayo. Na nilishalijibu katika jibu langu la msingi kwamba kwa kadri ya upatikanaji wa fedha Serikali tutaendelea kujenga katika maeneo husika, na nimhakikishie kabisa kwamba Serikali inazingatia umuhimu wa maeneo hayo ambayo wananchi wanatokea. Kwasababu kama alivyoeleza hapo awali kwamba kuna changamoto nyingi. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tutayaingiza katika mpango na fedha itakavyopatikana ataona matokeo yake.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ameeleza kwamba katika maeneo hayo watumishi/wahudumu wa afya hawapo wa kutosha. Na sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tuna huo mpango, kwa kadri

tunavyokuwa tunaajiri kutokana na vibali ambavyo tunapatiwa tutaendelea kuwatenga. Kwa hiyo, hata maeneo hayo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kupeleka kulingana na vibali vya ajira ambavyo serikali itakuwa inatupatia. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pallangyo nilikuona, uliza swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Changamoto zilizoko Tunduru zinafanana sana na changamoto zilizoko kule Arumeru Mashariki, hususan Kata za Maruvango, Kikatiti, Malula na Majengo. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya kwenye hizo kata ambazo nimezitaja?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Silinde tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilijibu katika swali la msingi kwamba kwa kadri Serikali tutakavyokuwa tunapata fedha ya kutosha na bajeti yetu tutakavyokuwa tunaitenga, tutaendelea kujenga. Kwa hiyo, hata maeneo ya Arumeru Mashariki nayafahamu na ninajua umbali wake. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri fedha itakavyopatikana basi tutazingatia na maeneo husika. Ahsante.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hii ya TAMISEMI na bado tuko kwenye swali la afya pia; Mheshimiwa Mragaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, uliza swali lako tafadhali.

Na. 50

Ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Urambo ilijengwa mwaka 1975.

(a) Je, Serikali iko tayari kuifanyia ukarabati wa majengo na miundombinu yake yote?

(b) Je, ni lini Serikali itabadilisha mashine ya *X-ray* ya Hospitali hiyo ambayo imepitwa na wakati?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Hospitali ya Halmashauri ya Urambo ni kongwe na kwamba Serikali itafanya tathmini ya hali ya uchakavu wa miundombinu ya hospitali hiyo ili kuona namna bora ya kufanya ukarabati au ujenzi wa hospitali mpya ya halmashauri hiyo. Aidha, katika mwaka 2015 hadi 2020 Serikali imetoa shilingi milioni 413 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Ukarabati huo ulihusisha Wodi Maalum ya daraja la pili, ujenzi wa jengo la upasuaji, ukarabati wa mfumo wa maji taka pamoja na ukarabati wa Wodi ya Wanawake na jengo la wagonjwa wa nje na upo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji/ ukamilishaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mashine ya *X-ray* iliyopo katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ni ya zamani. Ni vema Halmashauri ya Wilaya ya Urambo itoe kipaumbele na kutenga fedha kupitia mapato yake ya ndani ili kununua mashine ya kisasa ya *X-ray*. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inasimamia utaratibu mpya wa Vifaa na

Vifaa Tiba unaojulikana kama *Managed Equipment Services (MES)* kupitia Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*). Chini ya utaratibu huo, Halmashauri zinafungiwa mashine za *X-ray*, kupatiwa mafunzo kwa wataalam kuhusu matumizi na utunzaji wa mashine hizo, huduma ya kinga na ukarabati kwa vifaa tiba (*Planned Preventive Maintenance*) kwa muda wa miaka mitano. Gharama ya kununua mashine ya *x-ray* kwa fedha taslimu ni shilingi milioni 393.40. Endapo halmashauri itaamua kununua mashine hiyo kwa mkopo, italipa kidogo kidogo kiasi cha shilingi milioni 19.67 kila baada ya miezi mitatu kwa muda wa miaka mitano.

SPIKA: Mheshimiwa Margaret Sitta, nimekuona.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, bado hali ya Urambo ni mbaya kuhusu upimaji wa afya ya akinamama na watoto kwa kuwa *X-ray* ni mbaya. Na wakati huohuo, pamoja na jitihada nzuri ya kupata *ultrasound* mbili, bado *ultrasound* hizo hazina watumishi, zimekaa bure.

Kwa hiyo, sasa kwa kuwa hakuna *X-ray* kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri, *ultrasound* tumejitahidi tumepata mbili, hazina watumishi. Je, lini Serikali italeta watumishi wawili angalau zile *ultrasound* zianze kupima akinamama na watoto? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na nia nzuri ya Serikali yetu ya kutujengea kituo cha afya Mlimani katika Kata ya Uyumbu, jengo la akinamama na watoto linakaribia kuisha lakini limepungukiwa milioni 100. Suala hili tulizungumzia Mheshimiwa Waziri mhusika alipokuja kutembelea, Mheshimiwa Dkt. Festo, bado ile hospitali inahitaji kumaliziwa jengo. Je, lini Serikali itatuletea milioni 100 ambazo tumekisiwa zimalize ili wodi ya akinamama ianze kutumika badala ya sasa wanakwenda mbali kwa lengo la kujifungua? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza na ameomba hapa kwamba walau wapelekewe watumishi wawili katika maeneo ambayo tumepeleka *ultrasound* na *X-ray* katika Wilaya yake ya Urambo. Nimhakikishie kabisa kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tumekubaliana kwamba Waziri husika anaendelea kufanya utafiti na kuhakikisha ndani ya kipindi hiki kifupi wanapeleka mtaalam katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, *commitment* ya fedha ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumaliza jengo lililoko katika Jimbo la Urambo ambayo inahitajika kuhakikisha hilo jengo linaanza kutumika kwa wakati. Nimhakikishie kabisa kwamba nimewasiliana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ameniagiza kwamba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapeleka wataalam wetu wakaangalie hiyo tathmini na baada ya hapo tutatoa majibu ya msingi kuhakikisha hilo jengo linakwisha na linaanza kutumika. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Kilombero, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, japokuwa ntaendelea kubakia kuwa mwananchi mtiifu wa Jangwani, na chini ya *GSM* naamini kwamba tutavuka salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja katika Jimbo la Kilombero na Mheshimiwa Job Ndugai akiwa Mjumbe wa Kamati Kuu alipokuja katika Jimbo la Kilombero, waliwaahidi wananchi wa Jimbo la Kilombero juu ya ujenzi wa Hospitali ya Jimbo la Kilombero. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, dada yangu, Mheshimiwa Umyy, ametuahidi kwamba tutapata milioni 500 za kuanza ujenzi huu.

Mheshimiwa Spika, swali langu; je, ni lini ujenzi huu utaanza?

SPIKA: Je, ni lini ujenzi utaanza Mheshimiwa Naibu Waziri David Ernest Silinde tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kabisa katika bajeti inayokuja ya mwaka 2021/2022, Serikali imehakikisha kuanza hospitali mpya katika halmashauri zote nchini ambazo hazina hospitali za wilaya.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, nilikuona.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, natambua mchango wa Serikali kwa kupeleka fedha kwenye ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nkasi lakini kilio cha Wanankasi ilikuwa ni kupata huduma kwa *leve* ya Wilaya. Mpaka sasa jengo lipo lakini huduma inayotolewa hailingani na huduma inayotakiwa kutolewa katika Hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba pamoja na madaktari kulingana na *leve* ya Wilaya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika eneo lake kuna jengo ambalo bado kutumika kwasababu ya vifaa tiba. Na hilo nimwambie tu kabisa kwamba mimi kabla sijafika hapa nilikuwa nazungumza na Waziri anayehusika na Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na katika bajeti yake ambayo tutakwenda kuipitisha, kuna fungu ambalo tumetenga kwa ajili ya kununua vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya hospitali zote ambazo majengo yake yako tayari lakini hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukishapitisha bajeti, ninaamini kabisa kwamba mara baada ya Bunge hili na mara baada ya bajeti kupita, basi hivyo vifaa na vifaa tiba vitatengwa na kupelekwa. Suala la watumishi basi tutaendelea kutenga kulingana na vibali vya ajira ambavyo tunapatiwa na Serikali. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aida, Mheshimiwa Ally Keissy hajambo huko? (*Kicheko*)

Swali la nyongeza Mheshimiwa Kasalali nimekuona.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, nilikuwa nalenga swali namba 51.

SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega tafadhali.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba nifanye marekebicho kabla ya majibu Kata ya Kihanga, sio Kata ya Kahanga.

Na. 51

Barabara za Kata za Kalenga, Ulanda, Maboga, Wasa na Kihanga

MHE. GRACE V. TENDEGA aliuliza:-

Barabara za kutoka Kata ya Kalenga kuelekea kata za Ulanda, Maboga, Wasa, Kihanga hadi Kijiji cha Mwambao ni mbovu sana: -

Je, ni lini Serikali itahakikisha barabara hizi zinapitika hata kwa kiwango cha changarawe?

SPIKA: Bado tuko TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali kupitia *TARURA* katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilichonga tuta la barabara lenye kilometa 25 iliyozinufaisha Kata za Maboga, Wasa na Kalenga kwa gharama ya Shilingi milioni 153. Vile vile *TARURA* ilifanya matengenezo ya kawaida kwenye barabara ya Magubike, Igangindung'u yenye urefu wa kilomita nane iliyovinufaisha Vijiji vya Kihanga na Mwambao kwa gharama ya Shilingi milioni 69.17. Katika mwaka wa fedha 2021 barabara hizo zimetengewa kiasi cha Shilingi milioni 54 kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara na madaraja nchi nzima kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Grace, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Kata hizo ambazo nimezitaja Kata ya Maboga, Kata ya Kalenga, Kata ya Ulanda, Kata ya Wasa wananchi ni wakulima ambao wanalima mali mbichi nyingi sana; viazi, njengere, maharage na mengine mengi na barabara imekuwa ni kikwazo katika kusafirisha hizo mali zao, na wamekuwa wakipata tabu mali zinaharibikia njiani. Mwaka 2020 pesa alizosema zimetolewa walikwangua sababu ilikuwa ni wakati wa uchaguzi, na sasa hivi barabara hazipitiki.

Je? Kwa nini Serikali haioni kwamba hii barabara sasa imekuwa ni kubwa na inahudumia watu wengi ambayo inaweza ikaenda mpaka ikatokea Madibila Mbeya ili iingie katika mpango wa *TANROADS* na itoke *TARURA*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna barabara ambayo wananchi wametumia nguvu zao ambayo imetobelewa kutoka katika Kata ya Kihanga ikaja katika Kata ya Maboga ambako kuna Zahanati na kuna Hospitali ya Wilaya iliyoko Tosamaganga, wananchi wanashindwa kufika kupata huduma hizo.

Je, ni lini sasa Serikali itaifanyia kazi barabara hii ili wananchi hawa waweze kupata huduma hizo za afya na kuweza kufika katika maeneo hayo kwa urahisi?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Grace, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika; naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameuliza kwamba kwa nini Serikali sasa isione umuhimu wa kuihamisha barabara ambayo inapita Maboga, Kalenga, Wasa, Kihanga mpaka kutokea Madibila kutoka *TARURA* kwenda *TANROAD*.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie kabisa kwamba si barabara zote zinahitaji kupandishwa kwenda na kuhudumiwa na *TANROAD*, lakini jambo kubwa ambalo naweza nikamuhakikishia ni kwamba kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Serikali itaendelea kuzitengea fedha barabara zote za muhimu.

Mheshimiwa Spika, na kikubwa ambacho alikuwa amekisema Serikali haifanyi kazi wakati wa uchaguzi peke yake, Serikali inafanya kazi muda wote, na katika bajeti hizi tumetenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ameuliza vilevile barabara ya kutoka Kihanga kwenda Maboga ambako amesema kuna kituo cha afya ni lini Serikali itahakikisha

kwamba barabara hiyo inajengwa, nimeeleza hapa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na kwa sababu fedha tumetenga katika bajeti na kwa sababu bajeti tunakwenda kupitisha sisi sote hapa nikuombe Mheshimiwa Mbunge tupitisha hiyo bajeti ili barabara zetu zitengenezwe, ahsante.

SPIKA: Nilimuona Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza, ahsante, Mbunge wa Jimbo la Kalenga. *(Makofi)*

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lakini pia namshukuru dada Grace kwa kuuliza swali ambalo tulikuwa tunajadiliana juu ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, aa ninacho...

SPIKA: Mheshimiwa Jackson kwa hiyo swali hili ulimtuma kumbe ee!

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, tunajadiliana, mimi na yeye tunafanya kazi kwa kushirikiana na kwa tunajadiliana; lakini amewahi kuuliza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza ni kuhusu barabara inayotoka Kijiji cha Wenda kwenda Lupembelwasenga inatokea Mgama. Barabara hii kwa taarifa nilizonazo ilikuwa imetengewa fedha katika ule mpango wa *European Union*, na tayari nilishauliza RCC lakini sikupata majibu yanayoridhisha.

Je, Serikali inaweza kunipa majibu sasa, kwa kuwa barabara hii ni muhimu kwa sababu ya wakulima wanaotoka maeneo hayo na kuyawaisha kufika kwenye barabara hizi za lami ili awahi huku Dodoma? Ni lini sasa Serikali inaweza kututengenezea? Ahsante sana.

SPIKA: Siyo watu wa Ujenzi na Uchukuzi ndio wangeweza kujibu hilo? Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu tafadhali.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, barabara hiyo tumeichukua na tutaifanyia upembuzi ili tuone kama inakidhi vigezo vya kuhama ili tuihamishe iende *TANROADS* naomba kuwasilisha.

SPIKA: tunaenda Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali linauliza Mheshimiwa Michael Mwita Kambaki, Mbunge wa Tarime Mjini.

Na. 52

Mgogoro wa Ardhi kati ya JWTZ na Wananchi wa Kinyambi na Bugosi

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaupatia ufumbuzi mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wa kazi wa Mtaa wa Kinyambi na Bugosi katika Halmashauri ya Mji wa Tarime?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhali.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali na kwa ruhusa yako naomba nimshukuru Mungu kwa afya na kuniwezesha kusimama hapa. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais mama yetu mama Samia Suluhu Hassan kwa kuniacha niendeleo kutumika kwenye Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama Waziri. Baada ya shukrani hizo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Kambaki Michael Mbunge wa Tarime Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wananchi waliokuwepo kabla ya eneo kuchukuliwa na Jeshi hawajalipwa fidia. Uthamini uliofanywa na Halmashauri ya Tarime ulikamilika na ambapo kiasi cha shilingi 1,651,984,692.76 zilihitalika. Jedwali lilipelekwa

kwa Mthamini Mkuu wa Serikali mwezi Machi 2020 kupata idhini na lilirejeshwa Tarime kwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2021 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na majibu yaliyotoka ni kwamba, uthamini huo utarejewa kwa kuwa ulifanywa kwa muda mrefu na pia baadhi ya nyaraka zilikosekana kuhalalisha fidia hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mtaa wa Kinyambi na Bugosi wanaombwa wawe na Subira katika kipindi hiki ambacho Halmashauri inafanya taratibu za kurejea uthamini huo. Utaratibu wa uthamini utakapokamilika Serikali italipa fidia kwa wananchi hao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi.

SPIKA: Mheshimiwa Kembaki.

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini ningependa kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mtaa wa Kinyambi na Bugosi hawafanyi shughuli zozote katika maeneo yale, na wengi wao walikuwa wanafanya shughuli ndogo ndogo za kujikimu kama kilimo na shughuli zingine na ukizingatia kwamba ni muda mrefu sasa tangu uthamini ufanyike, mwaka 2013 hadi sasa.

Je, wale wananchi wanaweza kuruhusiwa kuendelea na shughuli zile ili waendeleo kujikimu badala ya kutaabika na kuendelea kukaa pale bila kufanya shughuli ambazo zinawaongezea kipato? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tafadhali.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba maeneo yote ambayo yanamilikiwa na Jeshi letu ni muhimu na kwa manufaa ya nchi yetu na kwa wananchi kwa ujumla. Lakini niseme tu kwamba uwepo wa maeneo haya umepangwa *kistratejia (strategically)*, tumejipanga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kazi za jeshi zinafanyika vizuri. Niwaombe tu wananchi waweze kuvuta subira; kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, tunafanyia kazi ili tuweze kuwatendea haki wananchi hawa; hii ni pamoja na kuwalipa fidia zao ambazo zitawawezesha kwenda kufanya shughuli zao zingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kwanza nikupongeze kwa namna ambavyo mara kadhaa tumeweza kuzungumza na Mbunge ili tuone namna nzuri. Kikubwa nachoweza kusema hapa ni kwamba sisi tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba zoezi hili linakamilika mapema na wanachi wanapata haki zao. Tunaogopa kwamba tukiwaruhusu wananchi wakiendelea kutumia maeneo haya wanaweza wakafanya vitu ambavyo vina gharama kubwa na baadaye vikawatia hasara ndugu zetu hawa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wavute subira tu, nafikiri tutaendelea kushughulikia suala hili kwa kuwasiliana Serikali zetu za Wilaya na Mkoa ili tuone namna nzuri ya kuwafanya wananchi wasikwame, waendeleo kufanya uzalishaji na shughuli zao zingine. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante nakushukuru sana, nimekuona Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru ni dhahiri kwamba maeneo ya Bugosi na Kinyambi ni tatizo la takriban miaka 17. Mara ya mwisho Serikali kupitia aliyekuwa Waziri wa Ulinzi ambaye ni Rais wa Zanzibar kwa sasa walifanya tathimini kwa mara ya pili hapo mwaka jana na wakawa wameshajiridhisha kwamba ile ya kwanza ilikuwa inawapunja Watanzania wale wa Tarime, na wakasema tayari wameshapitisha wanasubiri HAZINA kulipa

hela na aliyekuwa Waziri wa Fedha ambaye ni Makamu wa Rais alidhihirisha hili kwamba tayari Fedha za Tarime zipo tayari kulipwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hayo wanayokuja kusema leo inaonyesha ni jinsi gani Serikali haitoi umakini na uzito pale ambapo wananchi wamekuwa wametwaliwa ardhi. Sasa, ningeomba Mheshimiwa Waziri alete zile fedha ambazo zilishapitishwa tayari walikuwa wanasubiria Hazina kutoa ziende kuwalipa wale wananchi wa Tarime ili waende maeneo mengine wapishe jeshi lifanye shughuli zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhali.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba ule umakini wa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki yao ndio huo ambao kwa namna nyingine umesababisha tumechelewa. Pia tumechelewa kwa sababu yapo matatizo kadhaa, Mheshimiwa Matiko anafahamu. Kwamba wakati wa zoezi hili likifanyika kwenye uthamini, na kwa uzoefu umeonyesha maeneo mengi, kumekuwa na changamoto hizi, na hasa Serikali inapona kwamba kuna wananchi watakosa haki zao.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana tukazingatia kwamba wananchi wapate haki zao. ndiyo maana unaona hata uthamini uliochelewa kwa utaratibu wa sheria na kanuni zilizokuwepo kwa nia hiyo hiyo ya kuwa-*compensate* wananchi kile ambacho wamechelewa kukipata ndiyo maana tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge, vuta Subira; na sisi tumejipanga na sasa tunacho

kitengo cha milki kwa nia ya kuhakikisha kwamba kinafanya kazi yake vizuri kwa matatizo hayo. Yako matatizo mengi maeneo mbalimbali; kwamba tumeweka kitengo hiki ili kiweze *ku-coordinate* ili tuone zile changamoto ambazo zilikuwa zinatokea zinaondoka. Tukienda kwenye hatua ya uhakiki wenzetu upande wa Hazina na kadhalika; changamoto nyingi zimekuwa zikionekana lakini tumedhamiria kuona kwamba maeneo haya, maeneo ya Tarime na maeneo mengine nchini yako mengi tunafanya hivyo kuhakikisha kwamba ile migogoro iliyokuwepo tunaenda kuimaliza. Kwa hiyo Mheshimiwa Matiko naomba uvute subira na ninaamini kwamba tutaenda kulimaliza mapema, tumejipanga vizuri. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri nawaona Waheshimiwa mnaosimama kwenye swali hili lakini mnikubalie tuendee kwa sababu Kamati yetu ya ulinzi inamambo ya nje chini ya Mheshimiwa Zungu ilileta jambo hili la fidia za maeneo ya Jeshi kama hoja maalum kwenye Kamati ya pamoja ya Uongozi na Kamati ya Bajeti; na tumelisukuma jambo hili kwenye Wizara ya Fedha, linatazamwa ki-aina yake ikiwezekana kabla ya mwezi Juni basi tumuwezeshe Mheshimiwa Waziri amalize baadhi ya haya matatizo. Kwa hiyo linafanyiwa kazi hivi sasa linao msukumo wetu sisi wenyewe Wabunge jambo hili la maeneo ya Jeshi. (*Makosi*)

SPIKA: Wizara ya Elimu Sayansi ya Teknolojia swali linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido. Mheshimiwa Kiruswa tafadhali.

Na. 53

Ufundishaji wa Lugha ya Viziwi

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA aliuliza:-

Uziwi ni moja ya aina ya ulemavu ambao una lugha yake ya ishara (*signal language*).

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kufundisha Lugha ya Ishara kama moja ya masomo ya lazima Shuleni kwa wanafunzi wote kuanzia Elimu ya Awali ili kuondoa kikwazo cha mawasiliano kati ya wenye uziwi na wale wanaosikia?

(b) Je, Tanzania tuna vitabu vya kufundishia Lugha ya Ishara katika lugha ipi?

SPIKA: Majibu ya Swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa Mbunge Longido, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Lugha ya alama katika kuondoa kikwazo cha mawasiliano kati ya wenye uziwi na wale wasio na uziwi. Aidha, ili kufikia lengo la kufundisha lugha ya alama kama somo katika ngazi zote za elimu, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuboresha ufundishaji wa lugha hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kukamilika kwa usanifishaji wa Kamusi ya Lugha ya Alama ya Tanzania pamoja na uandaaji wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi viziwi Kidato cha kwanza mpaka cha nne chini ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kupitia Chuo cha Ualimu Patandi na Chuo Kikuu cha Dodoma walimu wenye taaluma ya Elimu Maalumu katika fani ya ukiziwi na lugha ya alama wanaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, vitabu vinavyotumika kufundishia lugha ya Ishara vimeandikwa katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijauliza, niseme tu kwamba sijapata majibu kamili ya swali langu kwa sababu nilitaka kujua kwamba elimu ya viziwi itatolewa lini kwa wanafunzi wote wa shule zetu nchini ili kuweza kuondoa hicho kizingiti cha mawasiliano; lakini naona mjibu swali, Serikali inaonekana *ina-focus* katika kutengeneza mtaala wa kuboresha elimu kwa wale ambao ni viziwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba niulize maswali haya madogo ya nyongeza; swali la kwanza;

Je, katika nchi yetu tuna shule ngapi zinazotoa elimu kwa viziwi kwenye ngazi ya Msingi, Sekondari na Vyuo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ningependa kujua kwamba kwa kuwa katika nchi yetu lugha rasmi zilizo, zinazotumika kwa mawasiliano ni Kiswahili lugha yetu ya taifa nani ya kimataifa pia na kingereza; nikitaka kupata kitabu au Mtanzania akitaka kupata kitabu cha *sign language* kwa kiingereza na *sign language* ya Kiswahili atavipata wapi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa katika nchi nyingine wanafundisha hivyo *compulsory* kwa wanafunzi wote kusoma lugha ya alama?

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, kwanza *ni-declare interest* kwa sababu mimi nimekuwa nikisaidia watoto viziwi kusoma. Nina wachache wanasoma Kenya, nina watatu wanafikia kidato cha nne mwaka huu, na kitabu wanachotumia kinaitwa *Kenya Sign Language*. Lakini pia nilipokuwa nasoma Marekani nimeona *American Sign Language*; lakini hapa kwetu nafahamu shule moja ya msingi ambayo inasomesha viziwi iko Moshi -Kilimanjaro - Himo

na wale wanasoma kwa Kiswahili. Sasa kunakuwa na *crush*, kwamba wale watoto walioko Kenya wakija wakikutana na hawa viziwi walioko Tanzania wengine wanaongea *sign language* ya Kiswahili lakini wenzao wanaongea *sign language* ya kiingereza. Sasa nilikuwa nataka kujua jinsi ambavyo tungeweza kuwa na hivyo vitabu vya *sign language*...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, haya ahsante.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: ...katika lugha hizo ili tuweze kutoa hiyo...

SPIKA: Haya, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri eneo hili nyinyi ndio wataalam, majibu tafadhali Mheshimiwa Juma Kipanga. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kiruswa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameuliza suala la shule maalum mahsusi kwaajili ya wanafunzi wetu hawa wenye ulemavu wa usikivu. Tuna shule za msingi 14 ambazo ni mahsusi kabisa kwa ajili ya wanafunzi wetu hawa ambao wana matatizo ya usikivu. Pia shule za sekondari zipo 25, lakini vile vile tunachuo cha ualimu maalum kabisa ambacho kiko Patandi.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya swali la msingi nilizungumza kwamba hivi sasa tunaboresha au tuko kwenye mikakati ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kutoa elimu hiyo kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge, kuanzia ngazi ya elimu msingi mpaka chuo. Lakini katika muktadha wa vitabu nimezungumza katika majibu ya msingi kwamba tumetunga kamusi ambayo inatumia hiyo lugha ya alama.

Mheshimiwa Spika, lakini wanafunzi hawa jukumu letu kubwa sana ni kuhakikisha kwamba tunapata walimu wa kufundisha lugha hizi za alama. Kwa upande wa vitabu, vitabu vinavyotumika ni vitabu vya kawaida kabisa kwa sababu wao wanaweza kuona suala lililokuwepo ni namna gani ni kuweza kufundishwa au kufundishika. Kwa hiyo jukumu letu tunaoenda nalo hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza walimu wa kutosha wa kuweza kutumia lugha ya alama; na katika chuo chetu kikuu cha Dar es Salaam sasa tunatoa stahabada ya mwaka mmoja katika kipengele hiki cha lugha ya alama ili kuhakikisha kwamba tunapata walimu wa kutosha wakuweza kufanya *service delivery* na kutoa elimu hii kwa wanafunzi wetu hawa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata kwa Wizara hiihi ya Elimu, linaulizwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa uliza swali lako, tafadhali.

Na. 54

Kuboresha Miundombinu ya Chuo Kikuu cha Afya Mbeya, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Mbeya College of Health and Allied Sciences (UDSM - MCHAS)

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Chuo Kikuu cha Afya Mbeya pamoja na Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Mbeya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tupo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Naibu Waziri, Omari Juma Kipanga.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ndaki ya Afya ya Sayansi Shirikishi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilihamia Mbeya mwezi Desemba, 2017 ili kupata hospitali kubwa ya kufundishia. Ndaki ilipewa nafasi katika majengo ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya, baadhi ya majengo yaliendelea kutumika kama ilivyokuwa na baadhi yalihitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, imefanya upanuzi na ukarabati mkubwa wa bwalo la chakula na ukarabati wa madarasa na maabara. Pia Chuo kilinunua na kufunga jenereta la dharura kwenye maabara. Kutokana na ufinyu wa nafasi ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, kama mkakati wa muda mfupi, majengo matatu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yaliyopo eneo la Uzunguni yamekarabatiwa na kuwekewa samani ili yaweze kutumika. Pia Serikali imefunga vifaa vya TEHAMA katika majengo mbalimbali ya Chuo na kuweka mtandao wa *internet* kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa muda mrefu ni kupata ardhi Jijini Mbeya ili kuanza ujenzi wa majengo ya Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi. Mkakati huo utatoa fursa ya kuongeza miundombinu ya kisasa ya kufundishia na kujifunzia na kuongeza udahili wa wanafunzi wa shahada mbalimbali za Afya na Sayansi Shirikishi. Maombi ya ardhi yameshawasilishwa na ufuatiliaji unaendelea. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza na nishukuru kwa jibu kutoka kwa Wizara ya Elimu. Kutokana na umuhimu wa huduma ya afya na hasa kwa suala zima la kupatikana kwa wahudumu pamoja na madaktari katika kipindi hiki

ambacho milipuko ya magonjwa imepamba moto. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia ardhi ya Taasisi za Serikali zilizopo katika Wilaya ya Mbeya ikiwemo ardhi ya *Tanganyika Packers* ili iweze kukidhi mahitaji ya chuo hiki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, hii Ndaki ya Afya ina mkakati au mpango gani wa ziada zaidi ya kufundishia ili tuweze kupata huduma nyingi kutokana na hili eneo kubwa ambalo watakuwa wamepatiwa sasa hivi na Serikali? Nashukuru sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Kipanga.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anayozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mkakati wa kupata eneo hilo amelizungumza linalomilikiwa na *Tanganyika Packers*, ambalo liko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi lakini vilevile Wizara ya Ardhi pamoja na Menejimenti ya Chuo na Uongozi wa Wilaya tutahakikisha tunakwenda kupata umiliki wa eneo hilo ili kuweza kufanya ujenzi wa chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, pindi tutakapopata eneo hili, basi Serikali inaweza kutenga bajeti sasa kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga hospitali kubwa ambayo pamoja na Ndaki hii inaweza kuambatanishwa na Ndaki nyingine ili kuweza kupata wataalam wengi zaidi kwa ajili ya kuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, mkakati wa muda mrefu kama nilivyozungumza mwanzo ni kwamba Serikali inatambua jambo hilo na tutakwenda kushughulikia kwa kadri bajeti itakavyoruhusu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaelekea Wizara ya Nishati, swali sasa litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Edward Olelekaita.

Na. 55

Mkakati wa Ajira Kupitia Mradi wa Bomba la Mafuta Hoima – Tanga

MHE. EDWARD O. KISAU aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa ajira za upendeleo kwa vijana na fursa nyingine za kibiashara kwa wananchi wa Jimbo la Kiteto kupitia mradi mkubwa wa kimkakati wa Bomba la Mafuta (Hoima – Tanga) ambalo linapita katika Wilaya ya Kiteto?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Kabaale/Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, bomba litapita katika Mikoa 8 na Wilaya 24 ambapo Wilaya ya Kiteto itapitiwa na bomba kwa urefu wa kilomita 117.1 pamoja na ujenzi wa kambi ya kuhifadhi mabomba katika kijiji cha Ndaleta na kambi ya wafanyakazi katika Kijiji cha Njoro.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Bomba hilo kupita katika Wilaya ya Kiteto, wananchi wa Kiteto watanufaika na ujenzi wa mradi huu kwa kufanya biashara, ajira na fursa

nyingine za kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa kazi za mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Julai, 2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutoa hamasa ili wananchi wanufaike na shughuli za ujenzi na uendeshaji wa mradi.

SPIKA: Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Edward K. Olelekaita, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yenye furaha kidogo kwa wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna ajira nyingi sana zinsemwa kuwepo katika mradi huu, je, hawaoni kwamba wananchi wangu wa Kiteto hususan vijiji saba vile; Mwitikira, Ndorokoni, Dareta, Ovoponi, Kimana na Amei wakatengewa kabisa fursa za kibiashara na ajira za upendeleo kwa kuwa wao ndiyo wanabeba *burden* ya mradi huo kwa kilometa hizo 117?

Mheshimiwa Spika, swali lingine la pili dogo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa amesema Wizara itaendelea kuhamasisha wananchi wajitokeze kuchukua fursa hizi atakuwa tayari kuongozana na mimi tutembelee vijiji hivi saba ili tutumie wasaa huu kuendelea kuwaandaa wananchi wetu kwa fursa hizo, tena ikizingatiwa kwamba Mheshimiwa Rais, Mama Samia Hassan Suluhu jana amekwenda kwenye kutiwa saina sasa kwa mkataba huu na kwamba karibu sasa mradi unaanza? Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Dkt. Medard Kalemani, tafadhali.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitoe shukrani kwa jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri katika swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa ya jumla kwa wananchi wa Kiteto pamoja na maeneo mengine kwamba utekelezaji wa mradi huu unaanza mwezi huu Aprili, tulipanga tuanze mwezi Julai kama ambavyo tumeeleza kwenye jibu la msingi lakini tunaanza rasmi mwezi huu wa Aprili kwa muda wa miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Tanzania ni kweli mimi nilishiriki nikiwa na Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan utiaji saini utekelezaji wa mradi huu jana nchini Uganda. Mradi huu ni mkubwa utapita katika mikoa 8, wilaya 24, vijiji 127, vitongoji 502 vikiwemo vijiji na vitongoji vya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi utatoa ajira kwa zaidi ya Watanzania 10,000 katika hatua za awali na hadi ajira za Watanzania 15,000 katika shughuli za ujenzi na shughuli za kawaida. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba sana wananchi hasa katika maeneo ambapo mradi utapita wajitokeze kuchukua hizi fursa kwa sababu tumeziweka rasmi kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kufuatana naye, tumepanga kuanzia Kyaka nchini Tanzania kule Kagera hadi Tanga Chongoleani, tutaanza kufanya ziara wilaya kwa wilaya, mkoa kwa mkoa ili kuhamasisha Watanzania kuchukua fursa hiyo. Kwa hiyo, tutafika na katika eneo lake na kutembelea vijiji hivyo saba ambavyo Mheshimiwa amevitaja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali litaulizwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula. Mheshimiwa Mabula, tafadhali uliza swali lako.

Na. 56

Ujenzi wa Barabara ya Kinyata hadi Usagara – Mwanza

MHE. STANSLAUS S. MABULA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Kinyata kwa njia nne kutoka Mwanza Jiji kuelekea Usagara?

SPIKA: Majibu ya Serikali, Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Msongwe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyamagana – Usagara ni sehemu ya barabara Kuu ya Mwanza – Shinyanga Mpakani yenye urefu wa kilometa 104. Barabara hii ni muhimu katika kukuza uchumi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na ni kiunganishi kati ya Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Geita na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanza mipango ya kuanza ujenzi wa barabara ya Mwanza hadi Usagara kwa njia nne. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii unaendelea ambapo umezingatia kupanua barabara hii kuwa na njia nne kuanzia Mwanza Mjini hadi Usagara yenye urefu wa km 22. Kazi hii inafanywa na Mhandisi Mshauri *M/s NIMETA Consult (T) Ltd* ya Tanzania kwa gharama ya Shilingi Milioni 980.84. Aidha, usanifu wa kina unatarajiwa kukamilika Septemba, 2021 na baada ya kukamilika barabara hiyo itaingizwa kwenye mpango wa ujenzi ikiwa ni pamoja na upanuzi wa njia hizo nne kutoka Mwanza Jiji hadi Usagara kutegemea na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mabula nimekuona.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na changamoto za kifedha kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo jibu la Waziri linasema ujenzi wa barabara hii baada ya Mkandarasi Mshauri kuwa amekamilisha kazi yake itategemea na upatikanaji wa fedha. Upatikanaji wa fedha ni kweli kwamba unaweza ukachukua hata zaidi ya miaka mitatu au minne. Swali langu la kwanza, kwa sababu barabara sasa hivi imekuwa na magari mengi takriban 2,000 kwa siku kutoka Nyegezi kwenda Usagara mpaka Mjini, Serikali itakuwa tayari angalau kuanza kwa hatua mbili; walau baada ya Mkandarasi Mshauri kumaliza itakuwa tayari kuanza kujenga hata kwa km 10 kwa *phases* na baadaye km 10?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, wako watu kutoka Kata ya Nyegezi na Mkolani ambao wameongezeka zaidi ya mita 7.5 kwenye barabara hii na watu hao wanastahili kulipwa fidia. Je, Serikali itakuwa tayari kuwalipa fidia stahiki kwa sababu za msingi ili barabara hii iweze kujengwa bila vikwazo na wananchi wapate huduma?

SPIKA: Kwanza watu wa Mwanza barabara ile siyo ya Kinyata, maana wao wanaita ya Kinyata kama mtakavyoona kwenye *Order Paper* zenu, ile ni barabara ya Kenyata. Mheshimiwa Naibu Waziri, Eng. Godfrey Msongwe, majibu ya maswali hayo mawili, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, usanifu wa kina utakamilika Septemba na

baada ya hapo barabara hiyo itaanzwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Kuhusu upatikanaji wa fedha na ni kwa kiasi gani tunaweza kujenga, matarajio ya Serikali ni kukamilisha barabara lakini tutaanza kadri fedha itakavyopatikana ndiyo tutaanza kujenga kama ni km 5, km10 ama ikiwezekana zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu fidia, hatutajenga bila kufanya tathmini na ndiyo maana ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao unachukua masuala yote; kuangalia ni kiasi gani cha fedha kinatakiwa ili wananchi wa Kata za Buhongwa na Nyegezi ambao wameongezeka sana watafidiwa. Ni utaratibu kwamba ni pale ambapo wananchi wa Kata za Buhongwa na Mkolani watakapokuwa wamefidiwa ndipo ujenzi utaanza. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mwenyekiti wa PAC, swali la nyongeza, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Bunge lililopita la Kumi na Moja, Bunge lako Tukufu lilielezwa kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni 5 kuanza kuweka lami barabara ya kutoka Same Kisiwani - Mkomazi. Je, kazi hii itaanza lini? Ahsante (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Godfrey Msongwe, kazi hii itaanza lini, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ilivyoahidi kwamba imetenga shilingi bilioni tano kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Same Kisiwani, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bado barabara nyingi hazijatanzwa na zitaendelea kutanzwa kadri tunavyokwenda na barabara nyingi tu zitatangazwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Pia tunategemea

baada ya bajeti hii barabara hizo zitaendelea kujengwa ikiwa pengine ni pamoja na hii Same Kisiwani, itategemea na bajeti hii tunayoendelea kuipitisha itakavyokuwa imepita. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati DKt. John Pombe Magufuli, alivyokuwa Karagwe aliahidi kwamba watu wa Kyerwa watajengewa barabara kilomita 50 kwa lami. Hii barabara ya lami inahitajika kweli kwa sababu imekuwa ni mgogoro wa wananchi, je, itaanzia wapi hiyo kilomita 50 ya lami? Licha ya kuahidiwa bado ujenzi huo haujaanza. Swali, ni lini hizo kilometa 50 tulizoahidiwa na Mheshimiwa Rais zitaanza kujengwa hata ikibidi tukaongezewa zikawa hata 100? *(Makoff)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo la maeneo ya Kyerwa huko, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Godfrey Msongwe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi zote za Viongozi wa Kitaifa tunazizingatia na huwa tunazitekeleza. Ahadi ikishatolewa kuanza kwa barabara si kuingia *site* na kuona magreda yanaanza kutembea lakini barabara itafanyiwa usanifu na usanifu wa kina ndipo itakapoanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili barabara itaanzia kujengwa wapi, sisi kama Serikali kokote tukianza ili mradi kilomita 50 zitatimia tutaijenga barabara hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na taratibu za kutimiza ahadi za Viongozi wa Kitaifa ikiwa ni pamoja na barabara hii ambayo Mheshimiwa

Mbunge ameitaja kwamba zitajengwa kama zilivyoahidiwa na Kiongozi wetu wa Kitaifa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Kassinga nimekuona.

MHE. ALLY M. KASSINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Umuhimu wa barabara ya Kenyatta katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza ni sawa kabisa na umuhimu wa barabara ya kutoka Kiranjeranje - Nanjilini mpaka Ruangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Jimbo la Kilwa Kusini. Lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

SPIKA: Haya, barabara inayoelekea Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, lini mtajenga kwa kiwango hicho cha lami kutoka Nanjilini? Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, barabara hii ni kati ya barabara ambazo zimeainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ni barabara ambayo pia imeahidiwa na viongozi wa Kitaifa. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri fedha itakapopatikana barabara hii itanza kujengwa kwa kiwango cha lami mara baada ya kukamilisha usanifu wa kina wa barabara hii. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe. Mheshimiwa Mpembenwe tafadhali.

Na. 57

Minada ya Zao la Korosho na Ufuta

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha minada ya zao la Korosho na Ufuta inafanyika kwa wakati mmoja ili kuondoa mporomoko wa bei kwa baadhi ya maeneo yanayolingana kwa misimu sawa ya kuvuna mazao hayo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe tafadhali.

MHE. NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia mifumo miwili katika minada. Mfumo wa kwanza ni mfumo wa *TMX* na wa pili ni mfumo wa kutumia sanduku ambao umekuwa ukitumika katika maeneo mengi kwa muda mrefu katika nchi yetu. Serikali itaendelea kutumia mifumo yote hiyo miwili ili kuhakikisha minada inafanyika kwa wakati mmoja kwenye maeneo yenye msimu wa mavuno unaofanana ikiwemo Mkoa wa Pwani ili kuongeza ushindani wa bei na uwazi katika mauzo ya Korosho, Ufuta na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, kuanzia msimu wa 2019/2020 Serikali kupitia Bodi ya Korosho, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Soko la Bidhaa kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika, imeanza kutekeleza mauzo ya Korosho na Ufuta katika minada ya kielektroniki sambamba na mfumo wa uwekaji zabuni kwa njia ya sanduku kwa zao la Korosho.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mfumo wa kielektroniki yatasaidia kuendesha minada kwa wakati mmoja na kujenga mazingira bora ya ushindani na kuondoa changamoto iliyopo sasa ambapo baadhi ya wanunuzi hulazimika kwenda kwenye minada inayofanyika kwa nyakati tofauti. Ili kuhakikisha mkulima anapata bei nzuri, Serikali inasimamia suala la ubora na uzalishaji wa tija ili kuhakikisha mazao ya Korosho, Ufuta na mazao mengine yanafikia viwango vya ubora vinavyohitajika sokoni, pamoja na kuimarisha uwazi katika uendeshaji wa minada kwa lengo la kuimarisha ushindani wa bei.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hatua hizo, Serikali kupitia Bodi ya Korosho ya Tanzania na Soko la Bidhaa,

zimeweka utaratibu wa kusajili wanunuzi wa Korosho na Ufuta mapema kabla ya msimu wa mazao kuanza, na kuhakikisha mazao yaliyokusanywa na wakulima kupitia Vyama vya Ushirika yanatangazwa kwa wanunuzi mapema ili kuvutia wanunuzi wengi watakaoshindana kwa bei kulingana na ubora wa mazao yao ili mkulima aweze kuuza mazao yake kwa bei itakayompatia faida.

SPIKA: Mheshimiwa Mpembenwe, nimekuona uliza swali lako.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, wananchi wa Jimbo la Kibiti na wajomba zangu wa Rufiji wamekuwa wahanga namba moja sana wa bei za mazao ya Korosho pamoja na Ufuta katika kila msimu katika kila mwaka: Je, Serikali sasa iko tayari kutoa tamko ni msimu gani kutakuwa na mnada wa aina moja katika maeneo yote ambayo yanauza au yanavuna mazao haya?

Swali la pili; bei ya Korosho huwa itegemea sana na...

SPIKA: Hebu rudia swali lako la kwanza.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, Swali langu la kwanza ni kwamba, Serikali iko tayari kutoa tamko kwamba ni lini au msimu upi wataanza kufanya minada inayolingana katika maeneo yote yanayokuwa yanavuna mazao hayo kwa wakati mmoja? Kwa sababu mfumo wa *TMX*...

SPIKA: Nilisema urudie kwa sababu inaonekana, si ndiyo swali lako la msingi uliuliza?

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, hili halikujibiwa ipasavyo kwa sababu mfumo wa *TMX* ni mfumo ambao huwa unafanyika kwa kupitia Kanda moja na Kanda nyingine...

SPIKA: Haya endelea.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, Ahsante.

Swali langu la pili: Je, Serikali ina mpango gani; kwa kuwa suala la Korosho huwa linategemea sana na *grade* ya Korosho; *Grade A* huwa inauzwa kwa bei ya juu sana, lakini wananchi wa Jimbo la Kibiti pamoja na wajomba zangu wa Rufiji wamekuwa wahanga sana wa bei ya Korosho hasa *grade A* kwa sababu katika kila msimu Korosho *Grade A* inayouzwa katika Mkoa wa Pwani bei yake inakuwa chini sana ukilinganisha na Korosho *Grade A* inayouzwa katika maeneo mengine ambao wanavuna katika msimu unaofanana? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe tafadhali, kuhusu Korosho na Ufuta.

MHE. NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, kuhusu minada kufanyika kwa wakati mmoja, Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi kwamba toka msimu huu umeanza, tumeanza *ku-introduce* mfumo wa TMX. Mfumo huu umeanza kufanyiwa majaribio katika baadhi ya maeneo na tumeona upungufu wake na tunafanyia marekebisho ili uweze kujenga mazingira ya kuwa na *online platform* na kuongeza uwazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mfumo wa *TMX* utakapokuwa umekidhi vigezo tunavyovitarajia, utatumika katika maeneo yote ya kuanzia Pwani, Lindi, Mtwara mpaka Ruvuma ambako kuna uzalishaji wa Korosho lakini minada itaendana na mambo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ya kwanza ni Ikolojia. Kwamba wakati mazao yanazalishwa eneo A na kama eneo B wakati huo huo mazao hayo yamezalishwa, basi minada itafanywa kwa pamoja ili kuongeza *transparency*.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi timu yetu ya wataalam iko katika

Mkoa wa Pwani ikifanya tathmini kubwa mbili; moja, tatizo la ubora ambalo linasababisha Korosho ya Pwani ikose bei sawa sawa na Korosho ya Tandahimba. Kuhusu suala la changamoto iliyoko katika Mkoa wa Pwani, ambayo Waheshimiwa Wabunge na wenyewe wanaifahamu, kwamba, kwa kuwa Mkoa wa Pwani unakabiliwa na uwepo wa mvua nyingi kuliko maeneo mengine, wakulima wa Pwani wamekuwa wakikumbwa na tatizo la Korosho yao kuwa na unyevu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo imeiagiza Bodi ya Korosho sasa hivi kuangalia namna gani tutavisaidia Vyama vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika vya Mkoa wa Pwani hasa *CORECU* ili viweze kuondokana na tatizo la unyevu na kuwapatia vifaa vya kuweza kuanikia Korosho yao ili iweze kukidhi viwango vinavyostahili.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, wiki ijayo Ijumaa tutakuwa na Mkutano mkubwa utakaoongozwa na Waziri wa Kilimo hapa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge wa Korosho tutawaalika, tutagawa vifaa katika baadhi ya Vyama vya Ushirika ili kuongeza ubora wa Korosho katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge watupe muda, tathmini inaendelea na minada itafanyika kwa pamoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Vita Kawawa, utafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa. Kwa kuwa zao la Ufuta katika Mkoa wa Ruvuma linaonekana ni zao linalokua kwa kasi kibiashara: Je, Serikali ipo tayari kutuongezea mbegu na tuwe tunapata mbegu za Ufuta kwa wakati na zilizo bora? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, tafadhali.

MHE. NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo katika Bajeti mtakapoiona itakapokuja, *priority* yetu ni uzalishaji wa mbegu. Tunataka Mwenyezi Mungu akitujaalia katika Bajeti inayokuja, tuhakikishe nguvu zetu kubwa tunawekeza katika uzalishaji wa mbegu; na Ufuta ni moja ya zao ambalo lipo katika *list* yetu ya *priority* na kwa Mkoa wa Ruvuma vile vile zao la Soya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Bajeti ya Wizara ya Kilimo itakayokuja katika mwaka ujao wa fedha uwekezaji mkubwa utakuwa ni katika eneo la umwagiliaji na hasa uzalishaji wa mbegu ili tuweze kuondokana na tatizo la mbegu; na Ufuta ni moja ya zao litakalopewa kipaumbele.

SPIKA: Mheshimiwa Nape Nnauye nilishakutaja.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025, Chama cha Mapinduzi kiliahidi kwamba Serikali itaweka utaratibu sasa wa kuanza kununua chokocho au mabibo yaliyokaushwa: Je. Serikali iko tayari kuanza kununua mabibo hayo kwa msimu huu wa Korosho unaokuja? (*Makofi*)

SPIKA: Habari njema hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo. Serikali iko tayari kununua mabibo?

MHE. NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahadi iliyowekwa katika Ilani ni kuhakikisha kwamba mkulima wa Korosho anauza Korosho, anauza Bibo na ikiwezekana hata *product* ambazo zinatokana na zao la Korosho ikiwemo Siagi na vitu vingine. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie tu kwamba, *TARI* Naliendele wameshamaliza tathmini ya namna gani ya wakulima wataweza kuvuna Korosho na Ijumaa mkihudhuria kikao mtaona Mheshimiwa Dkt. Kapinga

anafanya *presentation* ya kwanza ya namna ya kuvuna kwa kutumia Neti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba Serikali haitanunua Mabibo, bali tutahakikisha Mabibo yanavunwa kwa ubora unaostahili ili yaweze kununuliwa na wafanyabiashara na yaweze kuongezewa thamani.

Mheshimiwa Spika, Kongwa vile vile Korosho zako ulizoanza kuvuna hivi karibuni ndani ya kipindi cha miaka hii mitano, Bibo na lenyewe litapata soko. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa nawaona mna maswali mengi ya Korosho, lakini basi tumalizie na Mheshimiwa Ahmed Katani mkulima namba moja wa Korosho kutoka Tandahimba.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Spika, msimu kwa Korosho unapofika kwenye minada yetu kumekuwa na ubora wa Korosho. Korosho ile ile yenye ubora wa *outturn* 52 ya Tandahimba, *nut-count* ya 180 ya Tandahimba, *moisture* ya 8 ya Tandahimba, inakuwa na bei tofauti na Korosho ya Newala, lakini kila kitu kiko sawa. Je, Serikali inatambia nini? Kuna nini kati kati yake kinachofanya bei hizi ziwe tofauti wakati ni Korosho zile zile zinazotoka Tandahimba kwenda Newala?

SPIKA: Kwa hiyo, ya Newala inakuwa na bei juu kuliko ya Tandahimba? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali kuhusiana na bei hizi tofauti tofauti.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Katani anafahamu changamoto zilizopo na michezo iliyoko. Nataka tu nimwahidi kwamba, michezo iliyoko na ambayo imekuwepo kwa muda mrefu katika ukanda huo, safari hii tunaenda kuimaliza na tumeanza hatua ya kwanza kwa kuwa na *transparency system*, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametusaidia sana kwamba minada badala ya kulaza gudulia kesho, kesho kutwa halafu bei ndiyo ifunguliwe, utaratibu huo umeondoka kwa mwaka huu wa kwanza.

Mwaka huu tumefanya *transparency* kwa mara ya kwanza minada hadharani inafunguliwa kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumejifunza jambo jipya. Nataka nimuhakikishie, mbinu za kivita hazitangazwi hadharani, lakini tutalimaliza Mwenyezi Mungu akitujaalia msimu ujao.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maji, swali litaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba. Mheshimiwa Chikota tafadhali.

Na. 58

Kujenga Miradi ya Maji kwa Kutumia Maji ya Mto Ruvuma

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutumia maji ya Mto Ruvuma kwa ajili ya kujenga miradi mikubwa ya maji ambayo itatatua changamoto za maji katika Jimbo la Nanyamba na maeneo jirani?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji kutoka Mto Ruvuma ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati ambapo Serikali inatarajia kuanza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2021/2022 kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia *RUWASA* ukarabati na upanuzi wa Mradi wa Maji kwenye Vijiji vya Makongo na Migombani umekamilika na unatoa huduma kwa wananchi.

Vilevile, visima viwili vimechimbwa, nyumba ya mtambo wa kusukuma maji, ulazaji wa bomba kuu kilomita 3.5, ujenzi wa tenki moja la ujazo wa lita 100,000 na ujenzi wa matanki mengine manne unaendelea kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji Nanyamba Mjini. Pia utekelezaji wa miradi katika Vijiji vya Ngonja – Chawi, Mayembejuu, Nyundo A na B, Nitekela na Misufini upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

SPIKA: Ahsante sana Engineer. Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; nafikiri mradi ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameujibu ni ule mradi unaotoa maji Mayembechini na kupeleka Manispaa ya Mtwara na Nanyamba itafaidika kwa kutoa maji Nanguruwe kupeleka Nanyamba: Serikali haioni sasa kwa sababu usanifu huu ni wa zamani, wafanye *review* ya usanifu ili maji yatoke moja kwa moja Mayembechini na kupeleka Nanyamba na hivyo kunufaisha Kata ya Kiromba, Kiyanga na Mbembaleo; na vile vile, itasaidia kupeleka Wilaya za jirani kama Tandahimba na Jimbo la Mtama jirani na Jimbo la Nanyamba? (*Makofi*)

Swali langu la pili; ili kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Nanyamba, pia mradi wa Makonde ambao unanufaisha Halmashauri nne lazima upatiwe fedha za kutosha za ukarabati: Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa wa Mradi wa Makonde ili Halmashauri ya Nanyamba, Tandahimba, Newala Mjini na Vijijini wapate maji ya kutosha? Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chikota. Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa ukarabati wa mradi tunafahamu kuna baadhi ya maeneo miradi ipo chakavu ikiwepo Nanyamba. Tayari Wizara imeshatoa maelekezo kwa Wahandisi wetu walioko maeneo hayo na ukarabati huu unatarajia kuanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa Mradi wa Makonde vile vile, tutaendelea kupeleka fedha kwa awamu kadiri tunavyopata ili kuhakikisha mradi huu wa Makonde kwa ukubwa wake na umuhimu wake, tutaendelea kuukarabati na kuuongezea thamani ili uendelee kutoa huduma kwa wananchi wa Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota kwa namna ambavyo ameendelea kufuatilia upatikanaji wa maji safi na salama ya kutosheleza katika Mji wa Nanyamba na tuseme tu kwamba kwa sisi Wizara tumejipanga kuhakikisha Nanyamba maji yanakwenda kupatikana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Maswali ya nyongeza sasa. Nilikuona Mheshimiwa Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa suala la upatikanaji wa maji safi na salama bado ni tatizo sugu katika Mkoa wa Mtwara na hivyo kupelekea akina mama kutumia maji ya kuokota okota na hivyo kuongeza gharama za matibabu kwa sababu ya matazizo ya homa za matumbo na kadhalika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tunamaliza tatizo la kuongeza gharama za matibabu kwa sababu ya upatikanaji wa maji ya kuokota okota ambao unapelekea wananchi kuendelea kupata homa mbalimbali? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo la maji ya kuokotaokota, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya umuhimu wa upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Mtwara, Serikali kwa kupitia Wizara ya Maji, tayari tumejipanga kuhakikisha tunakwenda kutumia maji ya Mto Ruvuma. Tutakapoweza kufanya mradi huu, adha ya maji katika Mji wa Mtwara, Nanyamba na maeneo yote ya mwambao ule yanakwenda kukoma kwa sababu itakuwa ni suluhisho la kudumu. Kwa hiyo, tunatarajia mwaka ujao wa fedha kutumia maji ya Mto Ruvuma.

SPIKA: Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Aysharose Mattembe, uliza swali lako.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Nimekuwa nikisimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuulizia Mradi wa Maji Kitinku-Lusilile ambao umechukua muda mrefu sana kukamilika, lakini bila ya mafanikio yoyote. Ningependa kupata *commitment* ya Serikali, ni lini Mradi wa Maji Kitinku-Lusilile utakamilika? Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Naibu wangu kwa namna anavyojibu maswali vizuri. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kubwa nimefanya ziara katika Mradi ule wa Kitinku-Lusilile, moja ya changamoto kubwa ilikuwa juu ya deni la mkandarasi, alikuwa akidai kama milioni 700. Wizara tumekwishamlipa milioni 700 zile mkandarasi yule. Mkakati wetu ni kuhakikisha mradi ule unakamilika kwa wakati na wananchi wale wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Bulaya, halafu Mbunge wa Nyang’hwale atamalizia.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wewe utakuwa shahidi hiki ni kipindi changu cha tatu katika Bunge lako Tukufu na siku zote tatizo kubwa kwenye Wizara ya Maji imekuwa ni vitu viwili, mosi; miradi kutokukamilika kwa wakati au ikikamilika haitoi maji. Hii Wizara tangu 2016 imekuwa ikitengewa pesa nyingi, lakini ufanisi na ubora na kile kinachokusudiwa, wananchi wapate maji safi na salama hakipo. Swali langu, je, Serikali ipo tayari kufanya ukaguzi maalum nini chanzo cha miradi kukamilika lakini maji hayatoki au ni nini kinachosababisha miradi ichukue muda mrefu? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu tafadhali.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru. Nikiri, moja ya changamoto kubwa sana ya miradi yetu ya maji ilikuwa moja, usimamizi lakini Bunge lako Tukufu limeona hili na ndiyo maana tukaanzisha Wakala wa Maji Vijijini kwa maana ya *RUWASA*, lakini kuhakikisha wahandisi wote wa maji waliokuwa chini ya halmashauri kuja chini ya Wizara yetu ya Maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumeshaainisha miradi zaidi ya 177 na *RUWASA* imeshaanza kuitatua miradi hiyo zaidi ya 85. Kubwa ambalo nataka niwaelekeze Wahandisi wa Maji pamoja na Wakandarasi, vipo vya kuchezea. Ukishiba, chezea kidevu chako au kitambi, si miradi ya maji, tutashughulikiana ipasavyo! Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Nimeipenda hii. Namkumbusha Mheshimiwa Mwigulu, umemsikia Mheshimiwa Waziri amesema vipo vya kuchezea, usichezee Simba! *(Makofi/Kicheko)*

Nilikutaja Mheshimiwa Mbunge wa Nyang’hwale, swali la mwisho Wizara ya Maji.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kidogo Wagogo mnapata shida kuita jina Hussein, jina langu ni Hussein Nassor Amar, ni Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kuishukuru Serikali kwa kuendelea kukamilisha mradi ya maji katika Jimbo la Nyang'hwale. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja na tukafanya nae ziara. Tukawa na upungufu wa shilingi milioni 250 tu ili tuweze kukamilisha mradi huo. Je, Naibu Waziri, ahadi yake ataikamilisha lini ya kupeleka milioni 250 ili kuweza kukamilisha Mradi huo wa Nyang'hwale? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, tafadhali utakamilisha lini ahadi yako kule Nyang'hwale?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor wa Jimbo la Nyang'hwale, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, hizi fedha tayari tuko kwenye utaratibu wa kuzipeleka, tutazipeleka katika awamu mbili, wiki ijayo tutajitahidi kupunguza awamu ya kwanza na baada ya hapo tutajitahidi kukamilisha kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo, bado tuko maji. Mheshimiwa Deo Sanga Mbunge wa Makambako.

Na. 59

Mradi wa Usambazaji Maji Makambako

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Kusambaza Maji Mji wa Makambako utaanza?

SPIKA: Ni lini Mji wa Makambako utasambaziwa maji? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* India jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28. Utekelezaji unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuchukua miezi 24.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Sanga au umeridhika?

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali ya nyongeza mawili. Swali la kwanza; kwa kuwa kuna miradi inayoendelea katika Jimbo la Makambako, Mradi wa kwanza mkandarasi yupo Usetule-Mahongole; mkandarasi wa pili yuko Ibatu; na mkandarasi wa tatu yuko Mtulingana, Nyamande na Bugani. Je, ni, lini Serikali itawalipa wakandarasi hawa ili waweze kumalizia miradi hii kwa sababu wanakwenda kwa kususasua ili wananchi waendeleo kupata maji yaliyokusudiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa mradi huu wa kutoka fedha Serikali ya India miji 28 ikiwemo na Mji wa Makambako. Miradi hii tangu yupo Waziri Profesa Maghembe inazungumzwa na kwa mara ya mwisho alipokuja Rais ambaye ni Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wananchi wa Makambako waliuliza ni lini mradi huu utaanza? Sasa nataka kujua kwa sababu kuna baadhi ya watu wanataka kuwekeza viwanda pale, wanakosa kuweka

viwanda, tunakosa wawekezaji wengi ni kwa sababu mradi huu haujaanza. Sasa nataka Serikali iniambie hapa na iwaambie wananchi wa Makambako, ni lini mradi huu utaanza ili wananchi waendeleo kuwekeza viwanda kama ambavyo wanahitaji pale Mji wa Makambako? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lini wakandarasi watalipwa? Tayari wakandarasi mbalimbali wameanza kulipwa na Wizara inafanya jitihada kila tunapopata fedha kuendelea kupunguza *list* ya wakandarasi ambao wanadai Wizara. Kwa hiyo kadri tunavyoendelea kupata fedha, *list* itakapomfikia mkandarasi huyu na yeye pia atalipwa.

Mheshimiwa Spika, Miji 28 utekelezaji wake kama nilivyojibu kwenye swali lake la msingi, mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka huu 2021 utekelezaji wa miradi hii utaanza na itatekelezwa kwa miezi 24.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza na Mheshimiwa Tabasam atafuata.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kiu ya wananchi wa Makambako inafanana kabisa na kiu ya wananchi wa Same. Mradi umechukua muda mrefu na wakati wa kampeni alipopita Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati huo akiwa Naibu Waziri na sasa Waziri ndugu yetu Aweso, aje mara moja na yeye akasema yale yale maneno ya kutokushika kidevu lakini uchezee kitambi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, je, ni lini wananchi hao wa Same watasambaziwa maji?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Same wanapata lini maji? Majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana mama yangu Shally Raymond, amekuwa mpiganaji mkubwa sana hususan wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro; Moshi, Same na Mwanga waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, moja ya miradi ambayo ilikuwa imechezewa na wakandarasi wababaishaji ni Mradi wa Same – Mwanga na nilipata nafasi ya kwenda katika mradi ule, tumekwishawaondoa wakandarasi wale. Kubwa kazi hii tumeweza kuwapa wenzetu wa *DAWASA* kuona tunaweza kuifanya kwa *force account*, mwisho jana Katibu Mkuu alikuwepo huko, tumewekeza nguvu zetu kuhakikisha mpaka Desemba mradi ule uwe umekamilika na wananchi wale waweze kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Tabasam, nilikuona.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Sengerema. Ni kwamba tuna miradi mikubwa, Mradi wa Sengerema ni mradi mkubwa katika nchi hii, una bilioni 23, lakini una deni la shilingi milioni 300 kutoka *TANESCO*. *TANESCO* wamekuwa wakikata maji toka mradi huu umefunguliwa na kuna mabomba yako Sengerema pale yanasubiri kusambazwa kwenye hiyo miradi ya maji.

Je, Waziri yuko tayari kukubali wananchi wa Sengerema wauze yale mabomba halafu wakalipie umeme ili tukae salama sisi.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni kubwa na namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji, yuko tayari kufuatana na mimi kwenda Sengerema akaone hii hali?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Sasa niko tayari kuongozana naye lakini hapa niwe muwazi, Serikali eneo la Sengerema imewekeza zaidi ya bilioni 20, imetimiza wajibu wake, lakini ni haki ya mwananchi kupatiwa maji nay eye ana wajibu wa kulipia *bills* za maji. Kwa hiyo kubwa yawezekana kuna changamoto pia ya kiutendaji kushindwa kusimamia na kukusanya mapato. Haiwezekani uwe na mradi wa bilioni 20, halafu ushindwe kukusanya mapato angalau kulipia umeme, haiwezekani! Kwa hiyo nitafika na tutaangalia namna gani ya kumsaidia. Tukiona mtendaji yule anashindwa kutimiza wajibu wake, tutashughulikiana ipasavyo kuhakikisha wananchi wa Sengerema wanaendelea kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema. Ujue Wasukuma wana matatizo, ujue Waziri ana kazi nyingi badala ya kuomba ufuatane na Naibu Waziri halafu sasa... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kunti, swali la mwisho kwa siku ya leo.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kwenye sekta hii muhimu. Suala zima la maji ya Mradi wa India imekuwa ni changamoto kubwa sana katika hii miji 28 na ambayo inasababisha Watanzania wengi kukosa maji. Nataka tu kujua, Mji wa Chemba ambao umekuwa kwenye ahadi ya Miradi ya India miaka nenda miaka rudi, ni lini Serikali itapeleka mradi mbadala wakati Watanzania wanaendelea kusubiri huo Mradi wa India ambao umeshindwa kutekelezeka kwa kipindi cha muda mrefu?.

SPIKA: Maji Chemba, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimtoe hofu dada yangu Kunti, Mheshimiwa Mbunge. Serikali haijashindwa, Serikali ipo kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji katika Taifa letu na ndiyo maana tuna miradi mikubwa mbalimbali ambayo tunaitekeleza. Katika eneo hili la miji 28,

wewe ni mmojawapo ambao sisi umetumia hatua ya kutuita kuona hatua ya utekelezaji wake. Nataka nimhakikishie ukiona giza linatanda ujue kunakucha, timu yetu ya *evaluation* imekamilisha kazi. Naomba watupe nafasi waone namna gani Serikali hii ya mama yetu Samia Suluhu ambaye ametupa maelekezo mahsusi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunawatua akinamama ndoo za maji kichwani itafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Chemba pamoja na hiyo miradi mikubwa ambayo ipo kimkakati, Mheshimiwa Mbunge tumekwishakutana nae ametuomba visima vya dharura katika eneo lake la Chemba ili wananchi wake waweze kuapat huduma ya maji. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda mkiangalia mtaona muda hauko upande wetu. Mheshimiwa Kunti hakuwa na muda tu wa kuzungumzia habari ya Bwawa la Farkwa kwenye Mpango wa Miaka Mitano hatuna hakika kama ujenzi wa Bwawa la Farkwa umo. Tukumbuke kuweka hicho kitu kama hakipo.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, sasa tusikilizane ili twende vizuri. Kwanza, wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Mgeni wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaye ni *Project Engineer*, Victor Ndozero. *Engineer* Ndozero karibu sana mjengoni. Azam mnaonekana *clear* kabisa. Tunawapa pongezi nyingi muendeleo kuimarisha muonekano wenu hasa kwenye eneo la michezo ambalo mnafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Wako wageni watatu wa Mheshimiwa Catherine Magige, kutoka Arusha ambao ni jamaa zake wakiongozwa na ndugu Adolph Raphael Olomy. Ahsanteni sana kutoka Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Mrisho Gambo ambao ni wapiga kura wake kutoka Jijini Arusha

wakiongozwa na Diwani ya Kata ya Moshono Mheshimiwa Miriam Kisawike. Karibuni sana wale ndugu zetu kutoka Moshono. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia yuko mgeni wa Mheshimiwa Jerry Silaa, ndugu Nuru Chalamila, karibu sana Nuru. Karibu sana. (*Makofi*)

Nitangaze kwamba kwa wale Wabunge wa CCM, kutakuwa na *Party Caucus* lakini jioni baada ya kuahirisha Bunge la jioni kwenye ukumbi wa Msekwa hapa. Wale wa CCM tukimaliza jioni *party caucus* Msekwa, sio saa nane, jioni baada ya kuahirisha Bunge. *Party Caucus* hii ni muhimu sana tunaombwa wote kuhudhuria.

Tuendeleo kupata vipaumbele vya Wabunge kama tulivyotangaza hivi karibuni vya bajeti za Wizara zinazokuja. Baadhi wameshawahi, wengine hamja-*indicate*. Waheshimiwa Wabunge wengi mnapenda kufanya vitu mwisho mwisho sijui kwa nini. Sijui mnapenda kusikiliza wengine kwanza halafu ndiyo upate wazo. Kama nilivyowaambia juzi, wale wa siku ya *day one* ya Mpango walipata dakika 10, *day two* ya Mpango wamepata dakika 10, leo ni dakika tano tano. Sasa inakusaidia nini kama ulikuwa na hoja yako muhimu si ungefanya kule mwanzo? Kwa hiyo jilandikisheni mapema ili kama kuna Wizara ambayo una nia kabisa ya kuweka mchango wako basi tuweze kuweka maneno. Tumia Bunge mtandao kama una mashaka namna ya ku-*lodge* kwenye Bunge mtandao wako vijana wetu wa *IT* wanapita mara kwa mara kwenye madawati hapo.

Leo tutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa Bunge *Sports Club* kuanzia saa nane kamili kwenye ukumbi wa Msekwa na uchaguzi huo utasimamiwa na Naibu Spika, naomba Wabunge wote wapenzi wa michezo pamoja na watumishi wa Ofisi ya Bunge ambao wanashiriki kwenye michezo kwa pamoja twende tuchague viongozi wetu wa Bunge *Sports Club* na wagombea tunao wengi kabisa tutajua wakati huo tutakapofika kule. Nisisitize kwa nafasi za juu za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti tujitahidi kuhakikisha kwamba walio wengi na walio wachache wanapata nafasi

kwa sababu vinginevyo twende na sura ile ile ya Bunge *Sports Club* kama kawaida kuwa na ushirikishi fulani hivi. (*Makofi*)

Baada ya tangazo hilo, sasa tunaendelea na uchangiaji moja kwa moja ili tuweze kuokoa muda wetu kwa sababu leo ndiyo siku ya mwisho ya uhitimishaji wa hoja, tutahitimisha jioni, lakini sasa tuanze na uchangiaji na mtu wa kwanza kutuanzishia uchangiaji leo ni Mheshimiwa Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Saasisha Mafue. Dakika tano tano nimeshasema.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2021/2022 – 2025/2026

(*Majadiliano Yanaendelea*)

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, lakini kabla ya kusema nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima. Kwa sababu ya muda nitachangia maeneo mawili tu kwenye mpango huu, nitachangia eneo la kilimo, lakini nitachangia eneo la viwanda. Na hii ni kubeba azma yetu, ndani ya Jimbo la Hai tumekubaliana kuwa na Hai mpya ya kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wametangulia kueleza sana azma hii ya kuwa na kilimo cha biashara kama ambavyo imeelezwa kwenye ukurasa ule wa 65 wa mpango huu kwamba, tunadhamiria sasa kuwa na kilimo-biashara.

Sasa tunazungumza sana, niombe ifike mahali sasa tuamue kwa dhati kuwekeza kwenye kilimo. Mpango huu unataja kwamba, ni eneo linalotoa ajira kwa Watanzania wengi zaidi ya asilimia 66.3 kwa hiyo, ninaomba sasa hebu tufanye kwa kudhamiria kabisa tukijua ni eneo ambalo linaenda kuokoa uchumi wetu Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa kufanya hivyo niombe tuanze kwa kufanya utafiti wa tathmini ya udongo nchi nzima. Ninajua ziko taarifa hizi, lakini sio kwa maeneo yote na kwetu sisi pale Hai tuliomba taasisi ya *TARI* Mlingano wakatufanyia tathmini ya udongo ndani ya Jimbo la Hai. Faida ya kuwa na tathmini ya udongo kwenye eneo hili ni kuondoa changamoto wanazokutananza wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nitoe mfano, mkulima wa nyanya anapambana sana na ugonjwa wa kuungua kwa nyanya yake, lakini bila kujua kuungua kwa nyanya kinachosababisha ni aina ya udongo alipopanda. Pengine *PH* yake *calcium* iliyoko kwenye udongo sio rafiki kwa hiyo, tukiweza kufanya tathmini ya udongo tukatoa taarifa kwa wananchi itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuwa na mbegu ya hakika. Wananchi wanawekeza kwa nguvu kubwa sana kwenye kilimo, lakini je, tuna uhakika na mbegu wanayoipanda? Lakini pia mifumo ya kudhibiti mbegu zinazoingiziwa barabarani ikoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Waziri wa Kilimo unanisikia. Wekeni mifumo Madhubuti ya kuwa na mbegu zetu sisi zinazozalishwa hapa Tanzania ambazo ni rafiki kulingana na aina ya udongo tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuwa na maji ya hakika ya kumwagilia. Mikoa mingi ukitazama, Mkoa wa Kilimanjaro, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Iringa na Mikoa mingine inayofanana na hiyo ina maji ya hakika ya kumwagilia. Tatizo ni miundombinu ya kutufikishia maji kwenye mashamba yale. Kwa mfano kule kwetu Mkoa wa Kilimanjaro na hasa Jimbo la Hai, tunavyo vyanzo vya maji, mifereji mitano. Tukipata mifereji hii namhakikishia Mheshimiwa Waziri wa kilimo tunaenda kuchangia vizuri sana kwenye pato la Taifa na tunaenda kutokomeza umasikini ndani ya Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Spika, tuna Mfereji wa Mtambo, Isimila, Kimashuku, Makeresho, Longoi, Metro, lakini pia tunalo bwawa la kihistoria ambalo limefanyiwa utafiti na wenzetu wa China, lina maji ya kutosha, Bwawa la Boluti. Kwa hiyo, nikisema pamoja na mengine kwenye mikoa mingine tuhakikishe tuna maji ya hakika na tuweke fedha nyingi kwenye bajeti inayokuja, ili wananchi walime kilimo cha biashara ambacho hakitegemei mvua kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuwa na wataalam wa kutosha. Maeneo mengine tumeweza kupeleka watumishi wa kutosha, eneo hili la kilimo na mifugo ninaomba bajeti hii inayokuja tutenge fedha kwa ajili ya watumishi wa kutosha, ili wakatoe ushauri kule wananchi waweze kulima kilimo hiki cha biashara ambacho ndio tunalenga huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuongeza thamani ya mazao. Na hii ndio dhana yangu ya kilimo na viwanda. Eneo hili linatusababishia umasikini na wananchi kutokunufaika na mazao yao kwasababu, tunalima hatuongezi thamani. Mfano pale kwetu tunazo taarifa kwamba, wapo wakulima wafanyabiashara kutoka nje ya nchi wanakusanya mazao yetu, nyanya, mbogamboga, wanapeleka nchini kwao wanaenda kufungasha. Wakifungasha wanaturudishia sisi kununua nyanya ileile, kununua karoti ileile kwasababu tu, wameongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sasa kwenye mpango huu Waziri wa viwanda tuhakikishe tunakuwa na viwanda vingi vya kuongeza thamani ili mazao yetu yaweze kuuzika ndani ya nchi na nje ya nchi yakiwa yamefungashwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine tuimarisha taasisi zetu, hii taasisi ya *TARI*, Mlingano na taasisi nyingine zinazofanana na hivyo zijengewe uwezo. Tunao wataalamu wengi ukienda Wizara ya Kilimo pale utakuta wapo wataalamu wengi na wengi wamesoma nje ya nchi. Huko kwenye mashamba

makubwa duniani wamesoma huko, lakini wamekaa ofisini pale tunataka watoke ofisini...

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa...

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: ...aai.

SPIKA: Dakika tano zimekwishapita. (*Makofi*)

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Asante. Mheshimiwa Rose Tweve, utafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa namna ambavyo ameandaa na kuwasilisha huu mpango hapa Bungeni, ili na sisi tuweze kutoa mapendekezo yetu.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye vipaumbele vitano ambavyo Mheshimiwa Waziri alivielekeza hapa Bungeni kuwa ambavyo, ndivyo vitakavyotusaidia kuhakikisha sisi kama Watanzania tutakuwa na uchumi endelevu na shindani na tutoke sasa kwenye hii asilimia sita tuweze kufika kwenye asilimia nane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na nita-zero in kwenye kile kipaumbele namba tano ambacho umehakikisha kama Taifa tutahakikisha tunaendeleza hii rasilimali watu. Na *issue* hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeeleza kuwa unataka kufanya maboresho kwenye sekta ya elimu. Mheshimiwa Waziri maboresho peke yake hayawezi kutusaidia sisi kufikia yale malengo yetu, *we need total transformation* kwenye sekta ya elimu, tunahitaji mapinduzi makubwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizobarikiwa Tanzania *is one of them*. Tuna *natural resources* za kutosha, tuna ardhi

ya kutosha na hii rasilimali watu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaiongelea ndipo hapa kwenye changamoto. Tuna vijana ambao zaidi ya asilimia 65 wangetumika kama nguvukazi ya kuja kuboresha uchumi wetu. Hapa ndipo tunapotaka kuanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata nchi za wenzetu ambazo zimepiga hatua, *let say China*, wao tayari wapo juu, lakini na wao wameamua kufanya *total transformation* kwenye mfumo wao wa elimu kuhakikisha vyuo hivi vikuu wamebadilisha vyuo vikuu 600, ili vije kuwa vyuo vya kati; vyuo vya ufundi kuhakikisha wanazalisha vijana ambao wana *skills* za kuajiriwa kwenye viwanda vyao na pia *thinking*. Wana *critical thinking* ya kuhakikisha wanatumia mazingira ya kujanzishia biashara na kufanya shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, twende Singapore. Wao kuanzia mwaka 1997 mpaka 2012...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nawaombeni sana, hata ninyi wenyewe mkikaa mnaona masikio yenu jinsi yanavyokataa hizi kelele ambazo mnapiga. Na hizi *five minutes* ambazo kila Mbunge anaongea hapa ni *very critical* ni vizuri ukasikiliza *argument* ya mtu anasema nini. Mkitaka kuongea mnakwenda *canteen* pale mnapiga na kahawa kidogo, mnapiga *story* zenu zote mnamaliza. Tupeane nafasi tusikilize watu wanaongea kitu gani, kuna hoja muhimu sana zinazoongelewa humu ndani.

Endelea Mheshimiwa Rose Tweve!

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nilikuwa natoa mfano wa Singapore wenzetu kwa miaka 15 walihakikisha wanabadilisha mfumo wao wa elimu wakajikita *focus* yao ikawa kwenye *skill development* na kuhakikisha watoto na vijana wao mashuleni wana uwezo wa kufikiri, *critical thinking*. Sasa sisi hapa Tanzania *it is opposite*, tuna *human resources*, tuna ardhi, tuna *natural resources*, lakini mfumo wetu wa elimu, tume-*focus* sasa kwenye vyuo vikuu

kuzalisha *degree* ambapo mmekuja kutueleza hapa hazina tija hata kwenye soko letu la ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndipo hapa ningeoomba kama Taifa tufanye *total transformation*. Mdogo wangu pale Viti Maalum kutoka Mwanza alisema tuwe na agenda za kitaifa; hii ndio iwe agenda yetu sasa kuhakikisha hawa vijana wetu wanaweza kuwa na uwezo wa kufikiri na kuwa na *skills* za kuweza kuajiriwa. Tuhakikishe hivi vyo vya kati ndio vinapewa msukumo na vyo vya ufundi. Sasa hivi *funding* zote zinakwenda kwenye elimu ya juu, hii ndio iwe *think tank* yetu, moja tutakuwa na vijana ambao wanajitambua, tutaongeza wigo wa walilipa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *as of today number* ya walipa kodi ni 3,985,493 *out of 60 million people*. Hata tukisema tutoe hao wazee na vijana bado tungekuwa na milioni 23 ya Watanzania ambao wangekuja kuongeza pato la Taifa. Hata tuweke mazingira mazuri kiasi gani kwa hawa watu *less than four million* hatuwezi kufikia malengo yetu ya kuhakikisha tunakuwa na uchumi endelevu na shirikishi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakuomba tuhakikishe sasa hata hivi viwanda tunavyoajiri tukiweka msukumo huku kwenye mfumo wetu wa elimu hata hawa *investors* wanaokuja watakuwa *attracted* kuja Tanzania kwasababu watakuwa na *guarantee* na vijana ambao wapo *much skilled*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata hizi nchi zinazokwenda ku-*invest* China kama Marekani wanakwenda kule sio kwasababu kuna *cheap labor*, wanakwenda kule kwasababu wana vijana ambao wako *much skilled*. Anaweza akafanya na akawa mchango kuhakikisha wanaendeleza viwanda vilivyopo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hapa ndipo tunapotakiwa kuanza. *This is a piece of the puzzle* ambayo ina-*miss* kwenye mfumo wetu wa elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimitakie heri Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji wa majukumu yake natuhakikishe tunaanza hapo. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rose Tweve, mchango makini sana huo. Wizara ya Elimu tunahitaji *transformation* ianzie kwenu. Katika mpango wetu wa miaka hii mitano tuje na *skills development plan* inayoendana na haya mabadiliko ambayo dunia inatulazimisha twende nayo. Nilishakutaja Mheshimiwa Aida, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Kyombo. Mheshimiwa Aida dakika kumi.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima kuweza kupata tena nafasi hii kuzungumza ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wote waliosema kuna umuhimu wa kuwa na *agenda* za kitaifa. Kuna maana kubwa ya kuwa na *agenda* za kitaifa. Tunatambua kuanzia Awamu ya Kwanza mpaka sasa tuko Awamu ya Sita, kuna mambo ambayo yaliibuliwa na awamu zote, lakini unaona umaliziaji unakuwaje. Tunapokuwa na *agenda* za kitaifa kila anayekuja, hatujui kesho atakuja Rais wa namna gani, atatokea chama gani, kukiwa na *agenda* za kitaifa zinam-*guide* kwamba Taifa tunakwenda hivi. Kwa hiyo, ni vizuri jambo hilo likaangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa letu limebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi, ukiangalia ndani ya Bunge, tika nimeingia Bunge lililopita, tukianza kuzungumza suala la maji kila Mbunge anasimama anazungumza uchungu ulivyo.

Mheshimiwa Spika, nchi hii tuna mito ya kutosha, tuna maziwa ya kutosha, tuna bahari za kutosha, nini kimekosekana kwenye nchi yetu? Je, wataalam wetu hawatushauri vyema? Au tumetanguliza siasa zaidi hata mambo ambayo yanahitaji utaalam? Ni vizuri tukajipima tuangalie shida iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisimama wiki iliyopita kuuliza Habari ya maji; Ziwa Tanganyika na kina chake, lakini kutoka Kilando kuja Namanyere ni kilometa 64 tunazungumza habari ya maji miaka nenda rudi, shida ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tumeanza kufikiria maji kutoa Ziwa Viktoria tumefikisha Tabora tufikiri mikoa hii mitatu, tufikir Katavi, tufikiri Rukwa, tufikirie Songwe hawa wote wanaweza kufaidika na maji kutoka Ziwa Tanganyika badala ya kutimia fedha kidogokidogo kwenda kuanzisha miradi ambayo haiwezi kutatua changamoto ya maji. Ni bora tukafikiria kitu ambacho tunaamini tunakwenda kumaliza changamoto ya maji na suluhisho ni kutumia maji kutoka Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Ziwa hilo Tanganyika ukiachana na kufaidika na maji tuna uvuvi pale. *Slogan* ya Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa ni Serikali ya Viwanda, tujulize tuna viwanda vingapi leo kwa ajili ya uvuvi kutoka kwenye maziwa yetu kama kweli tunachokisema ndio tunachokimaanisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba, Serikali imekuwa inakuja na *slogans* mbalimbali, lakini siamini kama *slogans* hizo zinakuwa zimeshirikisha kikamilifu wataalamu wetu na kama zinaweza kutekelezeka. Leo kama tunaweza kusimamia kwenye kilimo lazima tujue kabla hatujafikiri viwanda tunazungumzia *raw material*. Mashamba yapo, maeneo yapo, shida ni nini kwenye Serikali yetu ya Tanzani? Ni vizuri kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kumekuwa na ilani mbalimbali, kuandaa ilani ni jambo moja na kutekelea ilani ni jambo jingine. Tukianza kuzungumzia utekelezaji tunakuja kwenye mpango huu ambao tunausema. Na mpango lazima uendane sambamba na hiyo ilani ambayo mnakuwa mmeipanga ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ziwa Tanganyika pamoja na kwamba, hatujalitumia vizuri hilo eneo la Ziwa Tanganyika,

tuna-*share* zaidi ya nchi moja; tuna nchi ya Tanzania ambayo sisi tunamiliki kwa ukubwa zaidi, lakini kuna Kongo, kuna Zambia. Leo unapokuja na utaratibu wa kanuni juu ya wavuvi kutumia nyavu gani ni vizuri kabla ya kuja na hayo maamuzi mjiulize hizo nchi nyingine wanatumia nyavu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa Samaki hawajui kwamba, mpaka huu leo tuko Tanzania, kesho tuko Kongo. Inawezekana tunakuwa na sheria na kanuni ambazo zuinatuadhibu sisi wenyewe tunashindwa kutumia rasilimali tulizonazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo leo wakati tunafikiria viwanda tumewawezeshaje wavuvi wetu ambao wanaweza kutumia hizo teknolojia na kuwawezesha, sio kuwapa tu hizo kanuni na sheria kwasababu, lazima Serikali tujue tuna wajibu kwa wananchi wetu. Pamoja na kwamba, tunawaambia waende kutumia nyavu za milimita nane na hatujui zile nchi nyingine ambazo tuna-*share* kwenye ziwa moja hilohilo Ziwa Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tujiulize ni kwa nini wakati tunafikiri viwanda na kipaumbele chetu ni kuwaambia wananchi au wavuvi wetu watumie milimita nane tumejiwekeza kiasi gani sisi wenyewe kutengeneza hizo nyavu ambazo tunafikiri ni halali, ili tuweze kuwawezesha wavuvi wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inafikia mahali sio kila mvuvi ni mtaalamu, akienda dukani akauliza kwamba, hii ndio milimita nane, anapewa kwamba ndio yenyewe. Akifika kule, kwa bahati mbaya zaidi, Serikali badala ya kukamata kiwanda ambacho kinazalisha wanakwenda kwa mlaji wa chini kabisa ambaye hajui, yeye ameambiwa ni milimita nane anakwenda kutumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na miongoni mwa kanuni ambazo ni vizuri tukaziangalia kama lengo ni kuwasaidia wavuvi wetu na Watanzania, sisi hapa tunazungumzia milimita nane kwamba, ndio wakatumie kuvua Samaki, wavuvi hawa

wanatumia hizo milimita nane. Wakifika kule wakiwa wanavua samaki, wametega wale samaki, ile nyavu haizuii chini ya ile sentimita ambayo wanaitaka wao Serikali, unakuta Samaki wale wengine wamefuata. Kwa bahati mbaya zaidi watendaji walipo huko chini anapofika kwa mvuvi huyu badala ya kuangalia kwamba, ile nyavu ndio iliyosababisha sio mvuvi. Kwamba, ni kweli ni milimita nane, lakini Samaki waliongia pale labda wawili au watano, mvuvi anapigwa *fine* milioni mbili, milioni tano, milioni kumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yawezekana lengo la Serikali ni kweli ni kukomesha uvuvi haramu, lakini ni vizuri tukajua chanzo, ili tuje na suluhisho kama Taifa badala ya kuja na hizi *operations* ambazo hazieleweki, matokeo yake watendaji wamekuwa wamekuwa mahakama, wamekuwa ndio askari. Sasa kama tunataka hapa tunafikiri kwamba, namna gani sekta ya uvuvi imesaidia Taifa kwa pato, lakini tufikiri pia tunapotaka kupata pato kubwa tumeandaaje juu ya kesho? Hawa wavuvi tumewajengeaje mazingira rafiki, ili kesho tuendeleo tena kupata fedha zaidi kwa ajili ya kukuza uchumi wa Taifa letu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitarudi kwenye jambo ambalo ni la muhimu zaidi. Kwenye ileile ya kwanza kwamba, agenda za kitaifa. Kumekuwa na wimbo usioisha Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema Liganga na mchuhcuma, lakini limekuwa linazungumzwa halina majibu. Ni vizuri leo Mheshimiwa Waziri uje utuambie nini kimejificha kwenye hili jambo ili tuweze kujua tunachokizungumza. Kwasababu, kama jambo ni jema nini kinazuwia hili jambo lisitekelezeke? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika tuliambiwa tunaenda kwenye uchumi wa gesi. Gesi ya Mtwara imeishia wapi? Mje mtupatie majibu hapa nini kinaendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunaangalia zawadi nyingine ambayo Mungu ametupa Mkoa wa Rukwa, *helium*

gas, tunajua kwamba Serikali imefanya hatua mbalimbali, lakini tunataka kujua ukitazama kiuhalisia bado hatuko *serious* na uchimbaji wa gesi hii kuanzia miundombinu, kuanzia elimu kwa wananchi wanaozunguka eneo lile, tunataka tena mambo ya Mtwara yaje yajitokeze na Mkoa wa Rukwa. Ni vizuri tujipange vizuri na lengo ni jema, lile suala sio la Mkoa wa Rukwa ni suala la kitaifa. Makosa yaliyojitokeza iwe ni fundisho tunapoandaa jambo jingine kutokea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia, tumekuwa na utaratibu ambao tunatamani kumuokoa mtoto wa kike. Kumekuwa na mkanganyiko kidogo wa sheria zetu, sheria ya ndoa na sheria ya mtoto. Kwenye Mpango wa Miaka Mitano tunatamani akina Mheshimiwa mama Samia wengine, wajengewe mazingira rafiki ili tupate Marais wazuri wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kila sababu leo, natambua kwamba, sheria zipo, lakini kuna mianya ambayo bado watu hawa wanatumia kuwaumiza watoto wa kike. Ni vizuri tukalinda ndoto za watoto wa kike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeangalia kuna namna ambavyo Mkoa wa Shinyanga wameanza, pamoja na kwamba ndio walikuwa wanaongoza wakiwa na asilimia 59 kwa takwimu ambazo zimetokea 2006 nafikiri.

Mheshimiwa Spika, wale watu wamekuja na mikakati mbalimbali ambayo ni mizuri kuiga kama Taifa. Cha kwanza wamekuja na utaratibu wa kujenga shule ya *girls*, kwa maana ya kwamba wameamini mazingira pia yalichangia watoto wa kike kupata mimba za utotoni na ndoa za utotoni. Jambo hilo si baya kama likawa ni mpango wa kitaifa, kwamba kila Halmashauri angalau ikawa na shule moja ya *girls* ili tuone namna gani tunaweza tukalinda vipaji vya watoto wetu wa kike.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la kubadilisha vipengele hivyo ambavyo vimekuwa ndio uchochoro, yaani mtu amebaka, anafika pale mtoto wa kike anaulizwa

anasema ni kweli, wazazi walikubaliana lakini mimi nilikuwa nataka kusoma. Akija kwenye sheria hiyo ya ndoa wanamuuliza mlalamikaji kwamba wewe kuna taasisi ambazo zimejitolea kwa ajili ya kutetea haki za watoto wa kike, anapofika pale anaambiwa ulipoenda huko mpaka unataka kufunga ndoa ulikuta kwamba wameandaa sherehe kwa maana ya vyakula na nini anakubali kwamba ni kweli. Wanamwambia soma sheria ya ndoa ina maana kulikuwa makubaliano ya wazazi na ndiyo maana hatua hiyo ikafikia hapo.

Mheshimiwa Spika, bado bado narudi, pamoja na kwamba sheria tulitunga ndani ya Bunge kama lengo ni kumlinda mtoto wa kike, tufanye marekebisho ya sheria hizo ambazo bado zina mwanya ambao watoto wetu wa kike wanaendelea kuangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo hayo, namalizia kusema; kama kilimo tuna uwezo wa kulima Tanzania, kama uvuvi tuna uwezo wa kuvua zaidi kuliko maeneo mengine, tayari Serikali imewekeza kwenye Bandari mbalimbali ikiwemo Bandari ya Kagwe, tutumie Ziwa Tanganyika, kwasababu Mpango wa Serikali Awamu ya Tano ilikuwa ni kufua Meli ya MV Liemba; ile itasaidia kusafirisha minofu, kusafirisha mazao mbalimbali badala ya kupiga kelele habari ya soko. Leo Zambia wameanza kuchukua eneo la Kongo na sisi tupo jirani tunashindwa kutumia hiyo nafasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani. Mheshimiwa Florent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Kyombo.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.....

SPIKA: Dakika tano tano.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante niungane na wasemaji waliotangulia kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, lakini pia kuipongeza sana Serikali kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambao unaonekana ni taswira njema kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga hatua kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nijielekeze moja kwa moja kwa juhudi za Serikali ambazo kupitia mwongozo ulioletwa mwaka 2018, ambao ulikuwa ni mkakati madhubuti wa Serikali kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweza kutelekeza miradi ya kuchochea upatikanaji wa fedha ili ziweze kujitegemea na hivyo kutoa huduma sahihi kwa wananchi. Fedha hizo za kuwezesha miradi ya kimkakati ziliendelea kutolea na Serikali kutoka Serikali Kuu; na tumeona katika sehemu kubwa zimekuwa za tija na zimeleta matokeo chanya.

Mheshimiwa Spika, niseme katika maeneo ambayo miradi ya kimkakati imeweza kutekelezwa kwa ufasaha tumeona matunda mazuri, moja wapo ni ushahidi kupitia taarifa ya CAG. Jiji la Dar es Salaam kabla halijavunjwa kwa zile hesabu zilizofungwa tarehe 30 Juni mwaka jana lilikuwa na uwezo wa kujitegemea kwa asilimia 484; kwa hiyo maana yake lilikusanya Billioni 16 na lina uwezo wa kutumia Billioni tatu. Kwa hiyo tunaona kama tuna miradi mingine ya kimkakati, huduma za wananchi kama kujenga zahanati, kujenga vituo vya afya na Mengine kuchangia barabara kupitia TARURA jiji hilo lilikuwa na uwezo. Lakini siri ya mafanikio ilikuwa ni nini, ni uwezeshaji uliotoka Serikali Kuu, ni mbegu iliyopandwa katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa moja wapo ikiwa hilo Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tunaona sasa hivi mkakati wa Serikali unavyokwenda na katika bajeti hii inayokuja ni ushuhuda tosha, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeelekeza Mamlaka za Serikali zote 185 kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa kituo kimoja. Najua kupitia huu uwekezaji uliokwenda kule kupitia miradi ya kimkakati vituo hivyo vitajengwa; na baadhi ya

halmashauri ambazo hazijapata uwezeshaji huo inawezekana zikatekelezwa kwa kusuasua, lakini niseme ni mwanzo mzuri. Kwa hiyo tunachotakiwa kufanya ni nini? kwa kuishauri Serikali. Ni kukuhakikishia sasa huu mkakati ambao uliundwa madhubuti ambao umeanza kuonyesha matokeo chanya uendelezwe.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu kwa sasa haufanyi kazi ulisimamishwa na Serikali, na maelezo hayakuwa wazi kuonyesha kwamba umesimamishwa kwasababu gani na unaanza lini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe kwa kusema kwamba Serikali, kwa kazi nzuri ambayo tumeshaiona matokeo yake ni kwanini tusiwezeshe? Tukiziwezesha halmashauri hizi maana yake tunategemea sisi tunakuwa tunatoa maelekezo kwamba sasa mwaka huu kama nchi yetu kuna kigezo fulani cha kuanzisha miradi fulani weka katika bajeti zenu mradi moja, mbili, tatu unaweza kutekelezwa kwa ufasaha na tutaona maendeleo makubwa sana. Katika mwongozo huo kuna baadhi ya vitu ambavyo inatakiwa kama Serikali kuvifanyia kazi. Suala la kwanza vipo vigezo madhubuti 14 katika mwongozo huo, baadhi ni vizuri baadhi vinahitaji kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano suala moja wapo ni kuwa na hati safi. Tunaona kwenye taarifa ya CAG leo zipo halmashauri jumla 63 hazina hati safi, anayeadhibiwa ni nani? Ni yule ambaye alisababisha, kama mtaalam wetu au mwananchi? Kwa nini tunapeleka adhabu kubwa kwa mwananchi; ambapo Serikali ingeweza kupeleka fedha za kuwezesha miradi ambao utasaidia baade apate huduma tukamuadhibu kwasababu hana hati safi? Mwananchi hajui hati safi, hajui kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana Serikali, sisi wote ni waumini wa kuhakikisha fedha zinasimamiwa vizuri, kwa umadhubuti kabisa, lakini sasa suala hilo naomba tuliangalie kwa mapana, kama kuna hati ambayo sio safi

wale wawajibishwe lakini fedha ziendeleo kupelekwa kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Spika, wakati naendelea kumaliza dakika zangu zilizobaki kupitia meza yako hiyo nimuombe Waziri wa Fedha na Mipango. Zipo barua nyingi ambazo zimepelekwa kwake kwa zile halmashauri ambao zimeshakidhi vigezo. Moja wapo ni Wilaya ya Misenyi Jimbo la Nkenge ambapo ilipelekwa barua tarehe 4/09/2019 ya mradi wa maghala nane katika mpaka wa Mutukura kukiwa na stendi ndogo pamoja na jengo la biashara.

Mheshimiwa Spika, niombe, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, wakati unakuja kwenye bajeti angalau uweze kuhakikisha kwamba mradi huo ndani ya Wilaya ya Misenyi unaweza kutekelezwa. Tupo mpakani mwa Uganda mradi huo utaleta matunda ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, barua hiyo haina mradi wa Wilaya ya Misenyi peke yake, iko miradi mingine. Babati TC nao waliomba Bilioni 5.1 kujenga Stendi, kuna Meru DC nao waliomba Bilioni 10 kuna Lindi MC waliomba ujenzi wa Stendi 7.8 pamoja na Soko katika Manispaa yetu ya Lindi. Kwa hiyo niombe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: basi nikushukuru naunga mkojo hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo, nakushukuru sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Japhet Hasunga, na niseme kwamba pale kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu akishamaliza Babu Tale pale, nitaomba mtu mwingine yeyote asiende pale ili tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu kusikiliza hoja za Wabunge, la kwanza. La pili, mnafahamu bado mazingira yetu, si mnaelewa jamani, lazima tulindane

lindane, kwa hiyo ni vizuri kumvizia zaidi ofisini maana nimeona sasa foleni imekuwa inahatarisha hata Afya ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ule ukaribu; nini, na mkifika pale basi *well* mliobahatisha ni dakika moja, lakini Babu Tale ndiye wa mwisho, sitaki kuona kwenye kiti kile kuna mtu mwingine, na yeye afanye *short* ili Mheshimiwa Waziri Mkuu awasikilize Bunge. Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na nashukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono mazuri na hotuba nzuri aliyotoa ambayo imetoa matumaini makubwa sana kwa Watanzania na kuonyesha mambo mbalimbali ambayo tunatakiwa tuyasimamie katika kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mpango kwa kuja na Mpango huu wa Miaka Mitano ambao kwakweli umekuwa na majibu mazuri ya mambo mengi ambayo tunayahitaji kama nchi, na hasa nimepitia yale malengo yalivyoandikwa, shahaba za utendaji tulivyoziweka, basi nafikiri ni Mpango mzuri kama tukusimamia unaweza ukatufikisha mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, Mpango wowote ambao tunakuja nao lazima ujibu masuala mazito ya kitaifa ambayo tunaona kama Taifa ni changamoto; na moja ya jambo la kwanza ambalo ni changamoto sasa hivi ni umaskini ulio mkubwa kwa Watanzania walio wengi. Kwa hiyo katika mpango huu lazima tueleze namna gani tunakwenda kutatua umaskini huu ili Watanzania hawa sasa wakuwe na wawe ni wakulima wakubwa, wawe ni wafanyabiashara wazuri, wawe ni walipa kodi na ina maana tutakuwa tumeongeza idadi ya walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, tunalo tatizo kubwa la kitaifa la ajira, ajira isiyo rasmi na ajira ambazo ni rasmi. Kwa Tanzania sasa hivi watu tulio wengi uchumi wetu

ni uchumi ambao sio uchumi rasmi. Kama nchi hii haitupeleki pazuri. Lazima tuchukue hatua za dhati kuhakikisha tunajenga uchumi ulio rasmi ili tupate uchumi ambao ni imara na shindani.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuangalia dhana, teknolojia na tija katika nchi yetu, hili bado ni tatizo kubwa; hatuwezi kufika bila kuchukua hatua zinazostahili. Lakini la mwisho ni uongozi bora wenye maono na Rasilmali watu; hili ni eneo ambalo ni muhimu sana. Sasa nimeangalia katika *documents* zote tatu zinazotakiwa zihishwe ili zote zijibu haya tunayoyasema.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza ni Dira ya Taifa, dira yetu ya miaka 25 kuanzia 2000 mpaka 2025. Dira ile ina mambo matano ya muhimu ambayo tunatakiwa kuyafanya; na tutakapofika mwaka 2025, tunatakiwa twende tukapime, je Watanzania tumefikia kuwa na kipato cha dola 3000? na kama hatujafikia ni kwa nini? Hili lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ina vipaumbele sita na vimeandikwa vizuri sana. Vipaumbele vile kwasababu ya muda sitaweza kuvisema, ningetamani niviseme. Lakini unakwenda sasa kwenye mpango, mpango umekuja na vipaumbele vitano. Sasa tunaangalia ilani inasemaje, dira inasemaje na mpango unasemaje katika kutekeleza hivi vipaumbele. Nadhani tuna haja ya kuviangalia vizuri na tuhakikishe vyote vinatupeleka katika kwenda kufikia malengo tuliyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu walipa kodi wa kwetu wa nchi hii. Sasa hivi biashara nyingi Tanzania ni zile za wafanyabiashara wa chini na wale wa kati ndio walio wengi. Tunafanyaje sasa kuwasaidia hao wafanyabiashara wadogo wadogo? Kama vile boda boda, mama ntilie na wakulima watoke kwenye hizi biashara ndogo ndogo waende kwenye biashara kubwa ambazo wataweza hata kulipa kodi na wakachangia kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kuhusu wakulima wetu. Kilimo chetu hiki hatutaweza kutoka kama hatutaweza kuwahudumia wakulima wetu kama walivyo.

Mheshimiwa Spika, tatu wafugaji, lakini nne ni wavuvi na mwisho ni wachimba madini. Hivi vyote ni vitu muhimu sana, na ndiyo maana Ilani yetu, Mpango wetu huu wa Miaka Mitano useme ni namna gani tunaenda kufanya katika kuhakikisha sekta za uzalishaji zinaongeza uzalishaji. Mkazo katika huu mpango lazima uwe hizi sekta za uzalishaji, sekta za uzalishaji ndizo zitaleta fedha zitakazo kwenda kutumika katika sekta za huduma za jamii na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hasa sekta za uzalishaji ziko kama hivi zifuatazo; tuna kilimo, mifungo, uvuvi, madini, Utalii na Mazingira, Viwanda na Biashara. Sasa, mpango unatuambia nini katika kufanya haya? Tumeweka mikakati gani katika namna ya kwenda kuyatumia ili haya sasa yote yatupeleke kuhakikisha kwamba ikifika 2025 tumeshaingia kuwa nchi ya kipato cha kati lakini malengo yetu ni kuhakikisha nchi inakuwa ya kipato cha kati ambapo kila Mtanzania pato la kawaida iwe ni zaidi ya dola 3000? Sasa hili ndilo lengo tulilojiwekea miaka 2000 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninataka kusema tunatengenezaje hizi ajira? Tunawaondoaje hawa Watanzania hapa tulipo? Tunajengeje viwanda? Hii ya kuandika tutaandika vizuri sana na nimeona mipango ni mizuri, lakini tunajengaje viwanda kama ajenda ya kitaifa? Tuna mfuko wa kwenda kujenga? Na kama haya yahawezekani basi maana yake hatutaweza kuja kuyafikia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, Nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Hasunga ni mwenyekiti wa kamati ya PAC na mwenyekiti wako naye namuona yupo hapa, pamoja na LAAC, ninawaomba mje na mapendekezo ya namna mtakavyoshughulikia ripoti ya CAG kwa haraka kuanzia sasa katika Bunge hili. Kwasababu kwa kawaida huwa Bunge hili linaisha likishamalizika ndio tunaanza kuchakata taarifa ya CAG. Sasa tunataka safari hii tuanze mapema, *immediately*, ili Bunge linalokuja la Septemba Oktoba pale taarifa ya CAG iwe ni moja na inshu badala ya kuishughulikia Novemba tutaishughulikia Bunge la Mapema zaidi ya pale. Kuna umuhimu wa kufanya hivyo kwasababu baadhi ya watu wamejitokeza kupiga parapanda za uongo na upotoshaji na uzushi kwa kupitia taarifa hiyo; ilhali Bunge kupitia Kamati zake na Bunge lenyewe kwakweli ndio lenye *mandate* ya kuipitia na kuitafsiri na kuichambua taarifa ya CAG.

Si watu wengi wana uzoefu na uelewa wa kuchambua taarifa za *Ma-auditor*. Yapo maeneo mengi, sijui tuje tufanyeje, nafikiri ni moja ya kazi yenu PAC na wenzetu kutafsiri kidogo. Au sijui kazi ya CAG? Mtakaa wenyewe mtatushauri.

Yaani iko hivi panaweza pakawa na matumizi tuseme kujenga kituo cha afya milioni 500. Milioni 499 zimetumika vizuri kabisa, lakini milioni moja ikakosa kiambatisha Fulani. Kawaida ya ukaguzi wa wakaguzi wao wana *query* fungu zima la milioni 500; kwa hiyo wewe unayesoma mtaani unaona milioni 500 zimeibiwa kumbe pale ni milioni moja ambayo haina risiti. Akishapata hiyo milioni moja sasa ana li-*clear* lile fungu zima la milioni 500, ni masuala ya kahasibu. Sasa watu wababeba tu, mabilioni yameibiwa, nani kaiba wapi? Na hasa huyu yafiki yangu Freeman Mbowe alikuwa Ulaya, sijui wapi huko sasa katumwa na watu wake anakuja anapotosha mambo, nafikiri mmesikiliza hotuba za watu kama hao ambao ni wapotoshaji wakubwa. (Makofi)

Kwa hiyo, mtaianza mapema mnilitee mapendekezo ili tuangalie ratiba yetu inakaaje ili tuanze mapema na tuwaelimishe wenzetu kuhusiana na taarifa ya CAG ambayo

ni taarifa nzuri tu, lakini baadhi ya watu wanabeba na kupotosha mambo ambayo si sawa. Mheshimiwa Judith Kapinga atafuatiwa na Jumanne Kishimba. (*Makofi*)

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia na mimi ningependa nijielekeze katika mambo mawili. Tunapozungumzia maendeleo ya watu kwa kiasi kikubwa tunahusisha ukuaji wa uchumi, na tunapohusisha ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa tunaongelea mambo ya msingi sita; yaani uendelevu, uzalishaji, uwekezaji, mashirikiano, usalama pamoja na usawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa kwenye usawa ndipo ambapo ningependa nijielekeze kwasababu ni suala ambalo linahusisha haki na utu wa watu. Na tunapozungumzia maendeleo ya watu kwa kiasi kikubwa tunahusisha utu na haki za watu. Yaani lengo kuu la maendeleo ya watu ni uhuru na haki za watu; huwezi kutofautisha hayo masuala mawili.

Mheshimiwa Spika, nazungumza haya kwasababu uhuru na haki ya mtu unahusisha uhuru wa kipato. Tunapojadili mpango huu ni muhimu sana kuweza kuweka baadhi ya mambo sawa, ambayo yanashika uhuru wa kipato cha mtu; na uhuru wa kipato cha mtu mara nyingi unalindwa na Sheria na taratibu za nchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nijielekeze hapa kwasababu zipo Sheria ambazo zinakandamiza uhuru wa kipato cha mtu, inawezekana kukawa na changamoto, na hapa ningependa nijihusishe *specific* katika Sheria ya Uhujumu Uchumi, nafahamu imeongelewa sana lakini ningependa niweke mkazo hapa. Kwa ambao hawafahamu Sheria hii ya Uhujumu Uchumi na Utakatishaji Fedha ilikuja baada ya tukio la Septemba 11; pale ndipo ambapo Sheria hii ilisisitizwe iweze kuletwa katika mataifa ya Afrika na dunia kwa ujumla, ndipo na hapo sisi tukapata sheria hii. Lakini tulipokosea nchi nyingi za Afrika pamoja na Tanzania tulipata mapokeo ya sheria hii bila ya kuangalia mazingira yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, na vile vile tulipopata sheria hii hatari zaidi hatukuwa na uzoefu na kujadili ama kuendesha mashtaka haya, na hivyo tukajikuta tunapokonya haki za watu za dhamana, lakini vile vile tukapoka mali za watu kwa kudhania, kwamba sheria inaruhusu ilhali kimsingi ilikuwa labda ni tafsiri mbaya ya sheria ama sheria hazikukaa sawa ama matumizi mabaya tu ya nafasi pamoja na madaraka ya watu waliodhaminiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu makosa mengi katika sheria zetu za Tanzania yana dhamana; ukiangalia wizi, ukwepaji wa kodi ni makosa ambayo yana dhamana lakini ilivyokuja sheria hii dhamana ikanyimwa. Hata hivyo, watafsiri wetu wa sheria wametufelisha sehemu moja, makosa ya uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha ni matokeo ya makosa ya msingi yaani leo hii umeiba ama unatuhumiwa kwa ukwepaji kodi, mpaka ukwepaji kodi uwe-*establish* ndipo pale utaweza kujua, je, ukwepaji kodi ulisababisha utakatishaji wa fedha? Ndipo hapo unamhukumu mtu kwa kosa la kuhujumu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu makosa haya ya utakatishaji wa fedha ni vigumu sana kuya-*prove* wenzetu wa *DPP* wakaamua warahisisha Maisha. Moja, kwa sababu ni ngumu sana ku-*prove* sasa wanaamua pale kwenye kosa lako la msingi ambalo lina dhamana akuwekee na *money laundering* ili likose dhamana. Pili, kwa sababu halina dhamana utawekwa rumande sasa pale ndiyo wanakuja na *negotiations (pre-bargaining)* anakwambaia sasa hapa kuna shitaka hili na kwa sababu mashtaka haya yana sifa ya kukukalisha rumande miaka na miaka, mtu uko *frustrated* unawaza biashara zako, unawaza familia yako, unamuwaza mke au mume wako utakosa ku-*negotiate* ili uweze kutoka? Uta-*negotiate* tu na hapo ndipo ambapo watu wanapokwa mali zao kwa taratibu ambazo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema utaratibu huu ni unyang'anyi tu wa bila silaha, tunapokonya watu kwa taratibu ambazo zingeweza kutafsiriwa ili ziweze kurahisisha watu wetu walinde kipato chao na utu wao. Kwa

hiyo, haya masuala ya hii sheria, naomba sana Serikali yangu sikivu iangalie upya na inawezekana sheria haina matatizo ila tafsiri ya sheria kwa watendaji wetu iangalie mazingira ambayo tutalinda utu na kipato cha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo napenda nijielekeze nalo ni kuhusiana na masuala la mawasiliano na teknolojia. Inawezekana nikaonekana kama mlalamikaji lakini napenda nisisitize hapa. Kwanza napenda niishukuru Serikali yangu Sikivu, tulipozungumza masuala ya mabando ilisikia ikatoa maelekezo na tunashukuru sana. Hata hivyo, bado naomba Serikali iangalie masuala ya mabando ili wananchi waweze kujikwamua kiuchumi. Vijana wengi wanatumia huduma hizi, toka mwezi wa kwanza tunalalamika huu ni mwezi wa nne masuala haya hayajafanyiwa kazi, tunapewa tu matamko lakini vijana wengi zaidi ya milioni 23 wanatumia mitandao ya simu kwa ajili ya shughuli zao, tunaomba tuangaliwe. Unapewa MB 300 kwa Sh.2000 unafanya biashara, vijana huku ndipo tulipokimbilia kwa sababu mfumo wa elimu haujaweza kutusaidia. Sasa kwa mantiki kama hizi tunasaidiwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TCRA imetoa tamko kwamba ikifika Mei Moja vijana zaidi ya 90,000 wanaosajili *line* wawe wana vibanda, leseni na *T/V* namba. Anasajili *line* kwa Sh.1000 na anapata wateja kwa kusambaa huku mtaani leo hii unamwambia awe na kibanda wateja atapata wapi? *Airtel* inawalipa vijana hao zaidi ya shilingi milioni 700 ikilipa kima cha chini lakini inalipa mpaka shilingi bilioni 1 kwa vijana 30,000 lakini wanaenda kukosa kazi hawa. Naomba Serikali yangu iangalie mambo kama haya ili vijana wa Taifa hili wasiwe *frustrated* na mazingira ya kibiashara. Naomba Serikali yangu ituangalie sisi vijana ambao tunalipenda Taifa letu na tunafanya kazi kwa juhudi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunivumilia na kunipa dakika za ziada. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Judith Kapinga. Niliwaambia mtulie jamani madini yanateremka hapa leo,

nafikiri mnaona hapa. Ni mambo muhimu sana sina haja ya kuyarudia.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba (Profesa), una dakika 10 kwa sababu Mheshimiwa Cosato Chumi amejitoa, endelea Mheshimiwa.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami niungane na Wabunge wenzangu kuchangia Mpango huu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, nimeusoma Mpango huu vizuri sana lakini kuna mahali ambapo sipaoni pametiliwa umuhimu napo ni sehemu ya afya. Suala hili la afya kwa sasa sisi Majimboni ndiyo suala ambalo ni gumu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mwalimu Nyerere mpaka mwaka 1985 ilikuwa inatoa matibabu bure kwa raia wote wa Tanzania. Wakati huo tunafahamu vizuri labda tu kwa vijana, Serikali ilikuwa imefilisika baada ya vita vya Uganda lakini Serikali ilikuwa inatoa matibabu bure. Leo nikiangalia kwenye Mpango hakuna mahala ambapo panaelezea namna gani wananchi wetu wapatapa matibabu. Mheshimiwa Sunga ameeleza vizuri watu wetu kweli ni maskini na bei za matibabu na dawa mwananchi wa kawaida wa Tanzania hawezi. Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha afikirie kama anaweza kuongeza bei kidogo au shilingi 30/40 kwenye mafuta ili wananchi wetu tuwapatie matibabu bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu leo tunakusanya shilingi trilioni 2 na waliotuchangia hizi shilingi trilioni 2 ndiyo hawa, ni sahihi kweli mwananchi akienda hospitali akiwa hana pesa hakuna kitu chochote anaweza kufanya matokeo yake anaenda kukabiliana na kifo. Ni sahihi sisi Wabunge wote tunatoka Majimbo ambayo yana matatizo makubwa sana, hakuna Mbunge ambaye ametumwa nyama au sukari na wapiga kura wake labda Mheshimiwa Gwajima Mchungaji Kawe kwa kuwa Jimbo lake ni zuri kidogo lakini sisi kwenye Majimbo yetu hali ya umaskini wa wananchi

wetu ni mbaya. Kwa kuwa wananchi hawa hawana tatizo la nyama wala sukari, wanaipita nyama hapo wanaenda kununua mchicha bila hata malalamishi tatizo lao ni dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri ugonjwa ni kitu ambacho mtu hawezi akajisingizia. Sidhani kama hofu ya Serikali ya kutoa matibabu kuwa bure kama ina sababu ya msingi. Kwa sababu sidhani kuna nchi duniani ambayo iliwahi kutibu watu wake bure ikafilisika sidhani, haiwezi kufilisika. Duniani nchi zinafilisika kwa vitu viwili; ni vita na ujenzi, hakuna kitu kingine. Kwa mapato tuliyonayo, tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha afikirie ili tukawatendee haki wananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna hili tatizo la bima Mheshimiwa Waziri wa Afya yuko hapa, bima ni sawasawa na kamari. Tunaona Polisi kwa wachezesho kamari endapo mchezesho kamari ameliwa, akiwa hana pesa polisi wanakuja, vipi mtu aliye na bima anapokwenda hospitali anapoambiwa dawa hakuna kwa nini Mheshimiwa Simbachawene asipunguze *traffic* barabarani atuhamishie baadhi ya polisi hospitalini ili mgonjwa anapoambiwa na bima hakuna dawa aende akaripoti polisi. Kwa sababu *traffic* anahangaika na mtu ambaye hakufunga mkanda ana *Landcruiser* ambaye akimuona *traffic* anafunga akitoka anafungua lakini huyo ndiyo anakimbizana naye. Mheshimiwa Simbachawene tuhamishie baadhi ya *traffic* wawe hospitalini ili mtu akikosa dawa aende pale polisi ili anusuru uhai wake. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo panapohitaji usalama kabisa huku kwingine kote tunasumbuka. Usalama unahitajika pale mtu anapokuwa anaumwa, aende mtu polisi kawaida kama wanavyotetewa wacheza kamari itatusaidia. Sasa hivi simu zote tunazopokea Wabunge nusu ni kwa ajili ya dawa na matibabu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuwaombe pia wenzetu wa Wizara ya Afya, kwa nini hakuna *regulatory* kwenye hizi dawa na

matibabu. Tuna *EWURA* kwenye maeneo ya mafuta, tuna *TFDA* na *TBS*, kwa nini kwenye dawa pana kigugumizi na wakati dawa ndiyo kitu cha muhimu na cha mwisho kabisa kwenye maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, leo tumeshuhudia watu wana-*charge* dawa mpaka shilingi milioni 5, unaposema milioni 5 kwa mtu wa kawaida anazipata wapi pesa hizo. Vilevile tunaona sasa hivi ukiwa na bima ghafla wanakwambia tumeondoa hiki, wao ndiyo walipokea pesa, halafu wao tena katikati ndiyo walioamua kwamba ugonjwa huu tumeshauondoa na wewe umeugua na hauna kitu chochote, nafikiri hapo Mpango uangalie vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili la matibabu nafikiri hata mimi mwenyewe ningekuwa na maisha ya chini kule kijijini kwa hali iliyoko leo ni kitu kinahuzunisha sanasana. Tuwaombe Wizara ya Afya na yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri wa Fedha basi aruhusu hata bili za maji au bili za umeme ziwe dhamana ili mimi kama naumwa niende na bili yangu ya maji au umeme baada ya kupata ile hesabu ya hospitali wanigawanyie mle kidogo kidogo niwe nalipa pamoja na bili ya maji au umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naliongea suala hili kwa mapana kwa sababu hili suala linatusumbua sana. Unakuta mtu amepata matatizo unaambiwa kwamba huyu hana bondi ya pesa, hatuwezi kumtibu mpaka upate 300,000 za kuweka dhamana, je, huyo mtu anayesababisha kifo hiki kwa ajili ya pesa yeye siyo mhalifu kama wahalifu wengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna ubaya gani Serikali ikaweka utaratibu wa kukopesha wagonjwa kama inaona vigumu? Makampuni ya simu leo yanakopesha bila hata kumuona mtu mpaka shilingi laki tatu, Serikali yetu inaona ubaya gani kumkopesha mgonjwa matibabu? Atalipa tu maana tuna vitambulisho watu wote wanajulikana akopeshwe na baada ya mwaka kama itaona madeni yamekuwa hivi Serikali inaweza ikawafutia watu wake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hawa ndiyo wapiga kura wetu, haya mambo yote tunaongea kiingereza sijui nini, mimi naona shida kubwa. Kwa kuwa suala la elimu limeanza kujadiliwa, suala ambalo limebaki na mgogoro ni suala la afya. Tunaomba sana kwenye Mpango huu Mheshimiwa Waziri alifikirie sana. Tumeweka shilingi 50 kwa ajili ya maji tumeweka Sh.50 kwa ajili ya REA, afikirie kama anaweza kuweka hata Sh.30 kwa ajili ya afya. Wataalamu wa uchumi wanasema vitu au maisha yatapanda ni uongo. Bei ya nauli ya daladala leo ina miaka mitano haijawahi kupanda pamoja na bei ya mafuta kupanda, hata nauli za mabasi hazijawahi kupata, hata mafuta yakishuka hatuoni *impact* yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba wenzetu wataalamu wa uchumi wasije wakalivuruga wakasema sijui maisha yatapanda, maisha yapi, maisha ya Tanzania ...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnaona Maseneta wanavyo *argue point*, amekuja na *issue* yake leo ya afya na bima ya afya, dakika zake zote anazitumbukiza pale. Endelea Mheshimiwa. (*Makofi*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli wataalamu wetu wa uchumi wasije wakaleta yale matarakimu yao ya kusema ooh maisha yatapanda, uchumi wa Amerika ukiongeza bei ya mafuta ndiyo unapanda uchumi wa Tanzania hauna hata mahusiano.

Leo vijijini hata mafuta ya taa hakuna kuna *solar* kila kona, kwa hiyo, mtu asilete tena maneno ya uongo, hakuna. Hata kama mafuta ya taa yakipanda kule kijijini kibaba huwa hakibadiliki huwa kina bei ileile tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alifikirie kwani tutakuwa tumewatendea haki sana wananchi. Kweli tumejenga zahanati kila mahala lakini wananchi wanahitaji zahanati bila dawa? Maana kama mwananchi haponi, haoni thamani hata ya ile zahanati.

Mheshimiwa Spika, ni hofu bure tu, leo tunakopesha wanafunzi zaidi ya shilingi bilioni 600, kweli tunakataa kumkopesha mtu uhai? Ni suala ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatakiwa alifikirie kwa mapana kwenye Mpango wake. Hii itatusaidia sana na tutakwenda kule vijijini tukiwa kweli tuko huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Majimbo yetu yale ya vijijini hawana shida ya nyama wala sukari. Sisi kwetu kijijini ukinywa chai wanakuuliza leo unakunywa chai unaumwa? Hawana tatizo, ni haya ya mjini ndiyo yenye matatizo lakini sisi hatuna tatizo la sukari hata wanashangaa tunapolalamikia sukari. Kwa hiyo, tunaomba Waziri wa Fedha atufikirie sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ni kweli aisee, wakikuta una bakuli la uji halafu unawekewa sukari lazima mtu akuulize aisee unaumwa? Sababu kijijini hiyo ni *strange* kidogo. *(Kicheko)*

Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba kwa mchango wako wa leo. Tunaendelea na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Rais wetu, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amejikita katika kusimamia vizuri Serikali tangu alipoapishwa kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweza kutuletea hapa Mpango wetu uliowalishwa tarehe 8 na Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kujikita kwenye eneo la kilimo hasa kilimo cha ufuta. Kilimo cha ufuta kimekuwa kikifanyika kwa wingi sana maeneo mengi ya nchi yetu kadri siku zilivyokuwa zinakwenda hadi kufikia sasa. Ukiangalia kwa mfano katika Mkoa wa Lindi peke yake, katika mwaka 2020 zao la ufuta liliweza kuchangia au kuuzwa kwa thamani ya shilingi bilioni 110.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwa na changamoto nyingi kwa wakulima wetu kuhusiana na hili zao ambazo napenda sasa Wizara ya Kilimo inayohusika na zao hili basi iweze kushughulikia hizo changamoto ili hatimaye tupunguze umaskini kwa wakulima wetu wa ufuta lakini tuongeze tija katika uzalishaji na pia tuweze kukuza uchumi wa Taifa letu kutoka wa kiwango cha kati chini kuwa cha kati juu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la upungufu wa watumishi katika sekta hii ya kilimo. Naomba hilo lizingatiwe na Wizara husika ili tuweze kuona namna ambavyo tunaweza tukakuza zao hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna suala la mbegu bora, Serikali imeahidi kwamba itaendelea kuongeza uzalishaji wa mbegu bora. Naomba suala hili lizingatiwe kwa sababu imeonekana kwamba katika zao la ufuta kumekuwa na ongezeko pale mbegu bora zinapokuwa zinatumiwa. Mbegu bora ukilinganisha na zile za asili zimekuwa zikiongeza tija kwenye uzalishaji karibu mara mbili ya zile mbegu za asili. Kwa hiyo, naomba hilo eneo hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye eneo la vyama vyetu vya ushirika, kumekuwa na baadhi ya makarani ambao si waaminifu. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Kilwa katika Kata ya Miguruwe, wakulima 110 hadi hivi sasa tunapozungumza waliuza mazao yao mwaka 2019/2020 lakini mpaka leo hawajalipwa fedha zao. Fedha hizo zilipotelea kwa hawa makarani wa *AMCOS* na *TAKUKURU* waliingilia kati suala hilo lakini mwisho wa siku mpaka leo matunda hayajaonekana. Kwa hiyo, naomba Wizara husika ilisimamie.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna changamoto ya wanyamapori ...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo Mheshimiwa Francis anasoma kabisa yaani hana wasiwasi, hongera sana Mheshimiwa Francis. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na changamoto ya wanyamapori. Kuna Kijiji kule katika Kata ya Kandawale kinaitwa Ngarambeliyenga, kwa wale wasiofahamu ndiyo kule ambako yule shujaa wa Vita vya Majimaji Kinjekitile Ngwale alikuwa anaishi. Kwa hiyo, katika hiki kijiji kumekuwa na uvamizi mkubwa wa wanyama aina ya pofu na ndovu pamoja na Kata ya jirani ya Miguruwe. Kwa hiyo, naomba sana wenzetu wa Idara ya Maliasili watusaidie katika kudhibiti changamoto hizi sababu mpaka leo napozungumza wananchi wengi wamekimbia makazi yao lakini mazao yao yamekuwa yakiliwa na wanyama aina ya ndovu na pofu. Kwa hiyo, naomba sana Wizara inayohusika itusaidie.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa mifugo Wilaya ya Kilwa pamoja na Mkoa wa Lindi kwa ujumla kumekuwa na shida kubwa ya wafugaji wahamiaji, kwa sababu kwa asili Wilaya za Mkoa wa Lindi ni Wilaya za Wakulima. Kwa hivi karibuni tumewakaribisha wenzetu wafugaji katika Wilaya ya Kilwa peke yake. Katika siku za hivi karibuni imeingia mifugo zaidi ya 350,000, lakini huduma za ile mifugo zimekuwa zikikosekana. Kwa mfano kumekua na huhaba wa ujenzi wa malambo, majosho na hata watumishi wamekuwa wachache sana katika kushughulikia hii Sekta. Naomba hilo jambo lishughulikiwe.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa sababu ya muda. Nakushukuru sana Mheshimiwa Francis Kumba

Ndulane. Kwa kweli anasoma tena bila miwani. Nakushukuru sana. (*Kicheko/Makofi*)

Nilikutaja Mheshimiwa Esther Matiko, utafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Una dakika kumi. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naomba kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Ni dhahiri kwamba kitu na jambo la muhimu sana ambalo Serikali ingeanza nalo ni kushughulika na suala zima la mikopo ya Elimu ya Juu. Nimekuwa nikisema hili na nitarudia kusema tena kwa sababu tumeshuhudia wanufaika wa mikopo hii wanapata adha kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba Serikali inatakiwa kuwekeza kwenye elimu ambapo inatakiwa hata itoe elimu bure kwa watu wetu wa Vyuho Vikuu ili waweze kupata ujuzi ambao utaweza kutumika kwenye Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na hata wengine waende nje kama ma-*expert*, kama vile ambavyo tunaleta watu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ilivyo, Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Mwaka 2004 ambayo tuliifanyia marekebisho mwaka 2016 ni kandamizi. Hata kwenye ripoti ya CAG ametaja upungufu wa kisheria na kimfumo kwenye ukusanyaji wa haya madeni kwamba yanazidi uwezo ya walipaji. Tumependekeza na Waheshimiwa Wabunge wengi wameonyesha hii adha.

Mheshimiwa Spika, napenda kujielekeza na kuiomba Serikali ifanye marejeo; kufanya makato ya asilimia 15 ya mshahara ghafi wa huyu mfanyakazi ni kubwa sana. Tumesema mara nyingi hapa kwamba huyo mfanyakazi anakatwa asilimia 15 ya mshahara ghafi, anakatwa asilimia 10 ya mifuko ya jamii, anakatwa *Pay As You Earn*, anakatwa Bima, kuna wengine wana michango mingine, mwisho wa siku unakuta huyu mfanyakazi habaki na chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ile *penalty* ya asilimia 10 ambayo ameiweka baada ya *maturity* ya miezi 24 ni kandamizi. Ambapo amesema mnufaika baada ya miaka miwili kama hana kazi anatakiwa atoe shilingi 100,000/=, *short of that* anakuwa na *penalty* ya asilimia 10. Hii mikopo tunaipitisha humu ndani inaenda, *is a Revolving Fund*; kwa nini muweke hizi tozo kama vile ni riba za mabenki? Isitoshe wameweka na *six percent* ya kutuza thamani ya fedha (*retention*). Huku kote ni kumkandamiza mnufaika ambaye ni huyu mtoto wa masikini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu Serikali iangalie, hapa hatufanyi biashara, *after all* hii mikopo tunayotoa ni kodi zetu; hizi za Watanzania sisi masikini ambao tunatoa. Tuhakikishe: mosi, tunawapa Watanzania wote wenye hadhi ya kupata mikopo na wengi wao mayatima na bado wanafurahia masikini, wanapata hii mikopo. Hii mikopo iwe *reduced* kutoka *15 Percent* ije kwenye *single digit* 5 mpaka 8 ili tuweze kuwasaidia hawa Watanzania masikini. Kwa hiyo, ije sheria hapa, tumesema na tumeomba, wasipoleta natangaza rasmi, ninaandaa Muswada Binafsi wa Sheria wa Mikopo ya Elimu ya Juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kwenye Utawala Bora. Mmetaja hapa kwamba moja ya kiashiria cha utekelezaji wa mpango huu ni Utawala Bora. Hata hivyo ukiangalia kwenye Sheria ya Utakatishaji Fedha, kifungu namba 12, 13 na 14 vinatumika vibaya na vinakandamiza sana Watanzania hawa. Hasa tukichukulia mfano kifungu 12 (a) ambacho kinasema mtu yeyote ambaye atajihusisha na muamala ambao una viashiria vya utakatishaji wa fedha ama kwa kujua au kwa kutokujua anakuwa amekosa na anaenda jela.

Mheshimiwa Spika, ameeleza hapa Mheshimiwa Judith kwamba unakuta wengi wanakumbwa wanaenda bila dhamana. Inabidi tutambue kwamba uchumi wetu kwa Tanzania kwa asilimia kubwa unatumia fedha taslimu siyo *cash less*. *Is not a cash less economy*. Kwa hiyo, kama ni fedha taslimu, kwa mfano mtu anakuja kwangu, anataka

kununua nyumba, ana hela zake, nitajuaje kama hizi hela anataka kutakatisha fedha haramu ambazo amepata *somewhere else*?

Mheshimiwa Spika, au tukichukulia mfano wa kule kwetu Kijijini Nyanchabakenyi, huyu mtu amepeleka ng'ombe zake kwenye miradi ya Kenya, Mabera kule kwenda kuuza ng'ombe zake 80, anarudi na mfuko wa milioni 100, ikitokea amekamatwa anaambiwa anatakatisha fedha. Kule tunajua kwenye minada hatuna mabenki wala mawakala, hatuwezi kufanya *transaction* huko, lazima azibebe na akiwa na *knowledge* aje sasa aziweke kwenye benki; asipokuwa na hiyo *knowledge*, ataenda kuweka ndani kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba watu watoe fedha ndani wazipeleke kwenye mabenki. Ila akikamatwa anakuwa *liable* kwa *that*.

Mheshimiwa Spika, kuna mfano mwingine ambayo ni hai. Nilivyokuwa Segerea, kuna wadada walikuwa kule, wamekuja kwa kosa la kutakatisha fedha miaka saba. Wawili; kulikuwa kuna mtu aliyekuwa ni mfanyakazi wa umma, sitamtaja, kumbe amechukua fedha ya mishahara hewa huko, ana *girl friends* amewaingizia kwenye *account as normal transaction*. Hao nao wakakamatwa, wamekaa Segerea *seven good years*, pamoja na mke wake kwamba wametakatisha fedha. Wameachiwa muda siyo mrefu kama miezi mitatu nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii sheria ni kandamizi sana, lazima ifanyiwe *review* ili tusiweze kuwanyanyasa hawa Watanzania, tuwe na utawala bora tuweze kutekeleza huu mpango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine ni kwenye Sera ya Fedha na mifumo ya kibenki. Tunajua kabisa kwamba utekelezaji wa mpango huu na ushiriki wa sekta binafsi kwa kiasi kikubwa katika Taifa letu hutegemea Sera ya Fedha na mipango na mifumo yetu ya kibenki. Sote tunajua riba za mikopo kwenye mabenki yetu ziko juu sana; *sixteen percent*, nyingine

seventeen; hizi zimekuwa kandamizi ukilinganisha na nchi nyingine, unakuta ni *less than ten*; *single digit*; 3,4,5,6. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kikubwa kupitia Sera ya Fedha, Benki Kuu ilishusha kiwango cha dhamana kutoka 12% mpaka 6%. Cha ajabu mabenki yetu ya ndani yameshusha kutoka 17% mpaka 16.3% tu. Mbaya zaidi, hata kwenye mikopo ambayo ni *risk free*; kwa mfano, mikopo ya wafanyakazi ambayo marejesho yao yanatokana na mishahara, bado na wenyewe wanakatwa 16.5 *percent to 17 percent*. Huu ni ukandamizaji.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana, kama kweli tunataka utekelezaji wa mpango uende vizuri na kuweza kuhakikisha kwamba sekta binafsi inashiriki katika utekelezaji wa mpango huu, Serikali ihakikishe inaingilia kati na kuhakikisha kwamba viashiria vyote ambavyo vinapelekea kuwepo na hizi riba kubwa pamoja na kushushwa kiwango cha amani cha Benki Kuu kinapungua au mojawapo unakuta haya mabenki yanajiendesha, kuna gharama kubwa nyingine zinaweza kuepukika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia pia utolewaji wa mikopo ambayo haifuati utaratibu, inayoongeza kiwango kikubwa cha mikopo chechefu ambayo wanashindwa kui-*control*, kwa sababu mzigo unakuja kwa Watanzania hawa wengine wa chini. Kwa hiyo, ili tuweze kuwa na sekta binafsi nyingi na shiriki, napenda Serikali iingilie kati kuhakikisha kwamba riba za mikopo ya mabenki zinaenda chini.

Mheshimiwa Spika, kine ni usimamizi wa kodi. Tunajua kabisa kwamba haki ni wajibu. TRA wana wajibu wa kukusanya kodi, nasi wananchi tuna wajibu wa kulipa kodi, lakini kumekuwa na tatizo kubwa la muda mrefu. Malalamiko ya marejesho ya kodi ya ongezeko la dhamani, nina maana VAT. Kwa mfano, mwaka 2020 nilivyokuwa kwenye PAC, Kamati yangu ilitembea mashirika mbalimbali, madhalani ALAF; walikuwa wanalalamika wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 17.

Mheshimiwa Spika, nilivyokuwa nashiriki kwenye Kamati ya UKIMWI, taasisi mbalimbali zilikuwa zinalalamika kuhusiana na hii VAT kurejeshwa; na wakienda kuomba, TRA wana-order kwenda kukagua ili kuona kama kuna kosa lolote waweze kufidia zile fedha zinazodaiwa za Kodi ya Ongezeko la Thamani. Wakikosa kupata kosa lolote, wanaendelea ku-delay. Ukienda kukumbushia, wanakuja tena kukagua. Kwa hiyo, inaenda kwenye cycle hiyo, wanakutafutia kosa ili kuweza kufidia hiyo tozo la Ongezeko la Thamani. Hiyo siyo haki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine ni hili sharti la moja ya tatu ya kodi ambayo umekadiriwa. Ikitokea Mtanzania amekadiriwa; na kuna cases umekadiriwa shilingi bilioni tisa, umeweka pingamizi kwamba mliyokadiriwa sivyoo, wanakwambia, toa moja ya tatu. Moja ya tatu ya bilioni tisa is almost bilioni tatu. Unazitoa wapi wakati unajua labda hukuwa liable kulipa tu; kulipa labda shilingi bilioni moja au shilingi milioni 500 umeandikiwa shilingi bilioni tisa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi zote lazima ziweze kufanywa review ili tuweze kuwa na harmonization ya wawekezaji, kuvutia wawekezaji wengi waje Tanzania. Kwa hali hii hatuwezi kuvutia wawekezaji kuja Tanzania. Pia wale ambao wako kwenye sekta isiyo rasmi, hawatapata mvuto na mwamko wa kutaka kwenda kwenye sekta rasmi kama kuna bureaucracy hizi zinazoendelea katika mfumo wote wa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine na cha mwisho ni hili la Bandari ya Bagamoyo, limeshika kasi sana kwenye mijadala na ambalo lina tija kwa Taifa letu. Nadhani kama Taifa tujjuleze na tutafakari. Tuangalie kama project ya Bagamoyo is it viable? Ina tija? Kama ina tija, ni nini cha kufanyika? Tusikae na kuji-bide; naangalia mijadala mingi inaenda, ooh masharti yalikuwa makubwa na vile.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa lazima tuangalie, kama project ina tija, hatujabanwa kwamba twende na huyo mwekezaji. Tukiona project ina tija, tunaweza tukatangaza

tenda tena, kama kuna mwekezaji ambaye anaweza kuja kutaka kuchukua ile bandari kwa manufaa mapana; au Serikali tukaenda *through PPP* kuweza kujenga ile bandari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine nimejaribu tu kuangalia, narudia tena kusema, bado sijafanya tafiti ya kutosha. Ukiangalia Bandari ya Dar es Salaam, kwa mwaka ina uwezo wa *only seventeen million metric tons*, tunajenga *SGR*. Bandari ya Dar es Salaam pale ilivyo haina uwezo wa kupanuka zaidi, lakini kule Bagamoyo *already* zimeshatumika *twenty-seven billions* za Watanzania kulipa fidia. Kupitia *Special Economic Zone almost over thousand* viwanda vinatakiwa vijengwe kule.

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie tija, tufanye *cross benefit analysis*; tukiona kama Taifa kuwekeza Bagamoyo kuna tija, twende, hatujafungwa na huyo mnayemwita *the so called* Mchina. Tuna wataalam wa kutosha, waende wafanye tafiti za kina kule Bagamoyo, tukijenga bandari kama Taifa, tunaenda kupata faida ipi? Je, masharti yaliyowekwa kwa huyo mwekezaji wa mwanzo ambayo mmesema ni magumu, tuyachambue tuone masharti ambayo ni rahisi, tunapotangaza tenda sisi ndio tunashikilia ni yupi mwekezaji ambaye anakuja na tija akiwekeza hapa kama Taifa tutanufaika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kinyume cha hapo, una mamlaka na Bunge lako hili. Kama mikataba ipo, kuna Kamati Maalum ya Miundombinu, unaweza ukai-*task* ikaenda kufanya kwa niaba ya Taifa letu kuona kama huo mradi ni *viable* kwa Taifa au la.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Ni kweli kuna mijadala mingi kwenye mitandao na mambo haya yamepotoshwa sana, hasa kwa sababu nili-*comment*, basi

watu wamepata *a field day*, lakini ni upotoshaji mtupu mwanzo mwisho.

Meli za sasa hivi kubwa duniani ni viwanja vitatu vya mpira kwenda mbele. *Three hundred meters plus*. Hakuna meli ya *meter* 300 inayoweza kuingia Bandari ya Dar es Salaam, kwa sababu mlango wake ule ni mwembamba, ni mdogo. Bandari yetu inakuwa *affected* na kupwa na kujaa. Inatakiwa bandari ambayo haiwi *affected* na kupwa na kujaa ambayo sifa zote hizo Bagamoyo wanazo.

Waliokuwa wanawekeza kule hawakuwa Wachina peke yake, walikuwa na Oman, nadhani sijui ni *seventh five* kwa *twenty-five!* Wa-Oman hao ambao tumewakataa na hawa wameshaweka mkataba Zanzibar kujenga bandari mpya ndani ya siku 100 za Rais Hussein Mwinyi, *new brand!* Wa-Oman hao hao!

Kwa hiyo, hivi vitu, tunapochangia miaka mitano Mpango wa Maendeleo hakuna *feelings* yoyote kwa upande wa Bunge kama mnavyochangia. Nia ni njema, kuchangia kuona kwamba miaka yetu mitano twende vipi. *Nobody is carrying anybody*. Wala hakuna mtu anauza nchi hapa, hakuna! Kama alivyosema, siyo lazima awe wa kutoka nchi gani au nchi gani. *Canadian* kama ana *terms* nzuri, twende; Mmarekani, na kadhalika. Kuna vitu viwili; kuna umuhimu wa mradi huu, ni kitu kinajitegemea; *yes or no*; cha pili, mwekezaji awe nani? Nacho kinajitegemea, ambacho Serikali wenyewe wataangalia, wataamua. (*Makofi*)

Kwa hiyo, watu wetu wanapotosha kweli. Kama kawaida Watanzania wako wenye nia mbaya la, la, la, la, la, lah; wanapotosha kweli kweli hiki kitu, lakini bandari siku zote huwa ni *project* muhimu katika uchumi wa nchi. Ndiyo maana nchi kama Singapore, Dubai, sijui nani *whatever you name it*; kuwa na bandari peke yake kumechangia *a substantial amount of economic progress* katika nchi zile. (*Makofi*)

Nilishakutaja Mheshimiwa Jackson Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia huu mpango wa maendeleo kwa miaka mitano ijayo. Kwanza nashukuru wachangiaji wenzangu wengi wamezungumza katika maeneo mengi, lakini kipekee nataka kumshukuru pia Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Prof. Mkenda na Msaidizi wake kwa kazi nzuri wanaoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika michango yangu iliyopita nilikuwa nimezungumzia mambo ya kilimo. Kwa upande wa ugani nilizungumzia habari ya mbegu, habari ya utafiti wa udongo na pia habari ya soko. Nilipopata nafasi ya kuzungumza naye wiki iliyopita tukiwa tunakunywa chai, alinieleza kwa shauku kubwa sana ni namna gani ambapo ameweka bajeti kwanza kuhakikisha kwamba tunapata mbegu bora. Hiyo inatokana na kuwekeza kwenye maeneo ya umwagiliaji, kwamba katika maeneo yanayozalisha mbegu wanasema sasa watazalisha mwaka mzima, kwa sababu tunakwenda kuweka umwagiliaji. Kwenye soko akawa ananieleza kwamba mwaka huu tutafanya maonyesho ya bidhaa zetu China na Oman na mambo mengi alizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa udongo, alinieleza kwamba wanakwenda kununua vifaa kwa ajili ya Halmashauri 45 ili tuwe tunapima udongo. Kwa hiyo, kwa kweli kwa kazi hiyo nzuri nawapongeza, lakini baada ya hapo acha niendeleo na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii nimemsikia hata Mheshimiwa Rais akizungumza siku ile kwamba tunaweza tukapata pesa nyingi kwenye madini. Alizungumzia suala la Serengeti, lakini nchi hii ina maeneo mengi sana yenye madini ambayo Watanzania hatujafanya utafiti. Wazo langu nilikuwa nafikiri kwamba Serikali ingeweka bajeti ili tutengeneze kama kitabu ambacho kinaonyesha maeneo yote Tanzania. Tufanye utafiti ili tuandike na mwekezaji anapokuja aambiwe

ukienda Kalenga utapata madini haya. Kule Kalenga wazee wameniambia kama maeneo matatu muhimu, kwamba zamani tulikuwa tunachimba madini hapa; na kuna madini mengi.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naishauri Serikali, katika mipango yake tuweke alama (*marks*) kwamba eneo hili na hili unaweza ukapata madini haya, ili hata wawekezaji wanapokuja, ni rahisi sasa tukimpa kile kitabu, achague kwamba mimi nikawekeze Kalenga kwa sababu naweza kupata Shaba au Dhahabu. Kwa hiyo, hilo tulifikirie katika mipango ya baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna eneo la pili ambapo nimejihusisha kidogo katika utafutaji wa hizo wanazoita tunu na malikale. Nimewekeza fedha nyingi, lakini nimefanya katika kipindi cha miaka miwili nikakimbia. Hili eneo inaonekana ni muhimu sana na watu wapo wenye ushuhuda kwamba wamekuwa wakipata fedha na hizi tunu zipo. Sasa ushauri wangu, kuna mambo mawili kwamba ukienda Maliasili, wanataka ulipie ile leseni miezi mitatu mitatu. Sasa miezi mitatu mitatu hii, watafiti wengi wamekuwa wakifanya huko zaidi ya mwaka mmoja mpaka inaendelea hata miaka mitano au sita. Sasa inakuwa ni gharama kulipa laki tano tano kwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kwa sababu eneo hili lina watu wengi na wengi sasa hivi wanafanya na hawalipi hata leseni, kwa sababu wako huko porini, wanaona hii miezi mitatu mitatu ni gharama. Nilikuwa naishauri Serikali, wenzetu hawa wa Maliasili angalau wangeweza ku-charge hata kwa miezi sita sita ili kuwapa nafasi hawa watu wanaofanya utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, nimegundua kwenye huu utafiti wa tunu, kuna utamaduni wa Kijerumani katika mambo haya. Nikawa nawaza, kama hawa Wajerumani wanahusika, kwa nini Serikali isifikirie sasa kutafuta hawa wazee wa Kijerumani ambao wanaonekana wana ramani za haya mambo ya malikale, tukafanya *partnership*

kama tunaweza kutoa hizi tunu, basi wao wabakie na asilimia 40, sisi tubakie na asilimia 60. Ili sasa hili jambo liwe wazi, kwa sababu watu wanajitafutia tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina Ushahidi, kuna mzee mmoja ambaye nilikuwa nafanya naye utafiti, hata sasa nimemwacha *site*, mimi nimemkimbia baada ya kuona gharama zinakuwa nyingi. Anasema yeye alifanya kazi na Wajerumani na hiyo *scanner* anayoitumia katika kuangalia maeneo ambayo madini yapo, ni ya Kijerumani na alipewa na Mjerumani. Kwa hiyo, maana yake haya mambo yapo, lakini hayajawa wazi sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri katika eneo hilo nalo, tuone; kwanza, kupunguza hizo gharama za kulipia hivyo vibali na pili tuone kama tunaweza tukawatafuta hao Wajerumani ili tushirikiane nao.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa najaribu kuliangalia kwamba kwenye mashirika yetu ya Serikali *performance* yake imekuwa kidogo, lakini nikaja nikawa nafanya utafiti kujua kuna tatizo gani? Kwa nini kuna *performance* ndogo? Nikaliangalia kama shirika la *TTCL* ambapo mimi nimefanya kazi kwenye mitandao kwa miaka 20. Yaani hatujalipa nafasi, kama unamteua Mkurugenzi, basi mpe mamlaka ya kufanya maamuzi na kuweza kufanya maamuzi fulani hata kufanya *promotions*. Kwa mfano, kwenye mitandao tulikuwa tunasema, *we copy with pride*, kwamba ukionga mwenzako...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Mheshimiwa Sebastian Kapufi tafadhali, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba moja kwa moja nijielekeze eneo

la madini, niliwahi kuzungumza kwenye Bunge hili hapa eneo la madini pekee yake kwa maana ya nchi yetu ya Tanzania lina uwezo wa kuzibeba sekta nyingine. Nikilisema hili, niendeleo kusema mbele ya Bunge lako mimi ni mchimbaji mdogo wa madini, kwa hiyo naomba nielezee kile kitu ninachokifahamu.

Mheshimiwa Spika, acha madini mengine, acha *Tanzanite*, acha madini ya vito zungumzia dhahabu peke yake. Kupitia dhahabu kwa kupitia wachimbaji wadogo nishukuru kwamba Serikali imeboresha maeneo hayo tozo mbalimbali zimepunguzwa, sheria zimerekebisha, tunaweza kwenda mbali Zaidi. Nashukuru mara mwisho nimemsikia Rais wetu mpendwa akiongelea suala moja, leo unaweza ukawepo kwenye hifadhi, sikatai uhifadhi, lakini kwenye hifadhi kuna dhahabu, kuna almasi, kwa kupitia almasi hiyo, kwa kupitia dhahabu hiyo, tuna uwezo wa kufanya mambo mengine. Tembo hali dhahabu, kwa hiyo unaweza kwa kuitoa dhahabu tukajenga mahospitali, kwa kutoa dhahabu tukawaendeleza akinamama.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili pia naomba ulifahamu vizuri ninachokiomba sasa hivi, tafiti mbalimbali ambazo sekta imekuwa ikizifanya, tafiti hizo ziendee kwenda huko mbali. Kuna watu hapa wanatuangalia wachimbaji kama labda watu wa kupiga ramli hivi na mambo mengine ya namna hiyo, hapana. Tukiwa na tafiti kwa kupitia *GST* hakuna uchawi, ni suala tu la kujua kiwango cha mashapo, kujua dhahabu iko wapi, unachimbaje, kwa hiyo niombe na katika hili nafahamu kuna maeneo ambapo Wizara kwa kupitia Wizara ya Fedha, wameendelea kutoa ujenzi wa vituo mahiri. Niombe sana ili tuendeleo kupata zao hasa kwa maana ya zao la dhahabu, bila tafiti, unaweza kushangaa leo umekaa hapa Dodoma dhahabu mtu anachimba choo kapata dhahabu, mtu amekwenda shamba analima kapata dhahabu maana yake kama ni kwa kupitia tafiti hatufanya kwa kubahatisha kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, niseme, katika eneo hili leo sehemu ambayo inaisadia nchi katika eneo la ajira ni pamoja na

uchimbaji. Nikilisema hili namaanisha, unaweza ukakuta sehemu ya mgodi mmoja idadi ya watu kama wale wangekuwa barabarani ni tatizo kwa nchi. Kwa hiyo ninapozungumzia habari ya kwenda kuimarisha huko namaahisha.

Mheshimiwa Spika, kubwa tuende kwenye jambo lingine. Leo kwa mfano, maeneo mengine kwa mfano kama Mkoa wa Katavi unaweza ukachimba ukapata dhahabu, ile dhahabu ni asilimia themanini tu, ukienda kuuza wanakuambia madini yako ni asilimia themanini, Serikali iende mbali Zaidi, tukisema themanini ina maana hii ishirini ni kitu gani, unakuta ni madini mengine yanaweza yakawa madini ya fedha, yanaweza yakawa madini ya shaba. Kwa hiyo Serikali itusaidie, watu wanajenga viwanda vikubwa, leo teknolojia iko wazi, maana yake huyu mtu mmoja anapoteza hayo madini mengine, lakini kama Serikali itakuja na utaratibu kwamba bwana nyie wachimbaji kadhaa mji-*organize* najua mipango hiyo ipo, lakini twende mbali zaidi kwa maana huyu mtu ukimsaidia hapahapa nchini katika kuchimba madini yake, hiyo dhahabu yake, baada ya kuiuza nje kama madini ghafi, tukilifanya hapa nchini mbali ya kuuza dhahabu tu anaweza akauza na madini mengine, yawe madini ya shaba au yawe madini ya fedha. Naomba sana Serikali yangu sikivu iweze kuliangalia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia eneo hilo hilo la uchimbaji kwa maana ya teknolojia, leo nilisema hapa, zamani tulikuwa tukiwaona akinamama kama ni watu ambao hawawezi wakajikita katika eneo hilo la uchimbaji, wakifikiri kwamba ni kazi ilikuwa inahitaji nguvu zaidi na watu wenye misuli Zaidi. Serikali ina nafasi ya kufanya jambo moja, niwaombe turudi kwenye kuwapa ruzuku wachimbaji, nikisema hilo namaanisha kwa kupitia ruzuku, fedha iliyojificha huko itatoka na itaendeleza maeneo yetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Nakushukuru sana na Mungu akubariki. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi, mchimbaji miongoni mwa *fraternity* wa Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Halima Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza niungane na hoja ya mwisho ambayo amezungumza Mheshimiwa Matiko kuhusiana na Bandari ya Bagamoyo, lazima ifanywe uchunguzi wa kina wa kimkataba ili kama mkataba uliopo huko kwa lugha ambayo hayati Magufuli alizungumza ambaye alikuwa ni Rais *highest authority then*. Kwa hiyo, niungane na wewe kwamba lazima kama Taifa, tutulie, tuweze kufanya uchambuzi wa kina, tuje na kitu kitakachosogeza Taifa mbele, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa nini, majuzi CAG kazungumza kuhusiana na ATCL, nimesoma hapa kuhusiana na usafiri wa anga, taarifa Mheshimiwa Mwigulu, anasema tulikuwa tuna ndege moja katika utekelezaji huu wa mpango, sasa hivi tuna 11, lakini tulivyokuwa ndege moja miruko ya ndege ndani na nje ilikuwa 225,000 mwaka 2015, maandiko ya Waziri wa Fedha. Tulivyokuwa na ndege 11 miruko imekuwa 292,105 ndani ya miaka mitano. Kwa hiyo tumetoka ndege moja kuja 11 katika kipindi cha miaka mitano tulichofanikiwa ni miruko yaani ndege kuruka ni elfu 67 pekee. Sasa vitu kama hivyi vinakupa swali ama tathmini ndogo tu. Naomba tuangalie abiria waliosafiri walitoka 4,207,000 mpaka 4268,000, ndege moja *as against* ndege 11, maandiko ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa kama kulikuwa kuna walakini atakuja kuyasema yeye.

Mheshimiwa Spika, wakati tunahoji uwekezaji wa fedha kwenye shirika la ndege sio kwamba tulikuwa hatutaki shirika letu lifufuliwe, tulisema uangaliwe upungufu ambao umezungumzwa na wataalam. Wakati tunatoa fedha mara ya kwanza 2016, mara ya kwanza tumetoka kwenye ripoti ya CAG Utoho wakati huo, ameelezea masuala ya msingi zaidi

ya 15 juu ya ubovu wa *ATCL*, akapendekeza yafanyiwe kazi kwanza, hatukuyafanyia kazi tukaanza ku-*inject five hundred billion*, miezi mitatu kabla ya taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hazina akaenda akatoa taarifa *PIC*, akasema shirika hili hali ni mbaya, halina mpango wa biashara, kama uliandaliwa ulikuwa ni wa kukurupuka, haina mpango wa uwekezaji kama ulikuja kuandaliwa ulikuwa ni wa kukurupuka, halina mahesabu, halijafanyiwa mahesabu; hali ya shirika haijulikani kwa sababu hakuna ukaguzi wa kimahesabu uliofanywa. Tumezungumza hapa kama ndugu zangu kama nyie hapo wakapiga makofi wakasema hewala.

Mheshimiwa Spika, *CAG* Profesa Assad ripoti yake ya kwanza, huyu wa juzi amesema hasara ya miaka mitano, Profesa Assad ripoti yake ya kwanza baada ya kuteuliwa kuwa *CAG* alisema shirika limepata hasara kwa miaka kumi mfululizo. Sasa Waheshimiwa Wabunge, tukiwa tunapanga vitu kwa ajili ya Taifa hili, tuangalie namna njema ya kulisaidia. Leo hii ripoti ya juzi...

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Taarifa ipo upande gani? Sawa, nimekuona.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, tunapokuwa tunajaribu kuangalia *performance* ya shirika la ndege mara nyingi sana huwa hatuungalii *number of tourists* ambao wamesafiri kutoka sekta moja kwenda sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, tunapajaribu *performance* ya shirika la ndege mara nyingi tunajaribu kuangalia *amount of money which has been spends by the tourists* katika sekta moja mpaka sekta nyingine katika kipindi cha mwaka. Kwa mfano, sisi Tanzania tunajua katika kipindi cha mwaka 2015 tuliweza, watu waliweza kuja na kutumia fedha walitumia fedha dola milioni moja, milioni mia tisa na ishirini na nne

mwaka 2016 dola bilioni mbili milioni mia moja arobaini na tisa mwaka 2017 dola bilioni mbili, milioni mia mbili na sitini na tano elfu, mwaka 2018...

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, sasa nilichotaka kuwa kusema ni kwamba tusije kupoteza Taifa...

SPIKA: Ahsante. Taarifa inakuwa fupi.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, ahsante

SPIKA: Ahsante sana, nafikiri umeeleweka. Unaipokea taarifa Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Tatizo la hawa manjuka, ndio maana nawaambia watulie, unajua ukiwa *form one* inabidi utulie kwanza. Nimesema hapa kwamba hakuna anayepinga shirika la ndege kufanyiwa ama kuwekewa fedha, hakuna anayebisha...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, kuna kauli ameitumia Mbunge mwenzetu ya njuga, sasa sisi wengine tunatoka kijijini, sijui njuga ni nini, hatuelewi labda afafanune.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa...

SPIKA: Haina shida Mheshimiwa Msukuma unajua yeye ni darasa la saba, sasa hii lugha hawezi kuielewa kidogo. Endelea Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru njuka ni *form one*, sasa Msukuma si unajua ameishia darasa la saba mwanangu. Kwa hiyo njuka ni *form one*, hukufika kule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachofanya hapa, ni kujaribu kusaidia yaani huwa nawaambia watu sisi ni Watanzania, tunaishi Tanzania, pasipo kujali umetoka chama gani, yaani vyama ni njia ya kusaidia Taifa, kwa hiyo tukizungumza tusionane maadui.

Mheshimiwa Spika, ninachosema taarifa ya Kichere ambayo watu wanajifanya wanaifanya rejea na wengine kutoka huko sio mambo mapya. Yalizungumzwa CAG Bwana Utoh aliyazungumza, CAG Profesa Assad, tena Profesa Assad aliyazungumza kipindi ambacho ndio tumekuja hapa na Serikali inatuambia jamani tutenge bilioni mia tano, tunafufua ndege. Kazungumza hapa Mheshimiwa Aida, ni muhimu *as a nation* tuwe na vipaumbele vinavyo tu-*guide* ili CCM ikichukua sawa, ACT ikichukua anakuwa *guided*, CHADEMA ikichukua anakuwa *guided*. Sasa leo tunapanga kipaumbele kilimo, kesho *Alhamdulillah* Mheshimiwa Jenista anakuwa Rais, anakuja hapa anasema, mie nadhani nilikuwa napenda sana ndege nilivyokuwa mtoto, hapana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuweke kuji-*guide*, tutafanya mambo na kuweza kuyamaliza ndio hoja waliokuwepo wanajua kama sio wanafiki, suala la ndege halikuwa *priority* namba moja, *you know it*, tulikuja tu tukalichomeka, leo tunaambiwa *trillion 1.2* zimemwagika, CAG anatuambia shirika lina madeni ya bilioni 412, *this is...*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, taarifa

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa nilikuwa ninaishauri Serikali na namshauri Waziri wa Fedha...

SPIKA: Mheshimiwa Mpembenwe tena, Mheshimiwa Halima kaa, kuna taarifa.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, pamoja na u-*form one* uliyepo, nataka kusema tu sisi Wabunge tusijekupoteza wananchi. CAG sisi ndio tumempa kazi na kazi tuliyompa ya kwenda kuangalia mashirika tofauti, hasara iliyokuwa imepatikana, naomba nimpe tu taarifa mzungumzaji ni kwamba, shirika ambalo lina-*operate* kwa hasara kubwa sana Afrika kwa sasa hivi ni shirika letu ambalo ni majirani zetu hapo karibu wa Kenya, lakini kwa nini hawapigi kelele kuna sababu.

Mheshimiwa Spika, kwenye *economics* kuna kitu kinaitwa *complimentary goods*. Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati amechukua maamuzi ya kununua ndege hizi tafsiri yake ni kwamba alikuwa anaenda ku-*compliment* na sekta nzima ya mambo ya *tourism* na ndio maana *tourism* sekta kwetu sisi imepanda sawasawa na watu wa Kenya *tourism* sekta ilivyokuwa imepanda japokuwa wanapata hasara. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Halima, pokea taarifa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nafasi za uteuzi zimejaa. CAG ameambiwa aseme ukweli kulisaidia Taifa, CAG amesema shirika la ndege halifanyi kazi vizuri, lazima tuliangalie, tuangalie watu wameshauri nini, ndege zishakuwa hapa, hatuwezi kusema tukazitupe ama kuzichoma moto, tuangalie kwa makini tujirekebishe pale tulipojikwaa.

Mheshimiwa Spika, tunasema haya kwa nini? Unajua, nilikuwa nasikiliza hapa Wabunge wachanga, tunakaa tunajiaminisha eti miradi tunajenga kwa hela zetu za ndani *my friend* nchi yenu inakopa, kukopa sio tatizo, lakini kopa wekeza kwenye miradi ambayo...

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Namtafuata anayesema taarifa

MHE. ELIBARIKI I. KINGU Nipo hapa, Kingu.

SPIKA: Haya bwana endelea, Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango mzuri wa dada yangu hapa Halima, lakini naomba nimpe taarifa ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *most ya carrier* za mataifa mbalimbali hasa kwa Afrika, kazi ya mashirika ya ndege mengi duniani ukisema ripoti za shirika linalosimamia mashirika ya ndege duniani, kazi kubwa ya mashirika ya ndege duniani ni kuchochoa uchumi mwingine, si lazima kutengeneza *profit*.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda na *mentality* ya kutegemea *ATC* siku moja itengeneze faida tukataka ku-*discourage* juhudi zilizofanywa za kufufua shirika la ndege tutakuwa hatulitendei haki Taifa la Tanzania. Natoa mfano, Kenya *Airways* mwaka 2016 na 2017 ilirekodi *loss* ya dola milioni 249, mwaka uliofuata wa 2018 wakapata *loss* kutoka dola milioni 249 kwa asilimia 51 zikaenda dola 97 milioni, hasara. *South African Airways...*

SPIKA: Malizia taarifa yako.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, *South African Airways* mwaka 2017 shirika la ndege la *South Africa* lili-*accumulate loss* ya dola milioni mia moja hamsini na tatu, lakini uchumi mwingine kwa mashirika haya ulikuwa unachochozewa. Naomba tusibeze juhudi za kufufua *ATCL*.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Ahsante kwa taarifa, nafikiri ataipokea taarifa

SPIKA: Mheshimiwa Halima taarifa hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, ninavyomwona *senior* naye anaingia humohumo, unakuwa unaona kwamba naye dogo anataka kupotea.

Mheshimiwa Spika, ni hivi ndege tukianza kuzungumza katika zile ndege zilizo-*park* pale *airport* tukiuliza tu kati ya hizo nane zilizopo au 11, ngapi zinaruka tutaanza kupotezana. Wamenunua ndege, hawana *business plan* zina-*park* pale. Kwa hiyo ndege ziki-*park* kama hasara kama hii inazungumzwa, lazima mtoe *justification* kwa nini hasara kama hii inapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tusitake kwenda huko wala tusipotezeane muda, wataalam waliochaguliwa na Rais wamesema tumekurupuka kwenda kudandia treni kwa mbele wakati hatujajiandaa, hilo ndilo tatizo. Inawezekana tungejiandaa, sisi tungekuwa ni mifano yaani Kenya ingekuwa inaturejea sisi, *South Africa* ingekuwa inaturejea sisi, yaani wewe unajivunia vipi kuanza kufanya rejea *failures*, yaani unajivunia vipi, kwa nini usijivunie kwamba umejipanga vizuri wale *failures* wanakutumia wewe kama rejea. CAG amezungumza, mama Samia amesema, CAG funguka, maana yake mama Samia kawaambia na nyie fungukeni, acheni unaa, tulisaidie Taifa.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Jamani amebakiza dakika mbili, nafikiri amalize dakika mbili zake sasa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, dakika mbili.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa linakua kwasababu, kwa makusanyo wanayokusanya *TRA* tunaweza kufanya mambo makubwa matatu; tunaweza tukalipa deni lenyewe, tunapitisha hapa trilioni nane mpaka kumi, tunaweza tukalipa mishahara watumishi kwa mantiki ya *wage bill*; tunaweza tukalipa *OC* – matumizi ya kawaida ya ofisi ili watu waweze kwenda ofisini. Ukiacha mambo makubwa hayo matatu, *TRA* ama sisi kama Taifa kama kuna salio linabaki labda trilioni moja, tukijitutumua sana trilioni mbili. Kwa hiyo mkija kupitisha hapa trilioni 36 mjue kwenye 36, 22 ndiyo tuna uwezo nazo, 12 tunakopa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuzingatia kwamba miradi yetu ya maendeleo tunaendesha kwa mikopo ndiyo maana tunatoa mapovu hapa. Tufanye vitu vyenye tija. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninyi mnajua wakati Dkt. Magufuli anaingia mwaka 2015 – Mungu amlaze mahali pema peponi Mheshimiwa Rais – deni la Taifa lilikuwa *41 trillion*. Now, Ripoti hii ya *BOT* ya Februari, 2021 deni la Taifa ni trilioni 71, *public and private*. Kwa mantiki hiyo – msije mkasimama hapa mkaanza kusema tunajenga kwa hela zetu, hakuna hela, tena tunakopa mikopo ya biashara. Kwa hiyo, kila jambo tukilipitisha hapa tulipitisha kwa wivu mkubwa kwa kuangalia kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana, kengele ya pili hiyo. Ahsante sana. Mheshimiwa Edward Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii nichangie mpango huu. Kwanza nimpongeze sana Waziri wa Fedha kwa umahiri wa ku-*present* mpango huu. Katika kusoma mpango huu ziko baadhi ya taarifa ambazo ndiyo zinaongoza mpango huu. Moja ni Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, nyingine ni Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, nyingine ni hotuba mbili za Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, na Mungu amlaze mahali pema peponi; nyingine ni Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2020 na nyingine ni *Agenda 2063*. Lakini muhimu kuliko yote ni Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025, hii hapa.

Mheshimiwa Spika, kama kuna ilani bora ambayo imewahi kuandikwa kwa utaalum mwingi sana na kwa lugha nyepesi sana ambayo Watanzania wanaifahamu ni Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2025. Na kama kuna zawadi

ametuachia Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, ni ilani ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili mkitaka heshima kwa Watanzania, na *legacy* ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ni kuleta mpango unaotekeleza ilani ya miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunatafuta kura, nimenunua ilani hizi na nimewapa wananchi wangu, nimewaambia wasome; Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji. Kwasababu miradi ya kimaendeleo ipo. Kama Bunge hili linataka heshima kwa Watanzania tuisaidie Serikali kutekeleza ilani hii kwa asilimia 100. Na sisi tutakuwa tumejenga heshima kubwa sana kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa wale ambao walikuwa Chato, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alisema hivi; mwanasiasa kwa *level* ya Urais ukichaguliwa miaka mitano ya kwanza unafanya bidii ile miaka mitano ili uchaguliwe tena, lakini miaka mitano ile mingine ya mwisho unaacha *legacy*.

Mheshimiwa Spika, ilani hii ina tafsiri zote mbili. Ni *legacy* ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kama tutakuwa tumetekeleza kwa asilimia 100. Lakini vilevile kwa lugha ya kisheria, ni *fast turn* ya Rais mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama tutawekeza nguvu kutekeleza ilani hii kwa maana ya *fast turn* ya Mheshimiwa Rais wetu na *legacy* ya Dkt. John Pombe Magufuli, maana yake mpango huu tunatakiwa tu-*double* katika kuleta utekelezaji wa namna ya kutekeleza ilani hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukizungumza mambo ya kilimo, mimi nilikuwa naongea na wataalam wangu wa Wilaya ya Kiteto hapo. Kati ya hekta 1,000 walizowekeza kwa ajili ya umwagiliaji, ni hekta 15 tu ndiyo zinatumika. Na nilizungumza na Mheshimiwa Bashe hapa, *excellent*, alinishauri tulete

andiko la mradi ili tuweze kuongeza hekta zile kwa ajili ya umwagiliaji, na tumeshaandika Mheshimiwa Naibu Waziri, *the ball is on you*.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachotaka baada ya miaka mitano wananchi wale, Watanzania wale waliokuwa wanalia siku ile waweze kufuatilia ilani yao na kila kitu kilichosemwa kiwe kimetekelezwa kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, ilani hii inazungumzia barabara mbili kuu nzuri sana; Barabara ya kutoka Kongwa – Kiteto – Simanjiro mpaka Arusha, kilometa 430, ni mikoa karibu minne; Dodoma, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Unaunganisha mikoa minne, ni uchumi. Najua barabara hii iko kwenye ilani hii, lakini sasa tuweke vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Tanga – Kilindi – Kiteto mpaka Singida, karibu mikoa mingine mitatu. Tulete sasa mkakati wa namna ya kutekeleza ilani hii ili wananchi hawa, Watanzania hawa waweze kusema *legacy* ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imetekelezwa kwa imani kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia na kitu kimoja alichosema Mheshimiwa Rais wetu juzi. Kuna *concept* inaitwa ya Serikali moja, ambayo sasa naomba Mawaziri wasikilize vizuri sana; sisi Halmashauri yetu ya Kiteto kwa mara ya kwanza baada ya mvua za miaka miwili hii tumepata maji mengi sana na tuna Samaki sasa na wafugaji wameanza kula Samaki sasa. Na wilaya yangu imetengeneza kama *source* ya mapato kwamba ni pato jipya, wameanza kutoa leseni. Anakuja Wizara ya Maliasili na Utalii anasema ninyi mmepewa leseni lakini hamruhuswi kuvuna; *concept* ya Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu ishughulike na hii *concept* ya Serikali moja. Kitu ambacho wananchi hawataki kusumbuliwa kabisa ni Wizara moja inakupa leseni moja halafu mwingine anatoka anasema

haiwezekani, hiyo *confusion* tuondoe. Tukiondoa hiyo wananchi wetu watakuwa wamenufaika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ahsante sana.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa ambaye nitamtaja wakati huo ukifika.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji mzuri. Baada ya kumpongeza niombe nijikite katika sehemu mbili, moja ikiwa sehemu ya viwanda na ya pili ikiwa sehemu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na miundombinu. Awamu ya Nne ya Serikali yetu iliyopita ilifanikiwa sana katika kuhakikisha kwamba inaunganisha barabara katika kila mkoa ili kuhakikisha kwamba huduma za maendeleo zinapatikana kwa wananchi, lakini pia kupunguza gharama za maisha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ile ya Awamu ya Nne iliamua kujiwekeza katika chombo kinachoitwa *TANROADS*. Katika kujielekeza katika chombo cha *TANROADS* tuliweza kufanikiwa kuunganisha mikoa mingi, na wote ni mashahidi, mikoa mingi sasa inafikika kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi wetu ni lazima sasa Serikali ione kwa namna gani ambavyo *TANROADS* wanapata asilimia 70 ya fedha lakini tuna chombo kingine ambacho tumeamua sasa kuboresha kwa maana ya barabara za vijijini, chombo kinachoitwa *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, na tukiweza kufanikiwa kuiboresha *TARURA* tutafanikiwa kufungua barabara zetu za vijijini na

tutarahisisha huduma. Huduma ya kwanza tutakayoweza kurahisisha ni huduma ya pembejeo na kuwasaidia wakulima wetu kwasababu tunalenga uchumi wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuombe sasa kwa kuwa *TANROADS* sasa hivi wamebaki kuunganisha maeneo machache lakini pia maeneo yao makubwa ni kuangalia marekebisho pale ambapo panaharibika. Kwa maana hiyo kazi kubwa *TANROADS* imeshaifanya. Basi tuombe sasa Serikali iamue kuwekeza nguvu katika chombo chetu cha *TARURA* na kuongezewa fedha ili tuweze kufanikiwa kuleta maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hapo kwenye chombo cha *TARURA* kuongezewa fedha ili kuweza kukuza uchumi, niombe sasa nijielekeze katika kilimo cha alizeti, hasa kwa upande wa Kanda ya Kati. Serikali ilikuja na mpango mzuri na maono bora ya kuhakikisha kwamba kunaanzishwa kwa viwanda mbalimbali kulingana na jiografia ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna zao la alizeti ambalo kwa kiasi kikubwa linalimwa katika Ukanda huu wa Kati. Tuombe sasa kuanzishwa kwa kiwanda kikubwa cha mafuta ya alizeti ili kukuza zao la alizeti katika kanda hii ya kati. Na namna ya kuanzishwa kwa kiwanda hicho kikubwa maana yake ni kwamba kitabeba viwanda vidogovidogo, kitarahisisha wakulima kuongeza bidhaa na kuwa na soko la ndani la uhakika kwa maana tutakuwa tuna kiwanda kikubwa lakini kile kiwanda kikubwa kitakuwa kimebeba nembo ya Tanzania, ambapo baada ya kupata soko la ndani la uhakika tutatoka kwenye soko la nje, litakalokuwa limebeba *brand* ya Tanzania na kuhakikisha kwamba tunapata soko la uhakika la huko duniani huku ndani tukiwa tumeshakidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba zao hilo hilo la alizeti pamoja na kuanzishwa kwa kiwanda kikubwa kitakachowasaidia wakulima wetu wa wafanyabiashara, tuhakikishe pia tunatoa mbegu iliyo bora kwa muda na

wakati kwa wakulima wetu ili kuweza kufanikisha dhana tuliyoamini, dhana ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Vijana. Tunao vijana wenzetu kwenye makampuni na mashirika mbalimbali ambao wameweza kupata ajira zinazoweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaomba Wizara iende ikaangalie, vijana wengi wanafanya kazi lakini hakuna mikataba inayowalinda. Hivyo, tukiweza kusaidia vijana wakapewa mikataba na ajira za kudumu ama mikataba inayoeleweka, itaongeza mapato kwasababu wataweza kupata sehemu ya kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa siku ya leo mchango wangu ulikuwa ni huo, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Atakayefuata ni Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, lakini kabla Mheshimiwa Mwanaisha hajaongea, niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati yetu ya LAAC Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa iliwahi kuagiza huko nyuma kwamba pafanyike ukaguzi maalum wa miradi ya maendeleo iliyofadhiliwa na mradi unaoitwa *ULGSP* kuhusiana na miradi ya maji, mapato ya ndani, na udhibiti wa mifumo ya ndani katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea. *(Makofi)*

Kwa kuwa LAAC walishamuagiza CAG afanye kazi hiyo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Songea, naomba kulitaarifu Bunge hili kwamba tumepokea barua kutoka kwa CAG ambayo imenakiliwa kwetu inawasilisha matokeo ya ukaguzi maalum wa miradi ya maendeleo iliyofadhiliwa na Mradi nilioutaja wa *ULGSP*, miradi ya maji, mapato ya ndani na udhibiti wa mifumo ya ndani katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Kwa ujumla taarifa hiyo imeonesha upungufu na dosari kubwa katika mchakato wa ununuzi, ukiukwaji wa sheria kwa makusudi, uidhinishaji wa matumizi ya fedha za Umma kimakosa na kwa makusudi na hasara ya fedha za Umma kubwa. Vilevile, taarifa hiyo ina mapendekezo kuhusu hatua za kinidhamu dhidi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo ya Manispaa ya Songea na Mhandisi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea. (Makofi)

Kwa jinsi hiyo, kwa vile chimbuko la ukaguzi huo ni ushauri wa LAAC kwamba ufanyike ukaguzi huo. Basi taarifa hiyo sasa naipeleka LAAC ili LAAC muweze kuifanyia kazi kwa wakati na baadaye tujue nini kitakachofuata. Kwa hiyo LAAC muipokee na kuifanyia kazi, msisubiri tena. Ahsante sana. (Makofi)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo kwa Miaka Mitano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, leo nitachangia vitu vikubwa viwili, na kwa kuanzia nitaanza na suala zima la *monitoring and evaluation* yaani ufuatiliaji na tathmini. Nimejaribu kusoma Mpango wa Tatu wa Maendeleo, umeeleza vizuri sana kwamba Mpango wa Pili wa Maendeleo haukutekelezwa ipasavyo. Na miongoni mwa sababu kuu ni kwa sababu hakukuweco na mpango Madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini. Na imeelezwa pia mpango wa pili ulichelewa kuanza, umeanza miaka miwili baadaye.

Mheshimiwa Spika, lakini Mpango wa Tatu pia umeeleza kwamba idara mbalimbali za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zilitengeneza namna zao zenyewe za kufanya tathmini na ufuatiliaji bila kufuata mipango yetu mizuri iende kufanya kazi na kuleta matunda tarajiwa. Ni lazima tujipange vizuri katika ufuatiliaji na tathmini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia nchi zetu za jirani, *South Africa* ina taasisi maalum ya tathmini na ufuatiliaji ndani ya Ofisi ya Rais. Na ukiangalia Uganda, wana taasisi maalum ya ufuatiliaji ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ukiangalia Ghana ina Wizara maalum ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, lakini Tanzania tathmini na ufuatiliaji umepewa *vi-sub sectors* katika Wizara sita tofauti; Wizara ya Fedha imo, Ofisi ya Waziri Mkuu imo, TAMISEMI imo, Utumishi imo, *National Audit* imo na *NBS*. Wote wanafanya ufuatiliaji na tathmini bila kuwa na *heading entity*. Nani ana-*lead evaluation and monitoring* katika Tanzania yetu; hayupo. Naomba niishauri Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, ilibebe suala zima la ufuatiliaji na tathmini ili tuweze kupata matunda tarajiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kaka yangu, Mheshimiwa Reuben juzi alizungumza suala zima la kuwepo na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini. Naungana naye mkono asilimia 200. Lakini vilevile ni lazima tuanze na sera nzuri zenye miongozo ya kuhakikisha ufuatiliaji na tathmini inafanyika katika mikakati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala zima la kuwa na sera na sheria litatusaidia sana kuhakikisha miradi yetu inakwenda kusimamiwa ipasavyo, lakini pia itazuia kukubali mifumo holela ya mataifa yanayotupa udhamini. Kila anayetupa udhamini anakuja na mfumo wake wa tathmini. Sisi kama nchi hatuwezi kukubali kupokea mifumo holela kwasababu tu tunapewa pesa, ni lazima tuwe na taasisi imara ambayo itasimamia ufuatiliaji na tathmini na siyo ku-*accept* kila mfumo kutoka nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Nchini kwetu Tanzania tunafanya vizuri mno katika suala zima la *monitoring*, lakini tathmini za kina hazifanyiki. Mara nyingi tunafanya vikao vingi, tunaandika ripoti nyingi lakini tathmini za kina hazipo. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kutengeneza taasisi imara ambayo itasimamia na kubuni mifumo sahihi ya ufuatiliaji na tathmini. Bila namna hiyo, bila kufanya hivyo hatuwezi kutoka.

Na ndiyo ule utelezi aliosema dada yangu, Mheshimiwa Jesca. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia suala la ushirikishwaji wa wanawake katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu. Naomba ku-*refer* Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu alipokuwa anazungumza na Naibu Waziri wa Michezo alipomwambia kwamba wanawake nao wakanufaike na vipaji vyao katika Sekta ile ya Michezo. Ilinisababisha kufikiri kwamba kumbe mpaka leo bado katika Taifa letu kuna idara ambazo sera zake sio *gender inclusive*, maana yake ilikuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, bado katika taifa letu kuna idara ambazo sera zake sio *gender inclusive*, *this is* maana yake lilikuwa hivyo, lakini ukikumbuka Mkukuta ulishaweka wazi ikielekeza wizara zote kwamba zikawe na sera ambazo *zina-include* ushirikishwaji wa wanawake. Sasa kama mpaka leo hazipo maana yake ni nini? Wawawake wanakuwa wakiweka pembeni katika mpango wa ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Aisha, Ahsante sana; Mheshimiwa Tumaini.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

SPIKA: Mheshimiwa Tumaini Magesa atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Jerry Silaa ajiandae.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya kuweza kunipatia kuchangia katika Mpango huu wa Tatu wa miaka Mitano. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mpango mzuri uliojikita kutoka kwenye *document* takriban kumi na moja ambazo *amezi-refer*, ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa

ya 2025, ikiwemo *Agenda 2063* ya Afrika, lakini na nyingine nyingi mpaka hizo *document* kumi.

Mheshimiwa Spika, binafsi mimi nitajikita katika maeneo mawili tu kwa sababu ya muda. Eneo la kwanza ni la elimu, ambalo liliguswa na mchangiaji wa kwanza au wa pili wa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa naamba 25 wa mpango huu unaonyesha kwamba mwaka 2014 Tume ya Mipango ilifanya utafiti wa soko la ajira na ikaja na majibu kwamba ujuzi wa wale watu ambao wanapata elimu ndani ya nchi hii ulionekana ni pungufu kulingana na mahitaji ya waajiri. Maana yake waajiri kwenye viwanda, kilimo na sehemu zingine. Ukaja na mapendekezo kwamba tunatakiwa tuwekeze, kwenye mpango huo huo, wanasema tuwekeze mara tano ya uwekezaji uliokuwepo mwaka 2014 ili kuweza ku-*fill* hiyo *gap* ambayo inaonekana kwenye elimu tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nishauri; ukurasa namba 73 umekuja na majibu kwenye mpango huu huu. Kwamba tunatakiwa tuguse elimu ya msingi kwa kitu kinaitwa SATU (Sayansi Teknolojia na Ufundi); yaani wanategemea kwenye SATU tuguse hiyo *primary*; lakini tuguse kitu ya T and M kwenye elimu ya vyuo vikuu kwenye mpango huu. Lakini elimu tuliyonayo sasa ni *competence-based education*; ambapo *competence-based education* tunatakiwa tunapotengeneza mitaala yetu tuwe makini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ninategemea kabisa kama tulitakiwa kujaza huo udhaifu ulioonekana hapo tunatakiwa hawa waajiri na mazingira yetu ya kazi yahusike, tujue ni *competence* gani tunahitaji kwenye watu wetu. Kwa mfano, tunamuhitaji mtu ambaye atakwenda kulima maana yake *competence* ni kilimo; sasa ile *principal outcome* ya hiyo *curriculum* tunategemea ituletee mtu ambaye atakuwa na elimu ya kilimo, halafu twende kwenye hizo *enabling* kwamba tunakwenda *kumu-enable* nini ili aje ya hiyo *principal outcomes*.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaona kabisa kuna mahali fulani Wizara ya Elimu huenda inachukua kumbukumbu za *knowledge based* na kutengeneza *curriculum* na hatimaye ndiyo sababu hatuwapati hao ambao tunawahitaji. Kwa sababu kama tunahitahi na tunaujua mwisho wetu tunashindwaje kutengeneza *process* ya katikati ili tuwapate hao wataalam? Kwa hiyo niishauri Wizara ya Elimu waangalie *competence* gani tunahitaji kwenye eneo hili, baadaye waende kwenye *principal outcome* waende *sub-enabling* na mwisho wa siku tutakuwa tunaweza kupata *ability* ambazo tunazihitaji kwa watu wetu. Tutapata hicho tunachohitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini niguse viwanda. Mimi niseme tu *ni-declare interest*, mimi ni mhandisi; tunatatizo kwenye viwanda vyetu. Ukisoma kwenye *document* ya Mheshimiwa Waziri ya mpango huu ukurasa namba 68 unaonesha tutakuwa na viwanda vya *ku-process*; lakini umeonyesha mambo mawili kwenye ukurasa wa 68. Unaonesha kwamba ni lazima tuwe na mali ambazo tunaziua nje ambazo *zipo-process*. Lakini ya pili ulionesha kuwa lazima kuwe na *political will*, kuwe na utashi wa kisiasa wa kufunga mikataba ambayo ina faida kwa nchi, kwenye ukurasa wa 68; ni *document* hii ambayo ninaizungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa shida ninayoiona tunapoenda *ku-process* kwenye viwanda vyetu; kwa mfano viwanda vya alizeti, hakuna kiwanda cha alizeti kinachota *double refined oil* nchi nzima, tunatoa *semi refined* kila mahali, na haya ndiyo mafuta ambayo kila Mtanzania amekula. Kuna mahali fulani hata ukimuona mtu anachangangia anachemka unajua hii ni *semi refined* ilimu-*affect* tangu utoto mpaka leo ndiyo sababu anahemuka. Kwa hiyo kuna mahali ambapo tunatakiwa sasa tutengeneze *double refined* ili watu wetu wale mafuta yaliyosafi (*quality food*) lakini tunachotengeneza ni *semi refund* na watu wote wanakula *semi refined*.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme, tunatakiwa tuongeze ujuzi kama tulivyosema. Kuna njia mbili ya

kutengeneza mafuta kwanza ni *press*; yaani *ku-press you press by hydraulic* au *you press by expeller machines* kuna *machine kumal, kuna machine za VIP* zinafanya hiyo *pressing*. Hiyo teknolojia ya zamani, teknolojia ya sasa ambayo itatutolea mafuta mengi ni *solvent extraction* ambayo nchi nzima hakuna mahali ambapo tunafanya *solvent extraction* tunafanya *pressing* tu. Na ili *u-press* mafuta kutoka kwenye mbegu zetu lazima utumie *motor* kubwa na gharama yake inakuwa kubwa. Kwenye *solvent* unatumia *chemicals* tutaenda kufanya *double refine* tutakuwa na mafuta yaliyo safi. Nchi nzima sasa ina mafuta yanatoka Uturuki wanatumia *solvent extraction*, kwa nini sisi tusingie kwenye teknolojia hiyo ili tuweze kupata mafuta?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna habari ya *gape* ya ujuzi ambayo tunatakiwa kwenye viwanda na biashara sasa waangalie *gape* hiyo mahali gani kwenye uhandisi tunaiondoa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Yahaya Masarre halafu Mheshimiwa Godwin Kunambi.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie mawazo kidogo katika rasimu hii ya mpango 2021/2022 – 2025/2026, hasa katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wanategemea sana kilimo, lakini hata makusanyo ya serikali kupitia viwanda vyetu ambavyo vinatoa kodi kubwa ambayo tunategemea kwenda kukusanya mazao, kwa maana ya malighafi itategemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kuhusu suala la mbegu ambalo limekuwa nichangamoto kubwa na ni kubwa kweli kweli. Sisi Mkoa wa Singida ni wakulima wazuri wa alizeti, lakini mbegu nzuri ili mwananchi avune na apate kile ambacho anategemea, kulingana na mwaka mzuri wa mvua nzuri inauzwa Shilingi 35,000 kwa kilo moja. Lakini akishavuna gunia zima anauza Shilingi 60,000 na si Zaidi ya Shilingi 70,000. Maana yake ni kwamba, ataweza kununua kilo mbili kwa kuuza gunia moja ili aje alime.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliangalie hili kwa macho mawili . Unapomuuzia mkulima mbegu kwa bei kubwa hauchechemui uchumi hasa kilimo. Sasa, ni namna gani mpango huu utaenda kuangalia, kwa hii miaka iliyobaki, kuona sasa Serikali inaweka mkono wake kwa maana ya ruzuku katika mbegu ili wananchi wanunue mbegu kwa bei nafuu, uzalishaji uwe wa kutosha na mazao yawe bora?

Mheshimiwa Spika, kuchechemua uchumi ni pamoja na miundombinu. Barabara zetu za vijijini, barabara zinazounganisha mkoa na mkoa bado kunachangamoto kubwa kabisa tunapoenda katika mpango huu wa miaka hii ya kumaliza mpango huu ambao umebaki.

Mheshimiwa Spika, sisi wa Mkoa wa Singida ni miongoni wa watu wanaosononeka kwa kutounganishwa na mikoa mingine. Ni kweli tumeunganishwa na Mikoa ya Dodoma na Tabora lakini hatujaunganishwa na Mikoa ta Mbeya na Simiyu mpaka hivi tunavyoongea. Tumeshamaliza daraja ambalo ndilo lilikuwa kikwazo, Daraja la Sibiti, na leo limemalizika, lakini hatua mipango ambayo Serikali inaenda kuchechemua uchumi kwa wananchi hawa ambao ni wazalishaji wakubwa. Hebu tuje sasa na *plan* ambayo barabara hizi; barabara ya Mkiwa kwenda Makongorosi ambapo barabara kubwa iliyobaki ina kilomita 412 kutoka Mkiwa mpaka ilipoishia kandarasi inapoendelea sasa. Sasa, hawa wananchi unategemea nao washindane na wenzao? Hawawezi kwa sababu mahali pa kutembea masaa matatu unatembea masaa kumi na tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali ije na mpango mahsusi. Tunapokwenda kwenda na *standard gauge*, tunapokwenda kutengeneza Bwawa la Nyerere. Tuna vijana wasomi wanaotolewa na vyuo vikuu vyetu, sasa wanakwendaje kuingia katika ajira hasa hii ambayo tunaitegemea wakajajiri. Kilimo ukishalima, ukishavuna unaingia barabarani unatembea masaa mengi barabarani ili ufikishe mazao hayo sokoni.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu hii sikivu chini ya Mheshimiwa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye ameonesha dhamira njema kabisa kwa maneno yake na sisi Watanzania tuko nyuma yake tunaamini si miongoni wa wale watakaotia ulimi puani, kufata nyayo za aliyekuwa Rais wetu, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa haya ambayo aliyaanzisha hasa suala zima la miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sasa mawaziri ambao wako humu wamsaidie Mheshimiwa Rais kuona zile changamoto kubwa ambazo ndio kero ya wananchi zinatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote na changamoto lakini na pongezi zipo, Serikali hii imejenga miundombinu mizuri sana hasa katika vituo vya afya, katika huduma zote za afya na elimu. Bado suala hili tu, kidogo maji, lakini na miundombinu ya barabara zinazounganisha mikoa na mikoa. pia barabara zetu za vijijini ni za kutolea macho mawili. Kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyoshauri namna ya kuiongezea *TARURA* pesa; ni namna gani tuongeze na ni wapi muangalie ambako hakuna shida, wengine wameshauri kwenye mafuta. Busara itumike na *TARURA* waongezewe pesa ili barabara nyingi za vijijini ziweze kufanya kazi vizuri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry Silaa.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya njema hadi siku ya leo nikapata fursa ya kutoa mchango huu.

Mheshimiwa Spika, mimi nijielekeze moja kwa moja kwenye sekta ya kilimo. Unapozungumzia sekta ya kilimo kwenye taifa letu unazungumzia sekta muhimu sana, hasa ukizingatia zaidi ya Watanzania asilimia 65 wanashughulika na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia kilimo kuna mambo ya msingi hapa ya kuzingatia. Jambo la kwanza ni suala zima la utafiti, jambo la pili ni pembejeo na la tatu ni masoko; lakini wanavyokwenda kwenye masoko utagusa kidogo na masuala ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumzia tafiti mimi najiuliza maswali mengi sana hapa. Tumekuwa tuzijenga hoja za tafiti kwenye kilimo. Hatuna changamoto ya tafiti, tuna vyo ambavyo vipo hapa kama vile Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) ni maelekezo tu. Wenzetu Japan kule wana mfumo mmoja ambao wanasema *Public Private Academia*. Maana yake nini, kuna umuhimu wa wasomi kufanya tafiti; tungetumia vyo vikuu vyetu hivi kufanya tafiti, hamna haja ya fedha eneo hilo. Wape maelekezo SUA wafanye tafiti kwenye kilimo tuwekeze tupate kilimo chenye tija kwa taifa letu. (*Makofi*.)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nimezungumzia suala la pembejeo. Bado kuna changamoto kubwa ya pembejeo lakini kubwa zaidi ni masoko.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye zao hili la kimkakati la mpunga. Ukizungumzia Mkoa wa Morogoro hasa Jimbo la Mlimba, sisi katika taifa hili tunalisha zao la mpunga. Hata hivyo tuna changamoto ya kuuza mpunga nje ya nchi, lakini hatuwezi kuuza mpunga mpaka tuuchakate mpunga. Kwa hiyo naiomba Wizara ya Kilimo itusaidie. Jimbo la Mlimba tungeweza kufanikiwa sana kama tungewekeza viwanda vya kuchakata mpunga tupate mchele, mchele uwekwe kwenye fungashio *actually* uwe *branded* na upelekwe nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuona hapa wenzetu Japan wanaagiza chakula cha mwaka mzima, nilisema hapa awali, Zimbabwe wamekuwa wadau wakubwa wakiuza chakula nje ya nchi, na sisi tunaweza kufanya hilo; kwa hiyo tuongeze jitihada za utafiti kwenye kilimo, pembejeo lakini pia na viwanda pamoja na suala zima la masoko.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ninataka niliguse ni eneo la viwanda. Eneo hili nitagusa wizara mbili, Wizara ya Ulinzi lakini pia na Wizara ya Viwanda na Biashara. Naomba kama kuna Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri mnisikilize kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika safari ya maisha yangu mnamo mwaka 2002 niliwahi pita pale Nyumbu. Nyumbu pale kuna Shirika la Nyumbu la Taifa. Shirika la Nyumbu la Taifa, yaani Nyumbu *Automobile Engineering*, mimi nimekaa pale miezi minne; nchi hii ni Tajiri. Kama Shirika la Nyumbu likatumika vizuri hatuwezi kuagiza magari Japan. Pale Shirika la Nyumbu linavifaa vyote lina *foundry* zote, linafanya hata *iron processing*. Kuna *Electrical Furnace* ambayo kazi yake ni kuchakata chuma. Wana-pattern shop, *wana-foundryshop*, wana kila kitu. Mheshimiwa Baba wa Taifa alianzisha shirika hili ili tuweze kupata magari ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama tunafikiri kuna eneo la kuwekeza ili tupate fedha ni Shirika la Nyumbu. Kwa hiyo Waziri wa Ulinzi na Waziri wa Viwanda mtusaidie kufufua Shirika la Nyumbu ili Watanzania tusinunue magari nje ya nchi tununue

ndani ya nchi yetu. Labda niseme tu, kwenye uchumi mtanisaidia. Suala la mauzo nje ya nchi na kuagiza bidhaa nje ya nchi; Mheshimiwa Waziri wa Fedha kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba naomba unisikilize eneo hili. Kwenye uchumi kuna masuala tunazungumzia kuna jambo la *export* na *import* nchi yeyote yenye uchumi imara lazima izalishe na kuuza sana nje ya nchi. Ukiona mnaagiza sana kuliko kuuza nje ya nchi maana yake nini, ukikokotoa pale, kuagiza bidhaa nje ya nchi idadi ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi ikiwa kubwa kuliko idadi ya bidhaa tunazonunua unapata *favorable balance of payment, favorable balance of payment*, maana yake unapata jibu chanya na siyo hasi, eneo hili wachumi watanielewa kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukiendelea kuagiza sana kuliko kuuza bidhaa nje ya nchi bado tutaendelea na uchumi ambao unatusababishia kuwa *unfavourable balance of payment* na mwisho wa siku nchi yetu itapata tatizo la *capital flight*. *Capital flight* kwenye uchumi maana yake unavyoagiza bidhaa nje ya nchi unachukua pesa ya ndani ya nchi kwenda kubadilisha na pesa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: ...ya nje ya nchi yaani dola maana yake nini ndani ya nchi hiyo utapata changamoto ya *balance of payment*.

Mheshimiwa Naibu Spika; naomba nimalizie kwa jambo moja, dada yangu hapa Mheshimiwa Halima Mdee amezungumza jambo ambalo Mungu anisaidie Roho Mtakatifu anishukie wakati namalizia tu. Kwanza nianze na lugha za kejeli, lugha za kuudhi.

Mheshimiwa Spika, sisi wengine ni vijana pia na bado hata umri wa busara haujafika, tuna hofu sana. Tunasihi, na mimi niseme tu kwa dhati, namuonya, aache lugha za kejeli

ndani ya Bunge hili, aache lugha za kejeli ndani ya Bunge hili namuonya tu, hamna njuka hapa, njuka maana yake nini? kwa hiyo namuonya kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia amezungumzia suala zima ya ATCL, unapotosha. Uchumi wowote duniani unapozungumzia usafirishaji inamaanisha kuwa ni huduma, it's just a service, ni huduma tu, *ku-facilitate* maeneo mengine ya uchumi kama utalii, kilimo na maeneo mengine. Anakuja hapa anatudanganya, anadanganya Watanzania hapa tunampigia makofi hapa. Lugha za kuudhi nakuonya. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa

SPIKA: Ahsante sana huyo ni Mheshimiwa Kunambi! Sasa Waheshimiwa tusikilizane bahati nzuri hakuna taarifa kwa hiyo tunaendelea. Mheshimiwa Jerry Silaa. *(Makofi/Vicheko)*

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kupata fursa ya kuchangia kwenye Mpango huu wa Miaka Mitano. Nakushukuru zaidi kwa sababu pamoja na kupongeza Mpango huu mzuri, nitaanza kuchangia si mbali sana na alipomalizia mchangiaji aliyepita.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niipongeze sana Serikali kwa kuja na Mpango huu ambao ukusoma umezingatia sana michango ya Wabunge waliyotoa wakati Mpango huu umewasilishwa. Pia ukusoma Mpango huu...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize Mheshimiwa Jerry Silaa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, Mpango huu unakuja kuendeleza pale Mpango wa Miaka Mitano iliyopita; Mpango wa mwaka 2015-2020 ambao tumeona Serikali ikiwekeza kwenye miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaenda kulifanya Taifa letu kuwa na uchumi unaojitegemea.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika kwenye Bwawa la Stigler's Gorge. Kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika kwenye Reli ya *Standard Gauge*. Kazi kubwa imeendelea kufanyika katika miradi ya kufufua Mashirika ya Umma ikiwepo Shirika letu la Ndege la *ATCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine na mimi kidogo ni Mwanasheria. Ukisikiliza mchango wa Mwanasheria mmoja hapa dada yangu nauona kabisa umepungua sana *knowledge* ya kimkakati kwenye miradi ya kimaendeleo na fedha. Unapoongelea Shirika la *ATCL*...

SPIKA:Mheshimiwa Halima usikilize vizuri unasomeshwa shule hapa. Hii ni shule unasomeshwa, kwa hiyo tulia. Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, kule kwenye sheria tunafundishwa *purposive approach ya legal interpretation*, kwamba unasoma sheria kama ilivyoandikwa, kwenye fedha hatufanyi hivyo. Unapoongelea Shirika la Ndege, kwanza lazima utambue ni Shirika ambalo lilikuwa lina-*operate* kwa ndege moja. Katika miaka mitano iliyopita, Serikali imefanya kazi kubwa ya kufufua Shirika hili. Ndege ya kwanza imepokelewa mwishoni mwa mwaka 2017, zimekuwa zikipokelewa ndege mpaka tunavyozungumza zimepokelewa ndege nane (8) na ndege tatu (3) zitakuja kwenye Shirika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa wale wenye kufanya biashara wanafahamu, huwezi ukawa unafufua Shirika *at the same time* ukawa unatengeneza faida, hajjawahi kutokea. Ziko aina ya biashara ambazo mpaka sheria zetu za kodi zinaruhusu hasara miaka mitatu mpaka miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wako Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema, Shirika la Ndege si biashara bali ni huduma inayoenda kuchochea maeneo mengine ya biashara. Ukisoma Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali,

maana *Financial Statement* hazisomwi kwenye *purposive approach*, husomi tu ile hasara ukabeba ukaleta hapa Bungeni kuja kupotosha umma wa Watanzania, unasoma uwanda mpana wa ripoti ile.

Mheshimiwa Spika, yapo madeni ya kurithi kwenye Shirika hili, lakini ningetegemea maana na majina tunaitwa wengine Njuka ningetegemea maneno hayo yasemwe labda na Njuka, mzoefu alitakiwa kufahamu kwamba hata ndege hizi zilivyonunuliwa zinamilikiwa na *TGFA*, *ATC* inazikodisha. Kwenye Ripoti ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ukiisoma inasema kabisa kwamba kuna deni limetokana na kipindi ambapo *TGFA* inakodisha ndege *ATC* lakini wote tunafahamu, si *ATC* peke yake au hamtembei jamani, dunia nzima ndege zimepaki kwa sababu ya *COVID-19*! Hili siyo Shirika pekee lililoathirika! (*Makofi*)

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Elibariki.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe msemaji taarifa kwamba dunia kwa ujumla, kwa mwaka huu peke yake ime-*accumulate loss* ya dola bilioni 118 katika Mashirika ya Ndege. Kwa hivyo, hii haiwezi kutu-*discourage* sisi tuone kwamba *ATC* haina faida kwa Watanzania. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Jerry endelea.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa. Unaponunua ndege kwenye mizania ya kampuni ni *capital expenditure*. Kumbuka manunuzi haya yatakuja na mafunzo ya wataalam, marubani, wahandisi, kuboresha karakana; zote hizo huwezi ukaanza kuona faida kwenye miaka hii ya mwanzo. Pia ndege hizi, maana msemaji anasema ndege zimepaki, ndege haziruki kama kunguru zinaruka kwa mpango. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Jerry Silaa bado dakika tano zako.
(*Makofi/Kicheko*)

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, sisi wengine tumekulia kwenye familia za *aviation*. Tumenunua ndege za *Bombardier Q4100* kwa sababu ya safari za ndani. Tumenunua *Airbus*, jamani hata mitandao hamuangalii? Ukiona Mheshimiwa Rais Mama Samia anasafiri ndani anasafiri na Q4100; jana ameenda Uganda na *Airbus* kwa sababu ndege zile zimenunuliwa kwa sababu ya *Regional Flights*. Zile *Dreamliner*, kila siku mnatangaziwa kwamba zilinunuliwa kwa sababu ya safari za masafa, *trip* za Guangzhou, London, India, ndege ya moja kwa moja toka nchini kwetu. Ukitoka zako ulikotoka ukaja Jijini Dar es Salaam ukakuta zimepaki, usishangae, mashirika haya yameathiriwa na magonjwa ya COVID-19 ambayo imeathiri sana usafirishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunapofanya *capital expenditure* yoyote huwezi kuepuka kukopa. Swali huwa unakopa ufanyie nini? Kama tunakopa kwa ajili ya miradi mikubwa ya kimkakati, miradi hii ina tija kubwa kwenye uchumi wa nchi yetu, ni jambo la kupongezwa wala si jambo la kubezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa sisi tuliopewa dhamana na wananchi wa Tanzania, bila kujali umeingilia mlango gani, maana wako Wabunge hapa Vyama vyao wenyewe vinawakana...(*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tunawaheshimu kama Wabunge wenzetu, tukisimama hapa kuchangia tuweke maslahi mapana ya nchi yetu.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, tuweke maslahi mapana ya *legacy* aliyotuachia Rais wetu na tuisaidie Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Hilo ndiyo Bunge jamani. Naona *Njuka* wamechachamaa, wamekataa kabisa kuitwa *Njuka*. Halima umechokoza mwenyewe. Ndiyo raha ya mjengoni jamani eeee! Au sio? Mijadala ya moto kabisa namna hiyo lakini mwisho wa siku tutafika tu. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba niwashukuru sana, tunaendelea na shughuli yetu hii ya mjadala jioni na tutahitimisha hoja hii jioni kwa mtoa hoja kuweza kuweka sawa. Baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri watapata nafasi nao kuchangia Mpango wa Miaka Mitano wa Wizara mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge tutaanza kidogo leo jioni kwa hiyo ni vizuri tuwahi kufika.

Kamati ya Mheshimiwa Mussa Zungu ya Ulinzi na Usalama, ningeomba isikutane Kamati Ndogo ikutane Kamati nzima kwa ajili ya zile ajenda zao ili wawe na uelewa wa pamoja kwenye Kamati nzima.

Pia tunaokwenda kwenye kupiga kura, ukumbi wa Msekwa nimepata ushauri kwamba ni vizuri mkaenda moja kwa moja badala ya kusubiri saa nane. Mkitoka hapa, basi muende, mnapiga kura tu haraka haraka pale, mnatoa matokeo tupate uongozi wa *Bunge Sports Club*. Hili linahusisha pia watumishi wetu wa Bunge ambao nawaomba nao waweze kuwahi kufika pale, ukifika pale kura zimeshapigwa inakuwa tena umepoteza fursa ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Tutaendelea na uchangiaji jioni kama nilivyosema. Wale wote ambao mmejiandikisha basi mjitahidi kuwahi na wengine wote tuwahi ili tuhitimishe hoja hii muhimu sana ya Mpango wetu wa Miaka Mitano. Tukishapitisha leo tutakuwa ndiyo tumepata sasa Kiongozi cha Miaka Mitano baada ya *process* nzima ambayo tumeipitia kwenye Bunge lililopita na kwenye Bunge hili. Naamini tutakuwa na kitu fulani kizuri kabisa ambacho kitatusaidia kwenda mbele kwa haraka zaidi na kwa mwendo wa uhakika zaidi kama nchi.

Nikumbushe tena kwamba *Caucus* ni jioni tutakapoahirisha shughuli zetu. Nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 kamili jioni ya leo.

(Saa 07.11 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu. Mheshimiwa Masache Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack. Kama hawapo, naendelea na orodha inayofuata. Iddi Kassim Iddi au Mheshimiwa Deus Sangu.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, Francis nipo, nilikuwa nasubiri kama Mheshimiwa Kasaka atasimama.

SPIKA: Hapana, hayupo. Kwa hiyo, endelea Mheshimiwa Francis; na wale niliowataja wajiandae kama wapo.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi nami kuweza kuchangia Mpango huu wa Tatu. Kwa sababu nafasi yenyewe ni ya dakika tano, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajielekeza katika kutafuta fedha ambazo zitatusaidia kwenda kwenye *TARURA* ili Jimbo langu la Mkalama, Iramba Mashariki liweze kupata fedha za kutengeneza barabara. Yako mambo ambayo mara nyingi Serikali imekuwa ikiyatumia kupata fedha na mara nyingi sana wamekuwa wakienda kwenye vinywaji, lakini safari hii fedha ya uhakika ipo kwenye mafuta.

Mheshimiwa Spika, viko vifungu vingi sana ambavyo kwa ujumla wake vinatengeneza bei ya mafuta ya lita ambayo tunanunua kwa sasa. Katika vifungu hivyo, kimojawapo ni kifungu ambacho kinahusu *marking*, yaani kuweka alama ya mafuta ambayo yako *on transit* na yale

ambayo yanatumika ndani ili kuepuka wanaokwepa kodi na kuepuka uchakachujaji.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki, kinafanywa na Kampuni ambayo imepata *tender* na gharama yake inayolipwa, ni shilingi 14 na senti 22 kwa lita moja. *TBS* pia wanapata pesa kutoka kwenye hivi vifungu vya mafuta, wenyewe wanapata kama shilingi moja na senti kadhaa hivi.

Mheshimiwa Spika, naona kazi hii ya kuweka *marking*, *TBS* wanaweza kuifanya kwa uhakika tu, kwa sababu ndiyo Shirika letu la Viwango. Kazi hii ikifanywa na *TBS* hata kama wataongezewa fedha kidogo kutoka kila shilingi moja tutaokoa fedha nyingi sana ambazo zinafanywa na kampuni; na kwa bahati nzuri kampuni hii muda wake umeisha lakini wamekuwa wakiongezewa ongezewa muda tu kwa miezi mitatu mitatu na *EWURA* sijui kwa utaratibu gani? Kama kazi hii itafanywa na *TBS*, hii shilingi 14 tukaamua kui-*save*, tutaipeleka *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme jinsi fedha hii itakavyopatikana. Takribani kwa mwezi mmoja, mafuta yanayoingia nchini ni kati ya lita 390,000 mpaka 400,000 *metric ton* ambapo *Metric ton* moja ni sawa na lita 1,000. Kwa hiyo, ukibadili hizi *metric ton* 390,000 kuwa lita ni kama lita 390,000,000 kwa mwezi. *Uki-compute* hizi shilingi 14 kwa kila lita kwa mwezi mmoja, unapata takribani shilingi 5,545,800,000/=. Ukifanya mara 12 kwa mwaka unapata shilingi 66,549,000,000/=. Fedha hii ikienda *TARURA*, Majimbo yetu yatakuwa yamepoma na bado kazi ya *marking* inaweza ikafanywa na *TBS*.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha, hii ni shilingi bilioni tano kwa mwezi, ni hela ambayo anaweza kuipata mwezi ujao tu akiamua, kwa sababu hata hiyo Kampuni inayofanya kazi hiyo, muda wake umeisha. Kwa hiyo, ni kauli tu na maamuzi kwamba kazi hii sasa ifanywe na *TBS* na ile shilingi 14 kwa lita ambayo ilikuwa inachukuliwa na hii Kampuni ziende kwa ajili ya *TARURA*. Kila mwezi tuna uhakika wa kutengeneza shilingi bilioni tano ambapo

wananchi wetu na barabara zetu zitapata fedha ya uhakika kiasi cha shilingi bilioni 66,549,000,000 kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba hebu Waziri afanye maamuzi haya, kwa sababu ni maamuzi ambayo yana maslahi ya Watanzania hata Mungu ataona. Baada ya kutafuta pesa, naomba tu niseme, huu ni Mpango wa Tatu kuchangia, kuusikiliza tangu niingie Bunge hili kwa sisi ambao tunaitwa *Form One*. Mchango wa kwanza kwa Wabunge, ulikuwa unahusu Hotuba ya Rais; mchango wa pili, ulikuwa unahusu Rasimu ya Mpango huu; na sasa Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, ambacho nakiona, Waheshimiwa Wabunge wanatoa michango mizuri sana yenye mashiko ya kuongoza nchi hii, lakini yanapokuja majibu ya Mawaziri, zile dakika tano tano, yanakuwa majibu mepesi ambayo hayaendani na uzito wa michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiitoa.

Mheshimiwa Spika, nakuomba, ikikupendeza utengeneze Kamati Maalum ya Kudumu ambayo itakuwa inaangalia majibu, ili vitu ambavyo viko kwenye *Hansard* ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameshauri Mawaziri, kila linapokuja Bunge linguine, wameteteleza kiasi gani? Ili tupate Hadidu za Rejea. Vinginevyo, tutakuwa tunasema vitu vizuri, watu wanavisikia, wanatupia simu wanatupongeza, lakini *implementation* yake haipo. Hata vikao vya kawaida huko nje, kuna yatokanayo na maazimio, lakini hapa tukisema, vinaenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ukitengeneza Kamati hii, Mawaziri watakuwa wanajua kabisa Bunge Ijalo wataenda kuulizwa; hili lilichangiwa, hili lilichangiwa, limefanya kazi gani? Limefika wapi? Yako mambo mazito sana yamechangiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilisikia mchango mmoja wa Mheshimiwa Mbunge mmoja aliongelea suala la kiwanda kikubwa cha pamba kitakachomeza pamba yote ya nchi hii ambayo itatoa tija kwa wakulima, itatoa ajira kwa

vijana, tutauza majora nje, lakini ilipofika kwenye majibu, sikusikia, imeishia vivyo hivyo hewani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisikia Mheshimiwa Mbunge alisema kuhusu mambo ya *task force* ambayo inasumbua wafanyabiashara, alisema Mheshimiwa Nape pale, lakini ilipokuja kwenye majibu, kimya. Mpaka niliposikia Mheshimiwa Rais wangu analiongelea juzi, wakati anasema watu wasisumbuliwe kuhusu kodi.

Mheshimiwa Spika, hebu tutengeneze Kamati ambayo itakuwa inafuatilia mambo haya kwa Mawaziri ili vitu vinavyosemwa humu, tuvione vinafanya kazi kwa sababu ni vitu vyenye mashiko, ni nondo zinashuka humu lakini zinaishia hewani hewani tu. Matokeo yake mpaka watu wengine huko nje wanaanza kusema viongozi sio asilimia 60, hatuna uwezo. Uwezo tunao. Kama watu hawawezi kutoa mrerejesho, wapishe wengine waweze kufanya hizi kazi.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopatikana *TARURA*, naamini kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu atalijibu hili, kwa sababu ni kauli yake tu inatupatia mabilioni ambayo yanakwenda kwenye mambo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Francis Isack. Naendelea, lakini sasa nitaangalia ambaye atakuwepo ndiyo huyo, kwa sababu nina watu sita tu ambao wataongea na sina hakika nani yupo na nani hayupo. Kwa hiyo, tuendeleo. Mheshimiwa Neema Mwandabila yupo? Kama hayupo Mheshimiwa Paulina Nahato.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, nipo.

SPIKA: Neema yupo eeh! Ahsante, tuendeleo Neema.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia

kidogo katika huu Mpango wa Miaka Mitano. Kwanza kabisa kabla sijaendelea, napenda niunge mkono hoja Mpango huu. Pia napenda kuwapongeza Wizara ya Fedha kwa Mpango huu, tunaamini miaka mitano hii, haya mambo yote yaliyoandikwa humu yakitekelezwa tutakuwa tuko sehemu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu napenda kujielekeza katika mambo mawili. Katika hayo mambo mawili, napenda kuongelea mambo ya uzalishaji wa bidhaa muhimu za ndani; mfano sukari, chumvi, mafuta ya kula ambayo iko katika *page* ya tano na ya sita kwenye mambo ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuongelea kwenye ukuzaji wa soko la ndani. katika kukuza uchumi wa nchi, tunajua kabisa nchi yetu na Mataifa mengine yameathiriwa sana na suala la *Corona*. Tukisema kwamba tunaweza kuongeza fedha kutoka nje, siyo jambo jepesi, lakini lazima tujitathmini. Soko la ndani tulilionalo kwa bidhaa zile za msingi ambazo kila Mtanzania lazima atatumia, tumejidhatiti vipi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kuchangia hayo, nilitaka nirudi kule kwetu Songwe, Wilaya ya Momba katika Kata ya Ivuna ambapo tuna mradi wa chumvi. Huu mradi upo na tafiti zilishafanyika na ikaonekana kabisa chumvi iliyopo pale ni ya kiwango kikubwa sana ambacho hakiishi leo, lakini siioni ile dhamira ya Serikali kuwekeza pale pesa ya kutosha ili chumvi ile iweze kuhudumia angalau Kanda ya Chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea chumvi, ni kitu ambacho mtu anaweza asitumie sukari, lakini chumvi akaitumia. Kwa hiyo, katika Wizara hii nilitamani tuongezee kipengele cha chumvi, kwa sababu mpaka sasa hivi sielewi kama chumvi iko Wizara ya Madini au iko sehemu gani? Kwa sababu kwenye Madini haijawekwa na sioni popote chumvi ambapo inasoma katika Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, katika Mradi huu wa Chumvi, tunaishukuru Serikali, ilitenga shilingi milioni 535, lakini ikaweza kutupatia shilingi milioni 120, si haba, lakini kiwango cha pesa kinachohitajika ili uzalishaji uwe mkubwa ni karibu shilingi bilioni nane. Kwa Serikali hii ya Tanzania ambayo ni Tajiri, siamini kama inashindwa kweli kujikita kuweka fedha kiasi cha shilingi bilioni nane izalishe chumvi ambayo ni lazima itauzika na ikizidi tunaweza tuka-*export* nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nijikite hapo. *Otherwise* ningependa pia kuchangia kwenye kipengele cha mafuta kidogo. Tunaamini kabisa kwamba Watanzania wengi ni wakuliwa na wangeweza kupata fedha kupitia hii fursa ambayo ipo kwenye mafuta kwa kujielekeza kuzalisha mbegu za alizeti, chikichi na hata kuzalisha ufuta wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba kama kweli tuna dhamira ya kukuza uchumi, lazima tuwatazame hawa watu ambao wanaitwa wakulima; watu wa chini kabisa ambao ndio wanatufanya wote tuwe na amani hapa, maana bila chakula tunaamini kabisa hakuna mtu ambaye angekuwa yupo *comfortable* kukaa hapa kama chakula kisingekuwepo. Kwa hiyo, kabla haujatokea mgomo wa wakulima, napenda kuona kabisa wakulima wanapewa kipaumbele, kwa mambo yao yale ya msingi mfano hiyo fursa ambayo ipo ya kuzalisha mafuta, mahindi na kadhalika, yangukuwa yanachukuliwa kwa uzito. Kama ni viwanda vya uchakachuaji wa hizo bidhaa, viwekwe vile ambavyo vina ubora vitafanya *finishing* nzuri na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nisiseme mengi sana, naomba niishie hapo. *Otherwise* naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Paulina Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami pia nichangie juu ya Mpango

wa Tatu wa Maendeleo. Nami nitajikita katika masuala ya afya. Awali ya yote napenda sana kuishukuru na kuipongeza Serikali katika ujenzi wa miundombinu ambayo imefanya mpaka sasa katika masuala ya afya Na marekebisho mengi yaliyofanyika katika upatikanaji wa huduma ya afya, yaani huduma ya afya imekuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa, pamoja na kwamba tuna mambo mengi sana ambayo tunayaongelea, lakini suala la afya ni muhimu sana. Ninaomba kujikita katika sehemu ya kinga. Hili eneo la kinga au *preventive* au *public health* halijaangaliwa sana, yaani halijapewa kipaumbele sana kama tiba. Mambo mengi sana yanayoongelewa ni kuhusu tiba na siyo suala la kinga.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kabisa kwamba magonjwa mengi yanazuilika. Kama tutaweza kuzuia magonjwa mengi, tutaweza kukuza uchumi; Tutapata watu ambao watakuwa na afya na wataweza kujikita katika masuala ya uchumi hasa tutakapojikita katika masuala ya kinga. Magonjwa mengi yanatibika. Magonjwa ambayo tunaita *communicable diseases* na *non-communicable diseases*, magonjwa yote tuseme.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ili kuweza kufanikiwa katika eneo hili, kuna mambo matatu, kwa kifupi sana naomba kuishauri Serikali. Angalau kuwe na mipango ya aina tatu; mipango ya muda mfupi, mipango ya muda wa kati na mipango ya muda mrefu. Ninapoongelea mpango wa muda mfupi ni kwamba sasa ni kweli wananchi wengi vijijini elimu haiwafikii kuhusu visababishi vya magonjwa mengi. Matokeo yake, kunakuwa na mlundikano wa wagonjwa katika hospitali zetu, ambapo kama hao wananchi wetu watafikiwa na kujua vyanzo vya magonjwa mengi ni nini, wangeweza kujizuia, na hivyo, tuta-*save* fedha nyingi sana na tutafanya mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa hivi ni kweli elimu inatolewa, lakini inatolewa kwenye televisheni na redio ambapo vijijini watu hawana hivyo vitu. Tufanye nini? Tufanye

kila njia kuhakikisha kwamba wananchi wote hasa wa vijijini wanafikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba Wahudumu wa Afya wale walioko kule vijijini kule, *Primary Health Care* watumike kusambaza elimu ya kinga kwa wananchi wao. Watasambazaje? Ziko mbinu nyingi za kusambaza. Wale Wahudumu wanaweza wakaongea na wagonjwa asubuhi kabisa pale wanapofika kabla ya kupata huduma wakawaeleza, wale watu wakajua na hivyo wanaweza wakajikinga. Kwa mfano, magonjwa yanayotokana na maji machafu na minyoo na vitu kama hivyo, watu wanaweza wakajizuia tu. Kama ambavyo sasa hivi tumesambaza habari kuhusu *Corona* na watu wanajizuia.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa muda wa Kati sasa, labda kuweza kuwajengea hawa Wahudumu uwezo wa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi mfupi (*short trainings*) ili hata wao wenyewe wajue namna ya kuongea na wananchi kuanzia chini mpaka kwenda juu. Faida yake ni kwamba, magonjwa yatapungua. Magonjwa yakipungua hata matumizi ya dawa yatapungua.

Mheshimiwa Spika, pia katika Mpango huo huo wa muda wa kati kuna suala la kuongeza watumishi na kuongeza utafiti. Tafiti zinafanyika, wanafunzi wanakwenda *field*, lakini hizi tafiti zinaishia kwenye Ofisi za Kata. Maana utafiti ukifanyika, ukimaliza kufanyika, *report* ndogo inatolewa inafikishwa Ofisi ya Kata au ya Kijiji, lakini zile tafiti zinawekwa tu kwenye madroo. Watafiti wakirudi mara ya pili, wananchi wanasema sisi tulikuwa hatujui, hawakupewa matokeo ya zile tafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali iangalie kuhakikisha kwamba haya matokeo ya tafiti wananchi wanayapata. Kwa hiyo, msisitizo uwe kwenye Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba tafiti zinazofanywa na watafiti zinawafikia wananchi wote hasa wale wa chini. Basi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Paulina Nahato. Mheshimiwa Paulina Gekul, ah! Mheshimiwa Cecilia Paresso. Wananchanganya hawa wawili. Dakika kumi. *(Kicheko)*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano. Nitajikita katika mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kwenye suala la afya. Ni ukweli usiopingika kwamba, kama wananchi wetu wakiwa na afya imara na Madhubuti, bila shaka Taifa hilo litakuwa ni lenye neema, ni Taifa ambalo litastawi kwa vizazi na vizazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inapaswa ijikite katika afya za msingi, kwa maana ya kwenye Zahanati zetu. Tukiboresha afya inayotolewa, matibabu yanayotolewa katika Zahanati zetu, kwa hakika huu msongamano ambao tunaukuta kwenye Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa kwa kiwango kikubwa tutapunguza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijisifia hapa kwamba imejenga vituo vya afya vingi na kadhalika na imeeleza mambo mengi, imejenga vituo vya afya vingapi. Sawa, mmejenga, lakini vipi kuboresha huduma zinazotolewa katika zahanati zetu? Tukiweka mkakati wa kuhakikisha zahanati zetu zina maabara ya kutosha yenye vifaa vyote vinavyotakiwa, watumishi wa afya wanakuwepo kwenye *level* kabisa ya chini ya zahanati. Pia kuhakikisha miundombinu yote kwa maana ya nyumba za Madaktari, Manesi, barabara inayoelekea kwenye hivyo vituo, kuhakikisha vinapitika mwaka mzima, maana yake tutakuwa tumemsaidia mwananchi yule wa chini kabisa ambaye anakaa karibu kabisa na zahanati.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba, mwananchi wa kawaida akiagua huduma yake ya kwanza ni kwenye

zahanati kwa sababu pia iko karibu na yeye, anaweza kuifikia, tofauti na hata akitaka kutafuta huduma hiyo kwenye ngazi ya kituo cha afya. Kwa hiyo ni vema sana Serikali ikaona umuhimu wa kuwekeza na kuweka nguvu kubwa kwenye huduma ya afya katika ngazi ya msingi ambayo inamgusa mwananchi moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna mada hapa asubuhi, mjadala mkubwa kuhusu ununuzi wa ndege na Shirika letu la Ndege. Mpango sasa hivi unaonesha kuna kununua ndege zingine nne, wanaweza kufikiria kuacha kununua hizo ndege, zilizopo tuziboreshe, hiyo fedha tukapeleka kwenye zahanati zetu kuziboresha moja kwa moja tutakuwa tumemgusa Mtanzania wa chini kabisa kwa sababu sio Watanzania wote ambao kwa namna moja ama nyingine wanaweza kuwa na mwingiliano au kufaidika moja kwa moja na ndege tutakazonunua, lakini ukiboresha zahanati kwa namna yoyote ile umemgusa yule mwananchi wa chini kabisa, yule mpigakura wetu, yule mwenye uhitaji wa kutosha wa kuhakikisha anapata huduma bora katika zahanati zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine katika Sekta ya Afya, ningependa kuchangia pia kuhusiana na suala la magonjwa yasiyoambukiza. Asilimia 33 ya vifo vinavyotokea hapa nchini vinatokana na magonjwa yasiyoambukiza. Magonjwa yasiyoambukiza wataalam wanasema yanatokana na *lifestyle*, namna tunavyoishi, ukiacha mengine ya kurithi na kadhalika, lakini mengi ni namna gani tunavyoishi, *pressure*, sukari, moyo, saratani, figo na kadhalika na ndivyo nilivyosema kwamba asilimia 33 ya vifo vinatokana na magonjwa ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, haya magonjwa yasiyoambukiza, kama Serikali ikaweka mkakati wa dhati wa kuhakikisha tunawekeza kupunguza magonjwa haya yasiyoambukiza kwa kushirikiana na jamii na wadau wengine bila shaka tutapunguza vifo hivi, hata mwisho wa siku ule msongamano wa wananchi wetu kukimbilia huduma zote ambazo zinatakiwa kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali za

wilaya za kanda na za rufaa utapungua, kwa sababu tutakuwa tumejikita katika kuona namna gani tunapunguza magonjwa haya yasiyoambukiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi leo wote ambao tumesoma bila shaka tulikuwa tunafahamu, leo mtoto yeyote au hata sisi tuliosoma enzi hizo tunafahamu kabisa tunaambiwa, unapata malaria kwa sababu utang'atwa na mbu, ipo ni masomo yanafundishwa, ni mtaala upo na unafundishwa na watoto wanakua wakijua kabisa niking'atwa na mbu nitapata *malaria*. Sasa vivyo hivyo Serikali inatakiwa kufikiria kuingiza mtaala wa namna gani mtoto huyu anakuwa akifahamu kwamba kuna magonjwa yasiyoambukiza na naweza kukabiliana nayo kwa elimu nitakayoipata. Kwa hiyo ni vyema sana Serikali ikafikiria katika mpango wake namna gani ku-*appear* kupitia mitaala yetu kuingiza jambo hilo na lenyewe likawa sehemu kama ambavyo tunafundishwa kuhusu malaria na mambo mengine mengi, mwisho wa siku tutakuja kuona, inawezekana tusiyaone matokeo kwa muda mfupi, lakini kwa muda mrefu tukaona matokeo ya kile ambacho tunakieleza. Kwa hiyo ni muhimu sana Serikali ikaweka mpango thabiti wa kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, pia kutoa elimu kwa jamii ni muhimu sana. Kuna wataalam walikuwa wanatupa takwimu sisi Kamati yetu. Wanasema ni fahari leo kwa sisi wazazi unamchukua mtoto wako unampeleka asubuhi na gari lako kwenda shuleni na anarudishwa nyumbani jioni. Akifika anakaa kwenye kochi, anasema mama nataka chipsi mayai anapewa, anakaa kwenye kochi, labda mzazi ana na *tablet* kidogo anachezea, anaangalia *TV*, inafika jioni anakula analala, yaani hiyo inakuwa ni *lifestyle*, kumbe mtoto huyu anaandaliwa mazingira ambayo mwisho wa siku katika ukuaji wake anaanza kupata magonjwa yasiyoambukiza. Uzito kupita kiasi, sukari mwisho wa siku hata uwezo wa kufikiri na kuchanganua mambo unapungua kwa sababu ya *lifestyle*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapa iko haja ya Serikali kwa kushirikiana na jamii kutoa elimu ya kutosha, yaani tusione

kwamba huo ndiyo ukisasa au ndiyo *style* Fulani, wale wataalam wamekuja wametuambia kwamba walivyofanya utafiti kwenye aina ya wazazi ambao wanahudumia watoto wao kwa namna hiyo na yule ambaye anapanda daladala asubuhi kwenda shuleni, wakakuta kwamba mtoto huyu ambaye mzazi wake anamlea kama mayai ana-*risk* kubwa sana ukilinganisha na yule ambaye atapambana kivyake kutembea kwenda shule au atapambana kwenye daladala kwenda shuleni, yule *automatic* atajikuta mwili wake unafanya kazi kuliko hata yule ambaye tunampeleka asubuhi na gari kwenda shuleni na anarudishwa na gari na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niishauri Serikali katika mipango yake hii, lazima iangalie namna bora ya kuigeuza jamii yetu kulingana na maisha tunayoishi leo. Unaona tunafurahi kwenda kwenye ma-*supermarket* makubwa unaingia labda hapo *shoppers*, unaenda *Mlimani City* na kwingineko, tunachukua samaki waliohifadhiwa kwenye makopo, basi tunaonekana kama ndiyo tuna maisha fulani mazuri, kumbe tunajiandalia matatizo. Yaani mtu anayeenda maeneo hayo anaonekana ni bora kuliko yule anayeenda Majengo pale sokoni Dodoma. Kumbe yule ni bora zaidi kwa sababu anapata kitu *fresh!* Anapata matunda *fresh* kutoka shambani, anapata labda samaki *fresh*, nyama ya ng'ombe *fresh!*

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni kuangalia namna gani tunabadilisha *mind-set* ya jamii tunayoiongoza, Serikali wakaweka kitengo maalum au fungu maalum kwa kushirikiana na wadau, kushirikiana na jamii na viongozi sisi wa kisiasa, tukaendelea kuibadilisha jamii yetu kuishi kwenye *lifestyle* ambayo itatusaidia ili mwisho wa siku tuepukane na magonjwa yasiyoambukiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili inajikita katika Sekta ya Utalii. Bila shaka Serikali na wadau mbalimbali tumeona kwamba jinsi gani ambavyo *corona* ilivyofika imeathiri kwa kiwango kikubwa Sekta ya Utalii na imeathiri mpaka yule mtu mmoja mmoja ambaye anategemea utalii

ule. Naongea hivyo kwa sababu natoka Mkoa wa Arusha na nafahamu jinsi ambavyo watu katika Sekta ya Utalii wameathirika kwa kiwango kikubwa. Sasa huko nyuma tuliongea na kuishauri Serikali iangalie namna gani ya kuweka mipango, inapotokea dharura za namna hii wafanyabiashara na wale wanaonufaika moja kwa moja na Sekta hii ya Utalii wapunguziwe mambo fulani fulani yanayowaumiza.

Mheshimiwa Spika, mfano, hoteli nyingi zilifungwa wakati wa *corona*, nyingi mno kukawa hakuna wageni, wakapunguza wafanyakazi lakini mwekezaji au mtu yule mwenye hoteli hajawahi kupunguziwa kodi na Serikali hata siku moja, tena alitakiwa alipe na wengine kodi zikaongezeka. Sasa sina uhakika sana kama tunataka kweli kuendeleza utalii ambao unachangia pato kubwa la Taifa au tunataka kuumaliza na kuukandamiza.

Kwa hivyo nishauri kwamba ni vyema panapotokea majanga ya namna hiyo, hatuyaombe lakini yanaweza yakatokea, ni lazima kwenye Sekta ya Utalii pamoja na sekta zingine Serikali iwe na mipango ya kuhakikisha inatoa unafuu au kwa mwekezaji mmojammoja au wawekezaji kwa ujumla ambao moja kwa moja wanaungana, kunakuwa na mnyororo wa moja kwa oja ambao unamgusa mwananchi mpaka chini kuhakikisha inatoa unafuu wa mambo fulani fulani ambayo yatamfanya mtu huyu aweze kuendeleza biashara ile ambayo anaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado inatakiwa mikakati ya kuendeleza na kukuza utalii wetu. Bado tunahitaji kuwa na mikakati mizuri ya kuhakikisha Serikali inapata mapato katika utalii wa picha, hatujawekea mkazo na huko nyuma ripoti ya CAG zimeeleza mara nyingi kwamba Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kwa sababu haiweki mpango thabiti wa kuhakikisha utalii wa picha unatuingizia pato na kuhakikisha unasimamiwa vizuri. Vivyo hivyo kwenye Sekta ya Uwindaji pia inapaswa kuwekwa mipango thabiti ya kuhakikisha kwamba inaingiza kodi ambayo mwisho wa siku itatusaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kidogo pia kuhusu Serikali zetu za Mitaa hapa nchini. Halmashauri zetu nyingi zimepokonywa mapato, mwisho wa siku zinashindwa kujiendesha, mwisho wa siku ufanisi unaotarajiwa hauwezi kufikiwa kwa sababu hamna mapato yale yanayokusudiwa. Kwa hiyo niishauri Serikali, kuna mapato ambayo Serikali iliyachukua haiwezi hata hiyo *TRA* yenyewe kukusanya bado imekuwa ni changamoto, niishauri irudishe kwenye Serikali za Mitaa. Ikirudisha kwenye Serikali za Mitaa pawepo na usimamizi thabiti, pawepo uhakika kwamba kile kilichorudishwa kinatumika moja kwa moja na kinafanya kazi ambayo inakusudiwa. Hiyo itatusaidia sana kwa sababu kwenye wananchi ni kwenye Serikali za Mitaa, ndiyo tunamgusa mwananchi moja kwa moja kule chini. Ukiziwezesha na kuzisaidia halmashauri zetu moja kwa moja umemgusa Mtanzania. Kwa hiyo ni vyema sana Serikali ikalitazama jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, mno! Ripoti ya *CAG* na taarifa mbalimbali...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. Ripoti mbalimbali zinaonesha kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi vivyo hivyo basi ni vyema Serikali ikahakikisha watumishi wanapatikana. Watumishi wa kutosha wakiwepo, ukirudisha mapato, ukasimamia vizuri, matokeo tunayoyatarajia kwa nchi yetu yataweza kufikiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso. Mheshimiwa Dkt. Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa David Mwakiposa. Dakika tano, tano tuendelee.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia.

Pia nimshukuru sana Dkt. Mwigulu pamoja na timu yake kwa kuja na huu Mpango mzuri sana. Mapendekezo yangu yatajikita kwenye usimamizi wa miradi ya kimkakati. Wewe mwenyewe unatambua kwamba tumefanya mambo makubwa sana katika nchi hii katika miradi ya kimkakati ukiwepo ununuzi wa ndege zaidi ya 10, ujenzi wa reli ya kisasa, lakini vile vile tunategemea kuanza ujenzi wa bandari mbalimbali hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hapa Dodoma tumekuwa na miradi ya kimkakati mingi sana. Hivi karibuni wenzetu wa Jiji la Dodoma wamemaliza ujenzi wa hoteli kubwa sana ambayo itakuwa *five star* haya yote ni maendeleo makubwa sana ambayo yameletwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Sasa hoja yangu ni kwamba, katika hii miradi ya kimkakati ambayo ni uwekezaji mzuri sana kwa nchi yetu, lakini nalitazama katika upande wa usimamizi. Kwa sabbau tayari tuna sera ya *Public Private Partnership*, Sera ya Ubia kati ya Serikali pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo hususan *Private Sector*, lakini tuna sheria ya ubia kati ya *Public Sector and Private Sector*. Nadhani ni muda muafaka sasa sisi kama Serikali tuangalie jinsi gani tunaenda ku-*capitalize* kwenye hii sera ili tuweze kuisadia Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwa mfano, tuna mradi mkubwa hapa Dodoma wa hoteli, hoteli ya *five star*, je, tunaenda kutumia *business modal* gani kuhakikisha kwamba ile hoteli inaenda kufanya kazi vizuri. Kwa nini tusingie kwenye huu ubia sasa wa *Private Sector* na *Public Sector* tukaangalia ni maeneo gani ambayo *Private Sector* wana uwezo nayo tukawaachia, halafu yale maeneo ambayo sisi tuna uwezo nayo tukayafanyia kazi. Hilo ni la kwanza ningependa kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, lingine, tuna miradi mingine ambayo ni mikubwa tunaifanya. Sasa hivi tunasisitiza suala la *Public Private Partnership*, naomba nimshauri Waziri kwa nini wasiunde *task force* ikaenda kupitia miradi yetu yote ile mikubwa wakaja kuishauri Serikali kuja na *business modal* ya jinsi gani tunaweza ku-*manage* hii miradi. Kwa nini tusiende

kwenye ile *management contract* kwamba eneo ambalo Serikali tuna uwezo nalo tutalifanyia kazi, lakini yale maeneo ambayo Serikali hatuna uwezo nayo, nashauri tunahitaji kuchukua maamuzi magumu ili kuhakikisha kwamba *Private Sector* na yenyewe ili iweze kukua tunahitaji kuigawia sehemu ya ile miradi ili waweze kuisimamia. Kuna faida nyingi katika hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunaenda kukuza ajira; Pili, tunaenda kukuza mahusiano kati ya *Public Sector* na *Private Sector*; na Tatu, itatufanya sisi tulale. Badala ya Waziri wa Fedha kulala anawaza kwamba sijui mradi huu haufanyi vizuri, una-*transfer risk*, unampelekea mtu mwingine, kazi yetu inabaki kukusanya kodi lakini vile vile kuangalia gawio letu mwisho wa mwezi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, naomba kwamba Serikali ichukue haya maoni yangu na iyafanyie kazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Dkt. Chaya, nakushukuru sana kwa ushauri huo mwema. Mheshimiwa David Mwakiposa, tafadhali, halafu Mheshimiwa Abdullah Mwinyi atafuatia.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kwa Mpango huu ambao umeandikwa vizuri sana. Nitajikita kwenye sekta moja tu ambapo nizungumzia mahusiano kati ya Mpango hu una Sekta ya Ujenzi. Kabla sijafika huko, labda nimnukuu mmoja wa waasisi wa Marekani aliyekuwa anaitwa Benjamin Franklin ambaye aliwahi kutuambia kwamba *falling to plan is planning to fail*, unapokosea kupanga, basi unapanga kushindwa.

Mheshimiwa Spika, niungane kwanza na mtangulizi mmoja aliyezungumza pale juu kwamba tuweke mfumo mzuri wa kufuatilia, je, tunayokubaliana hapa yanatekelezwa? Mambo ya kimkakati na yenye tija sana yanapewa uzito sawa na Wabunge tunavyopendekeza? Hilo nataka iwe kama angalizo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Mpango katika maeneo ya kipaumbele, eneo namba mbili linazungumza linasema; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma. Pia ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wetu, kwenye malengo mahsusi, namba tatu anasema:

“Kujenga uchumi wa viwanda kama msingi unaoongoza mauzo ya nje ili kuimarisha Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, SADC na Central.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tumekubali, tumeamua kujenga nchi ya viwanda. Lazima pia tunapotamka hilo tukubaliane, tunatamka viwanda kama *theories* au tunatamka viwanda kiutendaji. Nitajikita kwenye maeneo machache kama nilivyosema na pengine labda ningeshauri na Wabunge wakasome tafiti ya mtu mmoja anaitwa Peter Samuel Abdi ambaye anasema anahusianisha *infrastructure* na *Industrialization*, jinsi vitu hivi vinavyokwenda pamoja. Naomba nijikite kwenye ukanda wa viwanda. Kama tunataka nchi yetu twende kwenye viwanda na mwaka 2015 hapa wakati Hayati anahutubia alisema angependa kuona mwaka 2020, Sekta ya Viwanda itoe asilimia 30 ya ajira. Tulipofanya tathmini mwaka jana tukabaini asilimia nane inatokana na ajira kwenye viwanda. Hakuna anayejiuliza, hii asilimia 22 tumekwama wapi? Naomba niende kwenye kesi ya upande kwa mfano wa viwanda pale Mufindi.

Mheshimiwa Spika, pale Mufindi ikiwa inawakilisha sehemu zingine za nchi hii, maeneo ambayo yamejitenga yenyewe kuwa ya viwanda pale kuna viwanda karibu 10 na viwanda hivi viko kuanzia miaka ya 1961 vilianza. Vinalipa kodi zaidi ya bilioni 40 takriban, naweza kukutajia kwa uchache. Kuna Kiwanda cha Karatasi, hiki kinatengeneza karatasi hapa nchini kwetu na kupeleka nje. Kuna Viwanda vya Nguzo, kuna Viwanda vya Chai vimekusanyana pale. Sasa niwaombe wenzetu wa Sekta ya Ujenzi Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi yuko pale, Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko pale; maeneo kama haya ambayo wakiyakusanya yanaweza kuingizia Taifa bilioni 40, lakini tunayasoma kwenye

takwimu pia kwamba katika miaka hii, kati ya viwanda 23 vya mbao peke yake, viwanda karibu 23 kati ya 27 vilikufa, hakuna anayejiuliza sababu ya kufa ni nini? Ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake walifanyie tathmini jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pia tunaposema tuimarishe Sekta ya Viwanda kama msingi wa kuongoza nchi yetu, tunamaanisha magari yanayopangana barabarani zaidi ya 200 kila siku kipindi cha mvua, yatapita kiurahisi, utasafirisha bidhaa zako kutoka kiwandani mpaka nje. Kumbuka viwanda hivi vinapeleka bidhaa ndani ya nchi yetu na nje ya nchi yetu. Unahangaika kuanzisha viwanda vingine wakati vile vilivyopo mahitaji yake 50 ikiwemo barabara hujajenga, *are we serious? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu, kwa kuwa agenda ya viwanda iliiasiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa kuwa, iliendelezwa na watangulizi wake mpaka Mheshimiwa Mama Samia sasa, Rais wetu wa Awamu ya Sita. Na kwa kuwa maeneo kama yale yametajwa kwenye Ilani ya CCM ninaomba tuyape kipaumbele ikiwezekana tuimarishe miundombinu yake, tujenge barabara, tupeleke umeme, tupeleke maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya siku moja ziara pale, unamkuta mwenye kiwanda anasema bwana mimi hapa kodi inayolipa ni dola milioni mbili karibu nukta mbili, lakini shida yangu kubwa tazama huko nje hali ilivyo mbaya, sina barabara, anakwambia lakini umeme hapa ndani hautoshelezi.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu, kwa kumaliza. Kwa kuwa, maeneo kama haya yametajwa kwenye Ilani ya CCM kuanzia 2005 mpaka sasa. Kwa kuwa, Mwalimu Nyerere aliahidi. Kwa kuwa, Rais Kikwete alirudia, kwa kuwa, baba yetu hayati Dkt. Magufuli ameyazungumza tena mwaka jana. Namna nzuri ya kuwaenzi viongozi hawa ni kuanza kutenda kusema inatosha. Tutakuwa na mipango hapa, tunakaa hapa ndani tunazungumza utekelezaji hauonekani wa

baadhi ya maeneo. Kimshingi maeneo ambayo sisi huku nje tunakuwa hatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana labda kuna maelezo mazuri kama kwa kutumia msemu wako. Kunaweza kuwa na maelezo mazuri sana ya kwamba, barabara hizi hatuwezi kuzijenga kwasababu hizi na hizi na hizi, lakini sisi hatuelewi. Eneo hili limeajiri watu karibu elfu kumi, eneo hili linalipa kodi zaidi ya bilioni 40, eneo hili magari yanayopita na ajira pengine, n.k. shida ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuhitimisha ninaunga mkono hoja, lakini naombeni maeneo ya kimkakati tuyatazame kwa njia ya kipekee. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa David Mwakiposa. Nilishakutaja Mheshimiwa Abdullah Mwyni na utafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Chege.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. ningependa kuanza mchango wangu kwa kutoa salamu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumepoteza Rais wetu, amefariki Rais wetu wakati yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili halina rejea ndani ya nchi yetu katika historia ya nchi yetu na si jambo jepesi kwa Rais kufariki katika nchi changa kama hii ambayo wapinzani wetu wanasema hatuna mfumo wa utawala bora, lakini amefariki Rais.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Serikali pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha Katiba na mfumo mzima wa utawala bora unasimamiwa na hali yetu mpaka Rais wetu mwingine aliyekuja akashika wadhifa bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi wamepata changamoto kama hizi na ikasababisha machafuko. Hili si bure, haya ni ukomavu wetu wa Serikali yetu chini ya Chama

chetu Cha Mapinduzi ambayo imewezesha utaratibu na kuonesha dunia nzima kwamba, sisi ni wakomavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeupitia mpango pamoja na kusikiliza hotuba za hivi karibuni za Mheshimiwa Rais. Na mambo ya msingi ambayo ningependa kuyachangia ni matatu, la kwanza ukimsikiliza Mheshimiwa Rais vipaumbele vyake ni vitatu cha kwanza ni kurekebisha mfumo wa biashara. La pili ni kuimarisha zaidi mahusiano kikanda na ya kimataifa na cha tatu ni kuhakikisha miradi yetu ya mkakati inakamilika. Hayo mambo mawili ya mwanzo yakifanyika vizuri ndio yatahakikisha hili jambo la tatu, miradi ya mkakati, itakamilika kwa salama na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwasababu muda si rafiki mimi ningependa kugusia suala la kwanza kuboresha mfumo wa biashara. Ukiungalia mpango mzima na *section* kubwa ya kuhusu *business environment* utaambiwa tumepitia kitu kinaitwa *blue print*; kila uki-*question* jamani tumefika wapi, tunafanya nini, *blue print implementation* imefika wapi?

Mheshimiwa Spika, utaambiwa ikikamilika mambo yote hayo unayoya-*raise* yatakuwa sawa. Sasa wenzangu humu ndani ya Bunge walilizungumzia suala la *monitoring* na *evaluation*. Ili tuweze kurekebisha yale matatizo tuliyokuwanayo lazima tuwe na taasisi rasmi ama hapa Bungeni chini ya kamati moja au Serikalini na sehemu bora zaidi ni chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwasababu, yeye ndio kiongozi wetu katika shughuli za kila siku za Serikali. Lazima tuwe na taasisi ambayo inahakikisha *quarterly* tunafanya *monitoring* na *evaluation* kwa yale ambayo tumeyapanga. Bila kuboresha mfumo mzima wa kibiashara *revenue* hazitakuja zile ambazo tunategemea, biashara haitakua, uwekezaji hautaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa sehemu hii ni sehemu ambayo ni nyeti sana ambayo ningependa kuunga hoja za miongoni mwa wenzetu ambao wamezungumzia kwamba, ama tufanye sehemu mbili Bunge liwe lina-*monitor* pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba, yale ya

kimkakati, *reforms tangible* kwasababu, kuna *projects* ambazo unaona kama kitu kimejengwa hakijajengwa, lakini kuna mfumo wenyewe inabidi ubadilishwe uwe rafiki zaidi kwa ajili ya kukaribisha uwekezaji. Kwa hayo machache ningependa kushukuru kwa fursa hii na napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri, hakika kila mtu humu ndani anajua, hili jambo la mfumo wa kibiashara yaani tumelisema sana, tunategemea wahusika watatuambia kidogo. Haya maneno ya *blue print* safari hii iko wapi? Kwasababu, ni kweli tusipobadilisha mfumo wa kibiashara kuwa *competitive* itakuwa ngumu kidogo. Asante sana Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

Mchangiaji wa mwisho upande wa Wabunge atakuwa Mheshimiwa Jafari Chege. Baada ya hapo tunaanza na Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, atafuatiwa na Waziri wa Mifugo.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Niseme tu kwa kuwa, hapo nyuma nilishapata nafasi ya kuchangia, hasa kwenye upande wa shughuli za kijamii, kwa maana ya maji, umeme na shughuli nyingine. Leo kwenye mpango nilitamani sana nijikite eneo moja la ardhi pamoja na makazi.

Mheshimiwa Spika, kwenye mpango natambua tumeiweka kwamba, Serikali ina mpango wa kuhakikisha angalao eneo lililosalia ambalo halijapimwa kwa ukubwa wa eneo letu zaidi ya 880,000 kilometa za mraba tumepima eneo zaidi ya asilimia 25 peke yake. Lakini kwenye mpango umetamka namna gani ambavyo kwa miaka hii mitano tunajikita kwa ajili ya kutambua, kupanga pamoja na kupima.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitamani nishauri kwasababu, uliwahi kusema hapa ndani na mimi niendele kuisema kama tukiitumia ardhi yetu vizuri, tukiipima vizuri ardhi

yetu naamini kwa sababu, ni mdau wa sekta hii ya ardhi naamini inawezekana ndio kikawa chanzo kikubwa sana cha mapato ndani ya nchi yetu hii Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nishauri? Nini tufanye kutokana na mpango uliopo? Cha kwanza. Ipo idara ambayo inasimamia shughuli za kupanga, kupima pamoja na kurasimisha ardhi ambayo iko chini ya Wizara ya Ardhi.

Tulivyokuwa na changamoto ya maji vijijini tulianzisha chombo cha kushughulika na changamoto za maji, *RUWASA*. Tulivyokuwa na changamoto za barabara vijijini tulianzisha *TARURA*, tulivyokuwa na changamoto za umeme tulianzisha *REA*.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri baddala ya kuwa na idara ambayo imejificha ndani ya wizara inayoshughulika na kupanga, kupima na kurasimisha haya maeneo, twende tuone namna gani tunatengeneza *agency* iwe wakala inayojitegemea ambayo kazi yake kubwa sasa iwe ni kupima na kuendana na mpango wa Serikali huu uliopangwa wa miaka mitano. Tukifanya hivyo, maana yake ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza itakuwa na wigo mpana wa kushirikiana na sekta na taasisi nyingine. Hii migogoro tunayoizungumza ya ardhi kati ya wananchi na jeshi tukiwa na wakala anayejitania maeneo yake maana yake atafanya kazi kubwa, lakini ataendana na kasi ya sisi tunayoizungumza kwamba, kwa muda mfupi asilimia 75 ya ardhi iliyosalia iweze kupimwa ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili. Mpango ujikite uone namna gani unaweza ukashirikisha halmashauri moja kwa moja. Pamoja na kwamba, halmashauri nyingi zina vyanzo vingi vya mapato ningetemani sana mpango upeleke maelekezo moja kwa moja kwamba, halmashauri zirudi sasa zitambue kupanga na kupima maeneo yao ya ardhi, ili angalau moja kuongeza mapato, lakini mbili kama mnavyotambua tukipanga na tukipima eneo tunapunguza

migogoro, kwa kufanya hivyo maana yake tutaipunguzia Wizara mzigo.

Mheshimiwa Spika, wizara sasa inafanya kazi kubwa sana ya kutatua migogoro badala ya kuibadioisha ardhi iwe *source* au chanzo cha mapato kwenye Serikali yetu. Ningetamani, sasa kwasababu Mheshimiwa Waziri ameshafanya kazi kubwa sana ya kukimbizana na migogoro aende aifanye sasa ardhi iwe ni sehemu ya kuongeza mapato, ili angalau mwisho wa siku tuweze wote kufaidika na sekta hii ya ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa miezi nane peke yake, kuanzia mwezi wa nane mpaka sasa Wizara imeingiza zaidi ya bilioni 93. Unaweza ukaona asilimia 25 ya ardhi iliyopimwa peke yake tuna bilioni 93, lakini asilimia 77 kati ya 880,000 ya ardhi ambayo haijapimwa tujiulize leo ardhi yote tukiipima kukawa na usimamizi thabiti ambao tukawa na mawakala ambao wanashughulika moja kwa moja na wanawajibika kabisa na upimaji na urasimishaji wa ardhi, Serikali itakusanya kiasi gani cha fedha kupitia sekta ya ardhi peke yake?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili. Nizungumzie kuhusiana na hii ni Wizara ya Ardhi pamoja na Makazi, niende sasa kuzungumzia kuhusiana na nyumba. Wabunge wengi tumekuwa tukilalamika hizi *real estate developers, National Housing, TBA* na watu wengine ambao wamekuwa wakijenga nyumba kwa gharama kubwa. Na wengine tulikuwa tukihoji hapa kwamba, *affordability* ya nyumba inapatikana wapi?

Mheshimiwa Spika, haya yote tunashindwa kufika mwisho kwasababu, hatuna *housing policy*. Tunazo sera za misitu na sera za nyuki na sera nyingine, lakini hatuna sera inayotudhibiti na inayotuongoza kwenye nyumba, ili mwisho wa siku *National Housing* wakijenga nyumba Rorya, tukisema nyumba ni ya bei nafuu iwe angalau tayari ina *limit* kwa sababu, tukiwa na *policy* maana yake tutatengeneza sheria. Akijenga Rorya nyumba ya milioni 20 tutakuwa tunajua kabisa hii kweli milioni 20 ni *affordable*. Akijenga Kongwa nyumba

ya milioni 20 tunaweza tukamhoji, hii ni *affordable* nyumba ya vyumba viwili?

Mheshimiwa Spika, kwasababu, kutakuwa kuna sheria inayomuongoza yeye katika ujenzi, sasahivi hakuna sheria. Anaweza akajenga nyumba akai-*term* kama *affordable*, ukimuuliza kwetu sisi, mimi inaweza isiwe *affordable* milioni 50, lakini kuna mtu mwingine milioni 50 kwake ni *affordable*. Na kwasababu hakuna *policy* wala sheria inayomuongoza inakuwa ni wakati mgumu sana kujua sasa wapi Serikali inasimamia kusema *affordability* ya nyumba ni ipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na huu utakuwa ni muongozo mzuri kwa *TBA, national Housing* na *real estate developers* wengine wote wanaofanya shughuli za kujenga maeneo. Hata Serikali kwa maana ya kupitia Wizara itakuwa na sehemu ya kujivunia, unapokwenda ukasema unaonesha nyumba za *affordability's* unaonesha kulingana na uhalisia uliopo.

Mheshimiwa Spika, sio uwongo gharama za ujenzi wa kila maeneo zinatofautiana. Gharama ya ujenzi wa Rorya haiwezi kuwa sawa na gharama ya ujenzi wa Dar-es-Salaam. Kwa hiyo, maana yake ile ukii-*term* kwamba, huyu mtu ambaye anajenga nyumba ajenge nyumba ya *affordability* Rorya ya milioni 30 ukasema sio *affordable* atakuuliza ni sheria ipi inayomuongoza? Kwa hiyo, ningependa nichukue nafasi hii kuiomba sana Wizara, lakini kupitia Waziri wa mpango, Waziri wa Fedha, ilia one namna gani ile sheria, ile *policy* inaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ni kwenye *RERA, Real Estate Agency*. Leo kuna watu sio vizuri kuwasemea, hawa tunaowaita madalali; *brokers* leo akiuza ardhi akiwa mtu wa kati hata kama ardhi ni ya milioni 500 akichukua *commission* hakuna kodi anayolipa. Lengo letu ni nini?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natamani sana tutengeneze *Real Estate Agency*, tutengeneze *Real Estate Regulations* ambazo zinawa-*guide* hawa ma-*brokers* na

hawa ma-*Real Estate Agency*, ili mwisho wa siku moja itasaidia ku-*regulate*, lakini mbili itasaidia kukusanya kipato ambacho anashiriki kwenye kuuza kama mtu wa kati, lakini tatu itakuwa ni fursa kwao kufanya shughuli za kibiashara kwasababu, sasa watakuwa wanatambulika wako wapi. Leo ni ngumu sana kumtambua *broker* yupo wapi na anafanya kazi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Asante sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege. Mheshimiwa Abubakari Asenga, tafadhali tumia hizo dakika tano za mwisho kabisa.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii kama ya bahati nasibu kuchangia mpango wetu ambao lengo la mpango huu ni kuwa na uchumi wa viwanda ambao unaenda sambamba na kilimo. Na unavyosema kilimo katika nchi yetu huwezi kuacha mkoa mikubwa ile ambayo inajishughulisha na kilimo na mkoa mmojawapo ni Mkoa wa Morogoro ambao unashikilia takribani asilimia 7.7 ya ardhi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi kwa kifupi kabisa tunaomba Mheshimiwa Waziri kwamba, katika mkoa tulikaa tuna mpango mkakati wa maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi Mkoa wa Morogoro. Kitabu hiki kina kila kitu, kimeelezea fursa mbalimbali ambazo zitasaidia sana Mheshimiwa Waziri kufika katika malengo yake ya mpango. Na tumesema fursa zilizopo katika mpango huu tukiunganisha mpango na kitabu ambacho mwaka 2020 tulikiombea kura kwa wananchi, yaani Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka mpango huu ufanikiwe katika kupanga ni kuchagua mara zote nimegusa kwa mfano suala la kilimo cha miwa tu peke yake. Nimesema kuna miwa Kilombero tani takribani 300,000 zinalala zinasalia na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Baba yangu Profesa Mkenda, tuliendanaye ameona hali halisi.

Wawekezaji wale katika Kiwanda cha Ilovu cha Kilombero cha sukari kwa mfano kwa sasahivi wanatafuta takribani bilioni 400 kukuza, kupanua kile kiwanda kiweze kuchukua miwa ile tani 300,000 ambayo miwa hiyo tani 300,000 ikichakatwa itazalisha tani elfu 30 mpaka 35 za sukari.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu leo inaingiza tani 40,000 za sukari, tukiweza kuchakata miwa ile ambayo ipo yani sidhani kama kuna mpango ambao unaweza kwenda kutuelekeza sehemu nyingine kwenda kupanda miwa, kuanzisha mradi mpya, lakini huku kuna watu akina Balozi Mpungu Mwenyekiti wa Bodi wanatafuta bilioni 400, bilioni 500 wapandue kiwanda kitumie miwa ambayo tayari ipo ya wananchi na nchi yetu isiingize tena sukari. Maana hapa keshokutwa tunaenda kwenye uhaba wa sukari watu wataanza kuingiza sukari, tunaingiza tani 40,000 wakati miwa inabaki tani 300,000.

Kwa hiyo, nisisitize tu Mkoa wa Morogoro una fursa nyingi. Kwenye kitabu humu tumesema kuna mashamba 12 makubwa. Tunahitaji bilioni 100 tu kwa mwaka huu akitutafutia Mheshimiwa Waziri tuta-*push* mpango wetu.

Mheshimiwa Spika, tuna hekta zinazofaa kwa kilimo milioni 2.2 tunatumia asilimia 43 tu, 900,000 ndio tunazolima. Tuna hekta zinazofaa kwa umwagiliaji 323,000 zinafaa kwa umwagiliaji tunalima 28,000. Sasa kam kweli tuna mpango tunataka ku-*boost* uchumi wetu wa nchi yetu na tunasema uchumi wa viwanda tunauunganisha na kilimo basi Mkoa wa Morogoro utazamwe, Wizara na wasimamizi wote wa sera watusaidie kupata fedha kuongezea halmashauri zetu fedha ili tuweze ku-*deal* na kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwenye miwa, kuna mpunga, amesema hapa *brother* wangu, pacha wangu Mheshimiwa Kunambi. Upande wake sasa hivi jeshi linatengeneza mradi mkubwa sana wa umwagiliaji. Kwa hiyo, kwa nafasi hii nilikuwa naomba baadaye nitamkabidhi kwa sababu, dakika ni chache, nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri kitabu hiki atusaidie.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuna miradi mkakati, sisi Halmashauri yetu ya Mji wa Ifakara ime-*qualify*na tumeomba takribani miaka miwili mitatu iliyopita kwamba, kama malengo mojawapo ni halmashauri zijitegemee, sisi tume-*qualify* kupata soko pale Mjini Ifaraka ni mji mkubwa sana. Kwamba, soko lile tukipewa zile fedha tulizomba takribani bilioni tano zitarejeshwa ndani ya miaka mitano na halmashauri yetu itapata mapato makubwa. Tunaomba hilo Mheshimiwa Waziri nalo alifikirie.

Mheshimiwa Spika, la pili. 2018 Mheshimiwa Rais, Hayati, alivyokuja kule kuna kiwanda kikubwa kilikuwa cha chuma, cha vifaa vya reli kina hekta 250-kina majengo, ma-*hall*kabisa na mashine zipo ndani yake. Tangu kimerudishwa kile kiwanda kipo *idle*.

SPIKA: Kiwanda cha Mang'ula?

MHE. ABUBAKARI D. ASENKA: Mheshimiwa Spika, cha Mang'ula cha chuma kimekuwa pori. Kuna wawekezaji wamepatikana huko nimemwambia Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Mkenda amenisaidia kuna baadhi amewaona, Mheshimiwa Profesa Mkumbo pia, tuwasaidie tuwaruhusu kama wako tayari kuwekeza hata wakiwekeza kiwanda kidogo cha miwa watatumia hiyo miwa tani laki tatu.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ABUBAKARI D. ASENKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa tunaingia upande wa Waheshimiwa Mawaziri, nitawaomba kila mmoja asizidi dakika saba ili tuweze kwenda pamoja, tujitahidi, itakuwa kengele moja tu. Tuanze na Naibu Waziri Katiba na Sheria halafu atafuata Mheshimiwa Waziri Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria ambaye, leo yuko kwenye majukumu mengine, ningependa nami kuupitia na kutoa mchango unaoendana na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ambao walipata nafasi ya kuchangia maeneo mbalimbali. Kwa upande wa sheria Waheshimiwa Wabunge wamechangia maeneo mbalimbali yanayohusu mtazamo wa kurekebisha sheria mbalimbali ili kuendana na wakati tulionao.

Mheshimiwa Spika, na katika hali ya kawaida wengi wa wachangiaji walikuwa wanaonesha kwamba, bado tuna sheria kandamizi ambazo kimsingi Tanzania haina sheria kandamizi. Na hili nalirudia tena na niliwahi kulitoa katika maelezo yangu wakati nikijibu swali, isipokuwa tunazo sheria mbalimbali ambazo zinatakiwa kupitiwa upya kulingana na wakati tunaokwendanao kwa sababu, hizi sheria hatuwezi tukazikosoa tukaziita sheria kandamizi kwasababu, chombo kinachotunga sheria ni Bunge lako tukufu na hivyo haliwezi kubebeshwa mzigo wa kutunga sheria kandamizi kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wako watu walihoji uhalali wa baadhi ya Watanzania wenzetu waliokamatwa na kuwekwa ndani wakati wa uchaguzi, na inaonekana kwamba haki haijafata mkondo wake, lakini hawa ni wahalifu na wahalifu wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Hatuna sababu yoyote kimsingi ya kumuacha mhalifu akitumia kofia ya siasa kutuharibia usalama wa nchi yetu. Kwahiyo hawa tutaendelea kushughulika nao kwasababu wanahitaji kufuata msingi wa sheria ya nchi yetu *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge waliona ni muhimu sana. Kwa mfano marekebisho ya sheria za mashirika ya umma ambayo yanaonekana yamepitwa na wakati, kimsingi haya ni mapendekezo ambayo Serikali inayachukua kwa ajili ya kwenda kuyapitia na kuona kama kweli hizi sheria zimepitwa na wakati, kama tunavyoendelea sasa kufanya marekebisho

mbalimbali ya sheria katika kuboresha mifumo ya sheria ambayo kimsingi ina mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo yale ambayo yameshuriwa tutayachukua na kuyafanyia kazi ili kuboresha. Na Waheshimiwa Wabunge tujue tu kwamba sheria iliyo bora inayokwenda na wakati ni nguzo imara sana katika kujenga uchumi wa nchi yoyote duniani. Kwahiyo kimsingi niseme kwamba tumepokea yale maeneo yote ambayo yameshuriwa na Waheshimiwa Wabunge, tutayafanyia kazi na chombo hiki hiki kitaletewa kwa ajili ya kupitisha sheria ya marekebisho ili tuweze kwenda na wakati na masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wako Wabunge wengine walizungumzia habari za rushwa. Waheshimiwa Wabunge sisi ndicho chombo ambacho kinaweza kikaondoa rushwa Tanzania. Bahati mbaya sana wakati mwingine sisi wenyewe tukawa hatujanyooka sana katika suala la kuzuia rushwa isiendelee kutendeka nchini.

Mheshimiwa Spika, sisi tukisimama imara sisi ni viongozi wa maeneo madogo madogo sana unaweza ukakuta Halmashauri moja ina Majimbo mawili mpaka matatu lakini sisi huko ndiyo hasa tunakuwa ni chanzo kikubwa sana cha kuji-*involve* kwenye mikataba ya ovyo ovyo huko kwenye maeneo ya Halmashauri zetu, na wala hatusimamii kuzuia rushwa isitendeke. Lakini linakuja Bungeni sasa linabebwa kama vile kuna mtu mwingine mbadala atakayekwenda kusimamia juu ya kuzuia rushwa zisiendelee.

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi tuko hapa kusimama kuisemea Serikali lakini sisi vile vile ni wawakilishi wa wananchi, tumetoka huko. Kama ingekuwa Waheshimiwa Mawaziri ni wakuteuliwa tu kutoka kwenye taasisi nyingine labda wangukuwa hawajui miondoko na mienendo iliyopo kwenye maeneo ya majimbo. Lakini ukweli ni kwamba, sisi tukiamua kuondoka kwenye rushwa tukasimama imara kama Waheshimiwa Wabunge,

na pale linapotokea jambo la rushwa kwenye Halmashauri yako kwenye Jimbo lako tukakuona umesimama Mbunge unazungumza kwa nguvu zako zote mimi naamini baada ya muda suala la rushwa litakuwa ni hadithi tu.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo haya maboresho ya kusimamia haki ambazo zinasababisha vionjo vya rushwa. Ukweli lazima tushirikiane wote, kwasababu hata kama sheria ikiwepo, hapa iko sheria ya kuzuia rushwa lakini rushwa bado zipo, ni kwasababu miongoni mwetu hatuzisemi hadharani, na matokeo yake tunapokwenda kwenye utekelezaji lawama zinarudi Serikalini na kuonesha kwamba Serikali haisimamii vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa Mbunge wewe ni sehemu ya Serikali; na tusipoteze nafasi kwamba sasa baada ya wananchi kukuchagua wewe ni mtumishi wa Serikali moja kwa moja unadhibiti mambo mbalimbali yanayotokea kwenye halmashauri zetu kwenye maeneo yetu ya kata na ya vijiji. Mimi ningeomba tushirikiane sana kwenye eneo hili. Sheria tu kama sheria hata ingekuwepo ya aina gani bila sisi kuisimamia vizuri bado itakuwa ni kazi bure tu.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwenye maeneo haya. Tumeweka taasisi kama *TAKUKURU* tuna vyombo kama Polisi, lakini bila kupewa ushirikiano watu hawa hawawezi kuliiondoa hili tatizo. Sisi ndiyo wengi tunaweza tukafanya ambushi ya kuondoa matatizo yote kwenye maeneo yetu na kimsingi tukaondokana na hii kadhia ya masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu demokrasia wengi wamesema. Lakini sielewi, nahisi labda kuna watu wanaamini kwamba Tanzania haina demokrasia;

Mheshimiwa Spika, lakini nikuhakikishie, demokrasia ya Tanzania huwezi kuikuta mahali popote, hata Uingereza wenyewe hawana demokrasia hii. Wanatawaliwa na Mfalme huwezi kupata demokrasia ya kweli, demokrasia inatoka

kwenye vyombo ambavyo watu wake wanatumia demokrasia ya kuchagua...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana...

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SEHRIA... sisi tunachagua hapa na tunaendelea vizuri kabisa na maisha yetu na wale wanaodai demokrasia kimsingi ebu wajitafiti wao wenyewe kama wana demokrasia ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Pinda, Naibu Waziri Katiba na Sheria tunashukuru sana mawazo yako. Nilikuwa nawaza tu kwenye eneo la rushwa; hivi ile Taarifa ya TAKUKURU kwa nini haiji Bungeni? Sasa Wabunge hawa watajuaje kama ikishafika kwenu halafu basi. Sina maana ujibu maana yangu ni kwamba tushirikishane zaidi mbona ya CAG inakuja kwa nini hii haiji? *(Makofi)*

Tunaendelea, nilishamtaja Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji. *(Makofi)*

WAZIRI NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia ningependa kukukumbusha kwamba siku mbili/tatu zilizopita kulikuwa na mechi kule Egypt na hujatuambia matokeo yake. Labda utatupa taarifa ukipata nafasi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa sana kushukuru michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli ni michango ambayo imesaidia sana kutengeneza Mpango wetu wa Miaka Mitatu ambao ni Mpango wa Tatu wa Maendeleo; na kwa kweli michango yenu tumeichukua na tutahakikisha kwamba tunaifanyia kazi kwenye maeneo yetu ya kisekta, lakini pia kuboresha huu mpango.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba uniruhusu niwataje baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao

wamechangia kwenye eneo la uwekezaji. Kulikuwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka (Mbunge wa Liwale), Mheshimiwa Tarimba Abbas (Mbunge wa Kinondoni); Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa (Mbunge wa Biharamulo) pamoja na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani (Mbunge wa Viti Maalum Ruvuma). Pia kuna Mheshimiwa Hassan Mtenga (Mbunge wa Mtwara Mjini); Mheshimiwa Simon Songe na Mheshimiwa Yahya Mhata, huyu wa Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushukuru kwa michango yao lakini naomba nijielekeze kwenye kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge lakini pia na wananchi kwa ujumla, kwamba Serikali wakati wote imekuwa ikifanyakazi ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwenye nchi yetu. Kama ambavyo mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge mwaka 1999 tulikubaliana kwamba tuunde Dira ya Maendeleo ya miaka 25 (2000 – 2025), tunaita *Tanzania Development Division 2025* ambayo ilianza mwaka 2000, mwaka uliofuatia. Tukawa na mipango midogo midogo ya kimkakati sasa kutekeleza ile Dira ya Maendeleo; na ni kwenye ile dira tulijipangia kwamba mpaka kufika mwaka 2025 tuingie kwenye uchumi wa kati, lakini pia tukiongozwa na sekta binafsi, lakini pia na tukiongeza uzalishaji wetu wa mazao kwa ajili ya kupeleka fedha nje, tuwe na fedha za kigeni nyingi. Pia shilingi yetu iweze kuwa imara, tuwe na mfumuko (*inflation*) ya *single digit*, ikiwezekana twende kwenye chini ya wenzetu kwenye eneo la Afrika Mashariki na *SADC* na tukajipangia mipango mingi ikiwemo kukuza ajira kwa vijana; sasa tunakuwa na mkakati midogo midogo ya kuweza kutekeleza hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna *reforms* ambayo ndiyo nilitaka iwe hoja yangu kubwa. Kwamba tunafanya maboresho kila wakati kama Serikali kwa kupokea mawazo kutoka kwa wadau, lakini pia watekelezaji wa programu mbalimbali za kissekta. Kama mtakumbuka tulikuwa na *Public Sector Reform Program* ambayo iliunda Idara yetu ya Utumishi kipindi kile, lakini pia kuna *Public Finance Reform Program*, pia tulikuwa na *Local Government Reform Program* ambayo

tumetengeneza hizi halmashauri kupitia hizo programu. Pia hata *Legal Sector Reform Program* tuliifanya wakati huo ili kuboresha sheria zetu zindane na mahitaji yetu sisi ya kuwa na uchumi wa kisasa kuendana na malengo ya kwenye Dira ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye kuyafanya hayo tukatengeneza mikakati. Tulikuwa na mkakati mdogo wa miaka mitatu wa kupunguza umaskini lakini tukasema huu mkakati baada ya kupata maoni ya wadau tuupanue zaidi kwa kukuza uchumi na kuupunguza umaskini. Tulikuwa na MKUKUTA, MKUKUTA I na MKUKUTA II wa miaka mitano, mitano kama mtakumbuka. Kwenye MKUKUTA II tukaona sasa tuje na mpango tofauti kidogo, ndipo tukawa na huu Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano ambao Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Nne Dkt. Jakaya Kikwete alizindua mwaka 2011/2012 mpaka 2015/2016 mpango wa kwanza ukilenga kuibua fursa za kiuwekezaji lakini pia kujenga miundombinu ili tuhakikishe kwamba tunajenga msingi mpana wa kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutekeleza huo mpango tukaja na mpango wa pili sasa wa miaka mitano mingine ambayo ni 2016/2017, 2020/2021 ambao ndiyo umekamilika, huu tukasema tujikite kwenye ujenzi wa viwanda, na ndiyo maana Serikali inaripoti mara kwa mara kwamba tumejenga viwanda zaidi ya 8,477 ambako vikubwa ambavyo tunaviona ni 210 kwenye nchi yetu, ambavyo vimetoa ajira za kutosha kwa vijana wetu, lakini kutengeneza mafungamano kati ya sekta ya kilimo na masoko kwa kuwa na viwanda katikati ili tuweze kuchakata bidhaa za wakulima, lakini pia kutengeneza *immediate market* (soko la karibu) la mkulima na kumuhakikishia mkulima soko la mazao yake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia sisi kama nchi tukasema baada ya kupata mafanikio kwenye Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Mipango ya Maendeleo kupitia *Long Term Perspective Plan* sasa twende kwenye Mpango wa Tatu ambao unaishia 2025/2026 na huu mpango umejikita kwenye ku-*consolidate* na kuchukua yote yale ya nyuma, lakini pia

na kuchukua yale ambayo hatukuweza kuyatekeleza au kuyaboresha ili tuweze kwenda mbele. Sasa kwa upande wa uwekezaji kuna mengi ambayo tumeyaona kuna mafanikio makubwa sana ambayo sana tumeyapata kipindi hiki cha miaka iliyopita kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano wa Kwanza na wa Pili.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye Mpango wa Tatu tumelenga kuongeza; moja, utekelezaji wa mipango ya kuboresha mahusiano yetu sisi na sekta binafsi na tutaongea hizi PPDs (*Public Private Sector Dialogue*) kwa kuwasikiliza zaidi wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kuweza kuboresha *complaints handling*; zile kero za wafanyabiashara zile tuwe na masikio mapana zaidi ili tuweze kuzisikia na kuhakikisha kwamba tunatekeleza yale ambayo wafanyabiashara wangetamani, kwa sababu wao ndio wazalishaji na wasambazaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kipindi hiki tunasema *blue print* ambayo imezungumzwa hapa tunaenda kutekeleza kwa uhakika labda niseme hivyo. Tangu mwezi Mei, 2018 baada ya Baraza la Mawaziri kuridhia na pia ndani ya Serikali kuweza kuhamasisha wananchi uwepo wa *blue print* na wafanyabiashara tumeweza kutekeleza mambo mengi ikiwemo kupunguza tozo 273 kwenye eneo letu la kujenga mazingira ya biashara na uchumi. Lakini pia kama mnakumbuka tulikuwa na *TFDA* ambayo ilikuwa inafanyakazi ambazo zinagongana kidogo na *TBS*. Kwa hiyo, Serikali baada ya kupata ushauri kutoka kwa wadau ikiwemo Waheshimiwa Wabunge hapa Serikali ikaamua kuchukua eneo la chakula na vipodozi ikapeleka *TBS* na kuiacha *TFDA* kushughulika na madawa na vifaa tiba ndiyo maana inaitwa *TMDA* kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunatekeleza mipango yetu ambayo tumejiwekea kupitia *blue print*, lakini pia na maboresho mbalimbali ambayo tulianza tangu mwaka 2010 kupitia ofisi

ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaita maboresho, ambayo imetokana na kufuatilia na kutafiti juu ya ripoti ya *IFC* ya Benki ya Dunia ya *Easy of Doing Business*, kuna *indicators* kumi na moja ambazo zinatunyesha hatufanyi vizuri kulinganisha na nchi zingine duniani. Kila nchi inapigana na kukimbia kwahiyoy tutajitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba tunatekeleza hiyo yale maboresho na kuwa na mazingira wezeshi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nipende kusema tui le miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo imelengwa kufanywa na Serikali itafanywa ikiwemo Mradi wa Bagamoyo ambao Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa ameulizia. Serikali iko wazi kwenye hilo kwamba tulichokataa ni yale masharti tu ambayo hayakuwa mazuri sana kwa nchi yetu, lakini kwa kweli wakija tena wale wawekezaji au wakitokea wengine tukakaa chini tukaongea tukaja na masharti ambayo yana *interest* kwa nchi, Serikali haitapinga kwa sababu ule mradi ni wa kwetu Serikali, wala si wa wawekezaji ni wa kwetu sisi. Na kwa kweli hayo maeneo mbalimbali tumeshalipia fidia sehemu ya viwanda, sehemu ya *logistics* lakini pia na sehemu ya bandari tumelipia fidia kabisa yako chini ya mikono ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningependa kuwahakikishia Wabunge na kuwahakikishia wafanyabiashara jumuiya ya wawekezaji kwenye nchi yetu, kwamba Serikali itaongeza usikivu na kuhakikisha kwamba tunafanya kazi pamoja kuweza kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana na naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Wenzetu Wajumbe wa Kamati ya *Public Investment Committee - PIC* ni moja ya Kamati muhimu sana za Bunge hili. Bado tunafikiri hatujaridhika sana na *role* yetu kwenye eneo hilo, sasa ninyi ebu m-*take lead*, muangalie na *best practices* toka kwenye Mabunge jirani na kadhalika namna gani tunaweza tukawa na *role* kubwa

zaidi kwenye maeneo haya ya uwekezaji wa mitaji ya umma ili tuwe na Kamati ambayo ni *more vibrant* namna ambavyo tunaweza tukawa tunapokea nafasi ripoti za *Treasury Registrar*, kama kuna haja ya CAG naye kugusa kitu fulani pale, na namna ya kuimarisha Kamati ile kwa kweli iwe na majukumu ambayo ni bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitaomba muifanyie hiyo kazi kama Kamati halafu mtatupatia mapendekezo ili tuweze kuimarisha maeneo haya.

Waziri wa Mifugo atafuatiwa na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Mpango wetu wa tatu kwenye mipango ya miaka mitano ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sekta yetu ya mifugo na uvuvi ni sekta ya uzalishaji, na Waheshimiwa Wabunge wamejikita sana kuchangia michango mingi inayohusiana na sekta hii ilikuwa inalenga changamoto ambazo zinakabili sekta yetu ya mifugo na uvuvi. Kwahiyo Waheshimiwa Wabunge mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwasababu mmeelezea changamoto ambazo zinakabili sekta ya mifugo na uvuvi ili isiweze kuzalisha sana kama ambavyo inategemewa; lakini pia mmeshauri kwa namna gani sekta hii iendeshe mambo yake ili iweze kuwa na tija kubwa kwa Taifa na iweze kuchangia kwa sehemu kubwa kwenye uzalishaji kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto nyingi zilizoelezewa na Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge kama wanane hivi wamechangia kwenye sekta hii; moja ya changamoto waliyochangia Waheshimiwa Wabunge ni changamoto ya miundombinu hasa inayohusiana na mifugo ndio michango mingi imetoka hapo. Miundombinu inayohusiana na mifugo juu ya afya ya mifugo lakini pia juu ya miundombinu wezeshi ili kufanyabiashara ya

mifugo iwe rahisi. Pia juu ya afya ya wanyama au afya ya mifugo yako masuala ya majosho, yako masuala ya malambo, visima, yako masuala ya kliniki za mifugo ndio hayo ambayo yanakwaza na yametajwa kwa sehemu kubwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kulihakikishia Bunge lako kwamba sisi pia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumewasikia na tutajitahidi kwa kadri itakavyowezekana kwa kadri ambayo tutakuwa tukipata fedha kwa kadri ambavyo tutakuwa tukipata rasilimali fedha kutoka kwa Serikali au kutoka kwa wadau wengine, tutajitahidi sana kumaliza au kupunguza matatizo ya miundombinu kwenye sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya mwaka ujao ambayo Waheshimiwa Wabunge mtatupitishia, tumeweka ujenzi wa majosho, malambo, kliniki na visima ili kuhakikisha kwamba afya ya mifugo yetu inakuwa bora ili mifugo yetu nayo iwe bora kuwezesha kutupa nyama bora na fedha nyingi ukilinganisha na leo. Tuondokane na ule usemi ambao hata Mheshimiwa Rais aliu sema: “Mfugaji anakonda na ng’ombe mwenyewe au mfugo wenyewe nao unakonda”

Mheshimiwa Spika, sasa angalau mwakani tumeweka bajeti ya majosho 129, tutaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kutupitishia. Pia tumeweka bajeti ya malambo na visima kadhaa; tumeweka bajeti ya *clinic* kadhaa, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie ili angalau tuweze kusukuma mbele uzalishaji katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi uweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linakwaza uzalishaji ambao limetajwa na Waheshimiwa Wabunge hasa upande wa uvuvi ni juu ya Sheria yetu ya Uvuvi ya mwaka 2003. Napenda kuliambia Bunge lako sheria hii ya mwaka 2003 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2009, lakini ikatengenezewa pia Kanuni zake mwaka 2009. Mwaka 2020, Kanuni zinazoongoza utekelezaji wa sheria hii zilifanyiwa tena marekebisho. Kwa hiyo, tumeendelea kufanya marekebisho

ya Kanuni zetu ili kuwarahisishia wavuvi waweze kuvua samaki wale ambao wanatakiwa na wale ambao wao pia wavuvi wetu watajipatia fedha au kipato.

Mheshimiwa Spika, lakini tumeendelea pia kufanya mapitio ya Kanuni zetu, mwaka huu tulikutana na baadhi ya Wabunge na nikawaeleza kwamba tunafanya tena mapitio ya hizi Kanuni tujaribu kuona baada ya kuzitumia wavuvi wamesema ni Kanuni ipi ambayo bado inaendelea kukwaza. Kwa hiyo, tunaendelea kupitia tena Kanuni zetu na nimewaagiza *TAFIRI* waanze kufanya utafiti na walishaanza kufanya ili watuletee ni Kanuni zipi ambazo zinakwaza uvuvi kwenye bahari, maziwa na hata sehemu nyingine ili tuzifanyie marekebisho kusudi tu uzalishaji kutoka kwenye sekta ya uvuvi uweze kuongezeka. Niseme tu kwamba marekebisho haya yanaendelea na lengo lake ni kuboresha ili kwamba uzalishaji kwenye sekta ya uvuvi uweze kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati watu wetu wanapita kule na kujaribu kuangalia vipimo au kupima nyavu zetu zinazotumika ili pengine kuangalia ni nyavu zipi zinatumika kwenye uvuvi haramu, kulikuwa na kipimo kinaitwa *match gauge* na kingine ni *vernier caliper*. *Match gauge* ilikuwa inawapunja wavuvi wetu, wavuvi wakalalamika na wakaja Ofisini kwangu tukarekebisha hiyo hali. Sasa tunatumia *vernier caliper* badala ya *match gauge* ili kupima nyavu ipi inafaa kwa ajili ya uvuvi. Kwa hiyo, utagundua malalamiko mengi yanayohusiana na kukamatwakamatwa wavuvi wetu yamepungua sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki. Nilishawataja TAMISEMI, sasa ni Mheshimiwa Umyy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Odo, karibu tafadhali. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa

kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuongea katika Bunge lako la Kumi na Mbili, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema lakini wapiga kura wa Tanga Mjini kwa kunirudisha Bungeni. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kwamba naweza kumsaidia kusimamia na kuratibu shughuli za utawala na maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimpongeze Waziri wa Fedha, ndugu yetu Mheshimiwa Mwigulu kwa kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. Katika hatua hii, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri kwa sababu nimeona Waheshimiwa Wabunge wengi pia wamechangia moja ya vipaumbele vitano vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo ambao ni kuchochea maendeleo ya watu. Katika maoni ya Waheshimiwa Wabunge, niseme kwamba tumepokea na ufafanuzi mkubwa au zaidi tutautoa tarehe 19 - 21 wakati tutakapowasilisha bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu niguse maeneo makubwa matatu au manne. Eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliongelea ni kuboresha miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari. Tunakubaliana na nyie kwamba bado tuna uhaba wa vyumba vya madarasa, madawati, maabara za sayansi pamoja na nyumba za walimu katika Halmashauri zetu, katika Majimbo yetu lakini pia ni lazima tukubali kwamba kazi kubwa na nzuri imefanyika katika kipindi cha mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaeleze tu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika bajeti yetu 2021/2022, tunatarajia kuendeleza ujenzi wa madarasa ikiwemo kukamilisha maboma ya vyumba vya madarasa 2,695. Pia tutajenga maabara za sayansi takribani 1,280. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tumefanya tathmini na hili ni juzi tu, ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia kwamba hataki kuona mtoto wa Kitanzania akisoma chini ya mti akifundishwa katika shule yenye mwalimu mmoja au shule yenye walimu wawili. Kwa hiyo, tumefanya tathmini tuna upungufu wa madawati takribani 1,048,000. Katika bajeti yetu inayokuja tumepanga kununua au kutengeneza madawati 710,000 ili kuweza kutatua changamoto hii ya madawati. Pia tumeona tusiwaache walimu, ni lazima tujenge nyumba za walimu hususani katika maeneo ya pembezoni au maeneo ambayo yapo kidogo mbali na miji mikuu. Kwa hiyo, katika bajeti pia tutajenga nyumba 100 za walimu ili kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira mazuri kwa walimu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba nisema kwamba tukijadili bajeti yetu tutaeleza mambo gani makubwa ambayo tutayafanya katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia watoto wetu. Kubwa ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha tunatoa elimu bora na sio bora elimu kwa watoto wa kitanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa ikiwemo changamoto ya uhamisho wa walimu. Katika hili, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, kila mtumishi wa Halmashauri anataka kwenda kufanya kazi Halmashauri za Mijini, nani atafanya kazi katika Halmashauri za Vijijini au za pembezoni? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu mwalimu au muuguzi au daktari anayo haki ya kuhama kama mtumishi mwingine wa umma, lakini lazima tuangalie kule vijijini na pembezoni nani anaenda kufanya kazi. Kwa hiyo, hili tumelipokea kwamba Waheshimiwa Wabunge wamelitolea maoni, tutahakikisha kwamba tuna-*review case by case* lakini tutatoa mwongozo mahsusi kwa ajili ya ku-*make sure* walimu wanapenda kufanya kazi katika Halmashauri za pembezoni. Kubwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *incentive* kwa walimu na watumishi wa afya ambao wanafanya kazi katika

Halmashauri za pembezoni, kwa hiyo hili tutaliangalia.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni uboreshaji wa huduma za afya ya msingi. Kwenye hili tunapokea maoni na ushauri wa Wabunge kuhusu utolewaji wa huduma. Tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba bado tuna uhaba wa zahanati, vituo vya afya, pamoja na Hospitali za Halmashauri. Sasa hivi tumeamua kushusha badala ya kuwa Hospitali za Wilaya tunaenda kuwa ni Hospitali za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele chetu cha kwanza katika kuboresha huduma za afya ya msingi, tunaangalia utoaji wa huduma katika ngazi ya zahanati, kituo cha afya pamoja na ngazi ya Hospitali ya Halmashauri. Kwa hiyo haya mambo tarehe 19 mtakuja kuyaona katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nafahamu Wabunge wengi wanataka tujenge zahanati na vituo vya afya, tunaona tujikite kwanza kumaliza zahanati na vituo vya afya ambavyo vimejengwa na havijakamilika. Tumeonyesha katika bajeti yetu tuna vituo vya afya 52 ambavyo tunatakiwa kuvikamilisha lakini pia tuna hospitali za Halmashauri 68 ikiwemo kuhakikisha tunaviwekea vifaa tiba na vifaa pamoja na upatikanaji wa dawa na watumishi ili huduma bora za afya ya msingi ziweze kutolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa kuboresha huduma katika ngazi ya msingi *especially* huduma za kinga. Hili tumelipokea, ni kweli tukiweza kuzuia wananchi wengi wakawa wana afya bora kabla hawajaenda katika ngazi ya rufaa maana yake pia tutaokoa fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika suala la afya pia katika bajeti inayokuja Mheshimiwa Rais Samia amenielekeza, haikuwepo kwenye bajeti hii, lakini sasa ametafuta rasilimali fedha, Halmashauri zote 24 ambazo hazina Hospitali za Halmashauri tunaenda kujenga Hospitali za Halmashauri katika Halmashauri hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda umeisha lakini nataka kusema suala la *TARURA* tumelipokea ikiwemo kuongeza bajeti ya *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Umy Ally Mwalimu, Waziri wa TAMISEMI. Wewe ni mdau wetu mkubwa sana Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo tutakuchosha hasa, lakini tunaahidi kukupa ushirikiano wa kila aina kabisa. *(Makofi)*

Sasa ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Leonard Chamuraho, tafadhali.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Mpango huu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama rasmi kuchangia, napenda kushukuru Mwenyezi Mungu kwanza kwa kutuweka hai na kukutana hapa. Pia kumshukuru aliyeniteua Hayati Rais wetu Mtukufu lakini vilevile kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kunibakiza katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia hoja ambazo zimetolewa katika mjadala huu nikianza na Shirika letu la Ndege la Tanzania. Shirika la Ndege la Tanzania mpango wa kulifufua ulipoanza 2016 haukuanza kwa kukurupuka, kwani tulianza na mpango wa mwaka mmoja wa Oktoba 2016 hadi Oktoba 2017 na mpango mkakati uliofuata ambao ulikuwa ni wa miaka mitano ulianza Julai 2017 na utaendelea hadi Juni 2022. Kwa hiyo, tunaendelea vizuri na tija inaanza kuonekana kwani tulipoanza tulikuwa tuna miruko 576 kwa mwaka, lakini sasa tumefika miruko 4,752 kwa mwaka ambapo lengo letu ni kufika miruko 6,500 kwa mwaka lengo ambalo tumekwama kidogo kulifikia kwa sababu ya changamoto ya *COVID* ambayo imezuia ndege zetu kuruka kwenda katika

destinations mpya za China, Afrika Kusini, Nigeria na London. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na hoja ya ufanisi wa ndege zetu, lakini ndege hizi japokuwa tulianza na ndege moja mwaka 2016 na sasa hivi tuna ndege nane hazikuja kwa siku moja, kwa hiyo, kuchukua wastani wa pamoja siyo sawa. Ndege mbili za kwanza tulizipokea Septemba 2016, ndege iliyofuata ilikuwa Aprili 2018, *Boeing* ya kwanza tulipokea Julai 2018 na zile *Air Bus* ya kwanza tulipokea Desemba 2018 na ya pili Januari 2019. *Dreamliner* ya pili tulipokea Oktoba 2019 na *Bombardier* ya mwisho tulipokea Desemba 2019. Kwa hiyo, utaona hizi ndege zinakuja kulingana na mpango na tatu zilizobaki zilikuwa zije mwaka jana lakini zimekwamishwa na *COVID*. Hivyo mipango yetu inakwenda vizuri na miruko hiyo inadhibitiwa kisheria hivyo hatuwezi kuruka kukiuka Sheria za Udhibiti wa Marubani pamoja na Wahudumu wa Ndege. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwa wastani miruko ya *Bombardier* ya kwetu sasa hivi inaruka saa kumi na nusu kwa siku lakini saa ambayo inapendekezwa huwa ni saa nane, kwa hiyo, tumezidisha tunafanya vizuri sana. Kwa *Boeing 787* ambayo ni *Dreamliner* tunaruka sasa hivi saa tatu na nusu inapendekezwa saa 12 na *Air bus* tunaruka saa sita lakini inapendekezwa saa 10. Sasa hizi ndege mbili kubwa tumekwamba tufikisha hiyo miruko kwa sababu safari ya China ambayo ndiyo ilikuwa imepangiwa na ya Uingereza na Afrika Kusini ndio imesababisha changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea vizuri na ufanisi unajidhihirisha wazi kwani ukiangalia umiliki wa soko tulivyoanza mwaka 2016 ulikuwa ni asilimia 4.5 lakini leo tunaongelea umiliki wa soko wa asilimia 75. Hakuna Shirika la Ndege ambalo limeweza kufikia ufanisi huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile vile tukiangalia jinsi ilivyochangia watalii wetu, tulikuwa na watalii milioni 1.2 lakini sasa hivi tuna watalii wanaokaribia milioni mbili. Hawa wote wamesababishwa na hizo ndege zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile ndege zetu zimeweza kutoa huduma kwa Watanzania waliokwama nje ya nchi wakati wa janga la *COVID*. Vilevile zimechangia vizuri katika soko la mazao ya mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja za uendelezaji wa bandari. Uendelezaji wa bandari zetu unaendana pamoja na Mpango wa Taifa wa Uendelezaji wa Bandari yaani *National Port Master Plan* ya mwaka 2020-2040. Ukiangalia kwa sasa hivi bandari yetu ya Dar es Salaam ilikuwa na uwezo wa kubeba tani milioni 11 kwa mwaka lakini baada ya maboresho yatakatayokamilika mwaka 2024 itaweza kuwa na uwezo wa kuhudumia tani milioni 28 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tukiangalia bandari zetu za Mtwara na Tanga; ya Mtwara ilikuwa inaweza kuhudumia tani laki nne kwa mwaka lakini sasa hivi itahudumia tani milioni moja kwa mwaka. Bandari ya Tanga ilikuwa inahudumia tani laki tano kwa mwaka lakini nayo baada ya maboresha tunayofanya sasa hivi itaweza kuhudumia tani milioni moja kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Bandari ya Bagamoyo na ujenzi na uendelezaji wa bandari zote utazingatia mahitaji na ukuaji wa maboresho tunayoendelea kuyafanya sasa katika Bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Endapo atatokea mwekezaji yeyote ambaye ataweza kutusaidia katika kuboresha bandari yoyote kulingana na mahitaji mapya milango ipo wazi na tuko tayari kukabiliana na changamoto hiyo. Katika hoja hii ya bandari, tayari kama Serikali tumeshakutana na hoja hii tunayo kwa Waziri Mkuu ambapo tumeangalia mapendekezo yote na mmetoa mapendekezo mazuri ambayo tutayatumia katika ushirikishaji wa maboresho wa bandari zetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa ni kuhusu Reli ya *TAZARA*, ni kweli kwamba reli hii ilikuwa inasuasua hapo mwanzo. Tayari tuna mkakati mzuri wa

kuihuisha reli hiyo. Tumeshaanza mchakato wa sheria, sheria hii imechukua muda kidogo kuihuisha lakini imebidi iwe hivyo kwa sababu sheria hii inabidi iwe moja ambayo itapitishwa na Bunge lako pamoja na Bunge la Zambia kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, sheria hii tutakapoirekebisha itaruhusu wawekezaji kwani sasa hairuhusu, vilevile itaruhusu upatikanaji wa watumishi kutoka mahali popote kwani sasa hivi tuna hii changamoto ambayo sheria inasema lazima Mtendaji Mkuu atoke Zambia. Kwa hilo, lipo katika mkakati wetu wa kuendeleza hiyo reli mpya ya *TAZARA*. Vilevile tunaendelea na majadiliano na wenzetu wa China pamoja na wawekezaji wengine ili tuweze kuirekebisha hiyo reli yetu ili iweze kuwa na ufanisi zaidi kuliko ambavyo ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo katika mikakati hiyo, tunaungana na aliyetoa kwamba tuongeze matawi ya Tunduma hadi Kasanga Port, kwani upembuzi huo tunaangalia haya yote ili tuiboreshe reli yetu. Vile vile katika *TAZARA* tunafanya tafiti za bei ili kuwa na bei shindani ili iweze kushindana pamoja na taratibu nyingine za usafiri.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchangia kuhusu reli. Tuna reli za aina tatu hapa kwetu. Kwanza nianze na hii reli ya kisasa, *standard gauge* ambayo awamu ya kwanza ni kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na ina vipande vitano. Kipande cha kwanza ni kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, sasa hivi tumefikia asilimia 92; kipande cha pili ni kutoka Morogoro hadi Makutupora, tumefikia hatua ya asilimia 58; kipande cha tano ambacho ni Mwanza hadi Isaka, tumefikia hatua ya *mobilization* na tayari mkandarasi ameshalipwa malipo ya awali tarehe 1 Aprili, mwaka huu 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilizuka hoja ya ujenzi wa reli kwa muda mrefu lakini kwa ujenzi wa awamu ya kwanza imepangwa kukamilika 2025. Hivyo, tunaendelea na kutafuta wawekezaji ambao watatusaidia katika kumalizia kipande

cha tatu na kipande cha nne kutoka Makutupora hadi Tabora na kutoka Tabora hadi Isaka. Awamu ya pili itakuwa ni kutoka Tabora hadi Kigoma pamoja na Mpanda hadi Kaliuwa. Kwa hiyo, sasa hivi tunaendelea na upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina ili itakapokamilika tuweze kupata wawekezaji wa sehemu hizo. Hivyo mtandao wa reli nzima utajengwa kulingana na uwekezaji lakini mradi huo utakuwa ni mchanganyiko pamoja na fedha za ndani, kwenye mikopo, PPP, pamoja na fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, kulikuwa na hoja ya wafanyakazi wa kigeni kuwa wengi kule lakini hili linadhibitiwa kwa mkataba na tunahakikisha kwamba wafanyakazi wa kigeni ni asilimia 20 tu katika ujenzi huu na wazawa wanakuwa asilimia 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, tuna mpango wa reli yetu ya Mtwara hadi Mbambabay na Matai kuelekea Mchuchuma hadi Liganga. Hii imepangwa kujengwa kwa ubia kwa sekta binafsi na Umma. Tayari tulikuwa tuna Mshauri Mwelekezi *KPMG JV* ambaye alitufanyia kazi ambayo hatukuridhika nayo, tayari tumeshamwondo na sasa hivi tunatafuta Mshauri Mwelekezi mwingine ambaye atatupatia mwekezaji mahiri ili tuweze kuendelea na mradi huo kama ambavyo tumekuwa tumepanga.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuongelea masuala ya barabara ambayo tumeendelea na vipaumbele...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Dkt. Leonard Chamuriho.

Waheshimiwa mtakaofuata ni dakika tano tano sasa, kwa sababu ya hali ya muda wetu. Tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa *Angeline Sylvester Mabula*, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO NA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami kuchangia Mpango huu wa Maendeleo ambao ulikuwa unajadiliwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika suala zima la Wizara ya Ardhi kwenye Mpango; ni Wabunge watatu ambao wamechangia. Ninachotaka tu kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba Wizara, inatambua wazi ya kwamba ardhi ni mali, ardhi ni mtaji, ukiitunza itakutunza.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala zima la Mpango wa Maendeleo ambapo pia tunasema Tanzania inakwenda kwenye Sekta ya Viwanda na zaidi, tuko tayari; na ukiangalia kwenye ule Mpango kipengele cha 5.4.23 tumeainisha yale yote tunayokwenda kufanya.

Mheshimiwa Spika, tumeweka kipaumbele zaidi katika kupanga, kupima na kumilikisha, kwa sababu usipoipanga ardhi vizuri, utakuwa umekwamisha sekta nyingine zote katika suala zima la kimaendeleo, nasi tunatambua kwamba ardhi inahitaji kupangwa, kupimwa na kumilikishwa. Ni wazi mpaka sasa hivi hatujafikia asilimia kubwa, ni kama alimia 25 tu. Waheshimiwa Wabunge wameongelea hapa kwamba, ikiweza kupangwa vizuri na ikapangiwa matumizi, ni wazi inaweza ikakusanya kodi nyingi za kutosha. Ni kweli hatukatai hilo, lakini kama Wizara ndiyo maana mnaona kwamba Ofisi za kimikoa zilifunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge amependekeza suala la *agency*, ni wazo zuri, lakini kama tutatumia vizuri ofisi zile za Mikoa na Halmashauri ambazo ndiyo Mamlaka za Upangaji Miji zikaweza kukijikita katika kuweka mpango mzuri kama ambavyo upo kwenye suala zima la kutenga bajeti za

kupima maeneo yao, hatutahitaji suala *agency* kwa sababu kila Halmashauri inao wataalam. Kila Halmashauri ikiweka kipaumbele, itaweza. Kama Wizara, katika siku za nyuma tumetoa baadhi ya pesa katika Halmashauri na wamefanya vizuri katika upangaji.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia suala la Mbeya, Kahama, Bariadi na Ilemela, walipewa fedha na wamefanya kazi hiyo nzuri. Kwa hiyo, tuna Imani, mbali na bajeti zinazokuwa zimewekwa na Halmashauri zenyewe, lakini wakiwezesha kidogo na Wizara, tunawasukuma kuweza kufanya kazi yao vizuri. Kwa hiyo, kama Wizara, tunalionga hilo na tunalizingatia.

Mjheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo limeongelewa kuhusu kuwa na Sera ya Nyumba pamoja na Sera ya Makazi. Kama Wizara, tuko katika mchakato na tutaleta nakala kwa Wabunge ili muweze kuongeza *input*, kwa sababu tayari ile rasimu ya mwanzo imeandaliwa ambayo tunahitaji sasa tupate *input* za Waheshimiwa Wabunge kwa undani zaidi ili tuweze kutoka na *final product* itakayoweza kukidhi mahitaji na tutaondokana na haya malalamiko ambayo mara nyingi yanatokea.

Mheshimiwa Spika hata ile ya *Real Estate Regulatory Authority* nayo pia iko kwenye mchakato mzuri. Tumekuwa na madalali wengi hapa katikati na unakuta watu wengi wanadhulumiwa ardhi. Unaambiwa kuna ardhi ya uwekezaji hapa, lakini anayekwambia ni *Middlemen* mwisho wa siku unajikuta huwezi tena kupata ile ardhi. Kwa hiyo, sheria hiyo nayo iko ambayo, inaandaliwa kwa maana ya kwamba tutajikuta tumetoka katika suala zima la matapeli ambao wanakuwepo.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la uwekezaji kwenye maeneo ya viwanda ambayo hasa ndiyo tunafikiria kupeleka nguvu kule, tumetenga zaidi ya ekari 12,400 ambazo ziko tayari zinasubiri wawekezaji wakati wowote wakizihitaji. Kama Wizara pia, bado tunaendelea kupitia yale mashamba ambayo yameshindikana katika kuendelezwa ili tuweze

kuyachukua na kuyatenga kwa ajili ya kazi hizo kubwa ambazo tunazitegemea kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa vyovyote vile, ukiweka mpango mzuri kwenye matumizi ya ardhi, ukiweka mpango mzuri katika suala zima la kupanga, kupima na kumilikisha, hizi sekta nyingine zote zitakuwa katika hali nzuri katika utendaji. Nasi kama Wizara tunasema, Serikali ilishaelekeza nini cha kufanya, kwa hiyo, Wizara tumejipanga kuhakikisha kila mpango ambao unapangwa, uwe unawiana na Wizara nyingine katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hata haya ambayo yanaongelewa katika suala la kuwezesha kwenye maeneo ya huduma, bila kuwa na mpango mzuri na bila kufanya maandalizi, hatuwezi kufika huko. Kwa hiyo, niseme tu kwamba sisi kama Wizara, tuko tayari kuhakikisha kwamba mpango huu unatekelezeka kwa kuwa unakutekeleza yale ambayo tumeyaweka kama kipaumbele katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya.

Mheshimiwa Spika, pia katika upangaji wa miji yetu, kwa sababu usipoipanga miji pia, napo itakuwa ni shida. Kama Wizara, tayari tumeshaandaa mwongozo ambao sasa kuna mbunge alielekeza kwamba tunaweza pia tukadai kodi katika maeneo ambayo hayajapimwa. Kisheria huwezi kudai katika maeneo hayo, lakini tunaweka mpango mzuri ambao *draft* yake iko tayari ili zile Halmashauri katika ile miji inayokua kwa kasi, tuwape mwongozo wa namna ya kuwekeza, namna ya kupanga miji yao ili iweze kuwa na maeneo ya huduma, maeneo ya uwekezaji na maeneo ya makazi ili kila mji utakapokuwa unakua ukitangaza kama ni eneo la huduma, liwe limepangwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi. Sasa ni Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Waziri wa Afya, karibu sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu wa dakika hizi chache kuhusu wasilisho hili wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini niendeleo kuhudumu kwenye Sekta hii ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya ni sekta ya huduma za jamii na mpango huu hauwezi ukatekelezeka kwa ufanisi mkubwa kama Taifa hili litakuwa na afya isiyo njema. Kwa hiyo, Sekta ya Afya tunatambua kwamba lazima tujikite kwenye masuala mazima ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukizwa na pale inapotokea watu wameumwa, waweze kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala huu kwenye Bunge hili ukiangalia umepambwa na imani kubwa kabisa inayotutaka Sekta ya Afya tusimamie Bima ya Afya kwa wote. Natambua kazi kubwa iliyofanywa ya mchakato huu wa kuelekea kwenye Bima ya Afya kwa wote, nami nimeipokea, tuko kwenye hatua za mwisho kabisa za kuleta Muswada wa Sheria. Awali tulidhani ni Septemba, lakini tumeona hapana, hapa tulipo tumeongeza kasi mpaka salamu mle imebadilika. Tukiingia, "Bima ya Afya kwa Wote! Kazi iendele!" Ndiyo badala ya habari ya asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo ni kwamba, tupate ridhaa ya vyombo vyote vya Serikali kwenye hatua hii iliyofikia ya kuandaa rasimu wa Muswada wa Sheria ili Juni kwenye Bunge lako Tukufu tuje na huo Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepata michango mingine mbalimbali, huu *specifically* ulikuwa umechangiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege, Mbunge. Kwa hiyo, hili ndilo wasilisho letu kwenye hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, yeye alichangia kusema kwamba katika maendeleo haya, hawa wa *Biomedical Engineers* wanajifunza kwa vitendo ile *internship* yao kwa kulipa pesa, hatuwezi kuharakisha maendeleo ya matengenezo ya vitaa tiba vya kisasa tunavyovipata. Akaomba kwamba tuwapunguzie malipo. Nasi sekta yetu imefuta hayo malipo waliyokuwa wanalipa huko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala lingine lililochangiwa na Mheshimiwa Kandege kuhusu hatima ya maendeleo ya upatikanaji wa vifaa tiba nchini. Nitambue kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, kwamba mwaka 2018 mpaka 2020, shilingi bilioni 64 zimenunua vifaa tiba mbalimbali katika hospitali za kipigwa na katika Hospitali za Afya ya Msingi na bado zoezi hili linaendelea. Katika ngazi ya hospitali za kipigwa, tumeweza kutumia vifaa hivi vya kisasa kabisa kama *LINAC* na *CT Simulators* na vifaa vingine vingi, hadi tukapunguza rufaa za wagonjwa kwenda nje ya nchi kutoka 164 kwa mwaka 2015/2016 mpaka wawili mwaka 1920/2020. Kwa hiyo, mwaka huu sasa tutawasilisha bajeti ya shilingi bilioni 229 ili kuendeleza kupata vifaa tiba hivi kuanzia ngazi zote za kibingwa mpaka huko chini. Tunaomba Bunge lako Tukufu lipitishie. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la watumishi. Watumishi bado ni changamoto na hapa tutawasilisha bajeti ya shilingi bilioni 144.9 tukiomba Bunge lako lipitishie ili tuweze kusogeza upatikanaji wa watumishi kwenye vituo mbalimbali vikiwepo hivi 487 vilivyojengwa kwenye ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja iliyochangiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq ya kuhusu namna gani tutaweza kuwafuatilia akina mama wajawazito waweze kujulikana wanapopata huduma ya Afya ya uzazi kuanzia kipindi cha mimba, wakati wa kujifungua na baada.

Mheshimiwa Spika, kwanza tumejenga hivi vituo kama nilivyovitaja hapo ambapo huduma zimesongezwa karibu yao na hospitali 102 za Halmashauri zimejengwa. Hapa

tumemsikia Waziri, pacha wangu, Mheshimiwa Ummu Mwalimu Waziri wa nchi, TAMISEMI akisema kwamba amepewa maelekezo na Mheshimiwa Rais kuendelea kujenga hizo hospitali katika Halmashauri zilizobaki ambazo hazikujengewa. Yote hii ni mikakati ya kusogeza huduma za mama mjamzito ili aweze kuwa na ujauzito salama hadi kujifungua.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tumebuni kitu kingine ambacho ni kanzidata, kwamba anaporipoti tu kliniki, ule wakati aliporipoti anaingizwa kwenye *database*, anafuatiliwa ili hata kama akipotea, tujue amepotelea wapi? Utekelezaji huu umeshaanza kutekelezwa Arusha, ambapo huko ndiko ameteuliwa Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt. Sichwale na tunaupoleka nchi nzima. Kwa hiyo, itakuwa ikishaingizwa pale, akipotea tu, mpaka VEO atuambie alipopotelea huyu mama, yuko wapi?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa michango yote. Naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Waziri wa Afya. Sasa tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao kwenye Sekta ya Viwanda na Biashara ambayo kwa kweli ilikuwa mingi na imekuwa hivyo kwa sababu Mpango wenyewe kwa kweli ukiangalia malengo 12 ya Mpango wa Maendeleo ambao tumeujadili hapa, malengo sita yanahusu Sekta ya Viwanda na Biashara. Mule ndani kuna hatua 116 za kiutekelezaji. Zaidi ya theluthi moja tu, 54 zinahusu Sekta ya Viwanda na Biashara. Kwa hiyo, naelewa kwa nini michango imekuwa mingi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu ya muda, naomba nichangie tu jambo kubwa ambalo limejitokeza,

ambalo nawe umelisisitiza; na nipanue pale Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji alipoishia kuhusu suala la utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhidi wa Biashara, maarufu kama *Blueprint*, ambao unalenga kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, kwenye mpango huo kuliibuliwa changamoto nyingi ambazo zinakwamisha mazingira ya biashara na uwekezaji, lakini unaweza kuzigawa changamoto hizo katika maeneo 11 ambayo tunayafanyia kazi. Ningetaka kuleta taarifa kwenye baadhi ya maeneo ili kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nataka nitolee taarifa maeneo manne ambayo ni ya msingi sana. Moja sitalizungumza kwa sababu Mheshimiwa Mwambe ameshalieleza kuhusu suala la tozo, ada na adhabu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, kwenye mpango huu iliainishwa kwamba tozo 45 ziliainishwa kama ni tozo za kero; na ziondoke; na zilifutwa. Ukiacha hiyo, tulienda mbali zaidi, zimefutwa jumla ya tozo 273 kama ambavyo Mheshimiwa Mwambe ameeleza. Kwa hiyo, ni hatua kubwa na hii ilikuwa ni moja ya kero kubwa sana ambayo iliainishwa kwenye changamoto za kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ilikuwa eneo la utungaji wa sheria na uboreshaji wa sheria na kanuni mbalimbali. Hapa zilitambuliwa sheria na kanuni 90 ambazo zinakwamisha mazingira ya biashara na uwekezaji. Tayari sheria na kanuni 11 zimefanyiwa kazi, pia tumeweka misingi 10 ya kuzingatia katika kuboresha sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, baadaye ilikuja kuonekana kwamba kuna haja ya kuwa na sheria moja ambayo ni kubwa, inayozungumzia biashara. Kwa hiyo, tuko katika mchakato ndani ya Serikali kuja na Muswada wa sheria ambao kwa sasa unaitwa *Business Facilitation Act* ambao

utajibu changamoto nyingi za Sheria ambazo ziliainishwa hapa.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu lilikuwa ni kuweka mfumo wa *electronic*. Hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wanafahamu kwamba, ndani ya Serikali mifumo mingi ya *electronic* imeanzishwa kutokana na utekelezaji wa mipango hii ikiwemo *GePG, BRELA, TBS, TIC, TMDA*, kokote kule kwa sasa wanatumia mifumo. Wengi wanafahamu ukitaka sasa hivi kusajili Kampuni, huhitaji kwenda *physically* kwenye ofisi, una *log in* tu kwenye mfumo.

Mheshimiwa Spika, ya nne na hii ni kubwa ni suala la uanzishwaji wa vituo vya pamoja vya kutoa huduma. Vimeanzishwa ndani ya *TIC, EPZA* na mipakani. Nitoe taarifa pia hapa kwamba hatua inayofuata ni kuanzisha vituo vya kutolea huduma, yaani *One Stop Service Delivery Center* kwenye ngazi ya Halmashauri. Bahati nzuri tayari tumepata *grant* kutoka Umoja wa Ulaya *Euro* million 9.5. Hizi zinakwenda kujenga vituo vya *One Stop Center* kwenye ngazi za Halmashauri ili sasa kuja kwenye Halmashauri, badala ya mtu kwenda *TRA, BRELLA* na *TBS*, anaenda sehemu moja, anapata huduma zote kwa wakati mmoja. Tunaamini hili litakuwa ni mkombozi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka tu niseme kwamba utekelezaji wa *Blueprint* unaendelea vizuri, tutakachofanya ni kuimarisha utoaji wa taarifa, nasi ambao tumeteuliwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni, tutaongeza kasi zaidi ili kuona kwamba, utekelezaji unakwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe taarifa, ilitolewa hoja hapa kwamba viwanda vyetu vya mafuta vinavyo tu *single refinery*. Hii siyo kweli. Ninayo orodha hapa ya zaidi ya viwanda 20 ambavyo finafanya *double refinery*. Nami nataka kushauri Waheshimiwa Wabunge, Wazungu wanasema, *extra ordinary claim, demands extra ordinary evidence*.

Mheshimiwa Spika, sasa ukitoa hapa *claim* ambazo ni kubwa, kwa sababu inataka kuonekana kana kwamba

Tanzania mafuta ambayo tunatumia kule hayana ubora unaostahili, hapana. Mafuta yetu inajulikana kwa vipimo vyote kwamba ni mafuta bora sana ambayo tunazalisha hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kulitolea maelezo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni miradi ya kielelezo ambayo imetajwa hapa Mradi wa Chuma cha Linganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma. Nataka tu niseme mradi huu ni miongoni mwa miradi 17 ambayo ipo katika miradi ya kielelezo na kwa kweli ambacho kilichochelewesha na nilitolea taarifa mwezi Februari ni kwamba tutaleta taarifa kamili katika Mpango...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: ...na katika bajeti ambayo tutakuja nayo mwezi Mei.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo. Nisisitize jambo moja tu kwako, kwenye Bunge la Kumi na Moja, miaka yote mitano tulishughulika sana na suala Bima ya Afya na haikuja na tulipokuwa tunamaliza tulisema tumebakiza viporo viwili; cha Bima ya Afya na kiporo cha pili ni cha *Business Facilitation Act*. Ilishindikana miaka mitano havikuja, kwa hiyo mzee Mheshimiwa, tunaanza na wewe hapa. Itakuwa vizuri kama itasomwa mara ya kwanza mwezi wa Juni, lakini mwaka huu usipite bila hicho kitu kuja, kwa sababu ni malalamiko ya wengi.

Bahati nzuri Rais, Mheshimiwa Samia ameanza na hilo katika zile hoja zake, la kwanza, aliloanza nalo ni hilo. Ili hili

litekelezeke lazima hii *Business Facilitation Act* ije hapa, kwa hiyo *this time* kwa kweli Mheshimiwa Rais katuelekeza na sisi Bunge tunakuja kisawasawa, kwamba hicho kitu kije.

Kilimo, Profesa Adolf Faustine Mkenda, tafadhali.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja na kwa vile ni mara yangu ya kwanza kabisa kuzungumza kwenye Bunge lako Tukufu, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Chama Cha Mapinduzi na wapiga kura wa Jimbo la Rombo wa kuniwezesha kuwa Mbunge kwenye Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameniamini kwa kunifanya kuwa Waziri wa Kilimo. Shukrani pekee ninazoweza kumpelekea ni kwamba, nitafanya kazi wa bidii, maarifa na juhudi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepitia kwenye simanzi kubwa sana kwa kuondokewa na Mheshimiwa aliyekuwa Rais wetu, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, lakini tunamshukuru Mungu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametusimamia vizuri, tumeendelea na msiba vizuri ametufariji na kuleta matumaini makubwa sana kwenye nchi yetu. Tunamshukuru sana, tuendeleo kumuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kilimo kimezungumzwa sana katika mjadala wa Waheshimiwa Wabunge na masuala yaliyozungumzwa ambayo sitaweza kuyazungumzia yote, mengi tutayaona kwenye majibu ya bajeti yetu, ni umwagiliaji, zaidi ya Waheshimwa Wabunge 10; suala la mafuta ya kula, zaidi ya Waheshimiwa Wabunge saba; pembejeo za kilimo, Waheshimiwa Wabunge 12; huduma za ugani, Waheshimiwa Wabunge watano; utafiti, Waheshimiwa Wabunge wanne; masoko, Waheshimiwa Wabunge watano; sera kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge tisa, mazao na ushirika Waheshimiwa Wabunge 10.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia, sehemu kubwa wa yale yaliyozungumzwa ukiyatafrisiri yanazungumza kwenye umuhimu wa kuongeza tija kwenye kilimo. Yaani kuongeza kiasi cha mazao ambacho tunaweza kukipata kwa heka moja au kile ambacho tunaweza kukipata kwa juhudi ambazo tunazitoa. Kwa kweli hiyo inaendana sana na maudhui ya Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao moja ya *term, flagship statement* yake ni kujenga uchumi shindani. Hatuwezi kushindana kwenye mazao endapo gharama ya uzalishaji itakuwa kubwa sana, lakini kwa heka moja tunazalisha kidogo

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye mafuta ya kula kwa mfano changamoto yake, ni kwamba sisi gharama ya kuzalisha mazao yanayoweza kutuletea mafuta ni kubwa sana. Mchikichi kwa mfano, kwenye hekta moja sisi tunaweza tukapata mafuta tani 1.6, lakini wenzetu tunakochukua mafuta sasa hivi hayo Mawese Malaysia, Indonesia na kadhalika, wanapata tani 10 kwa hekta na hili ni suala la tija.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake ukiangalia kwa sababu siwezi kuingia kwa *detail* sana, ukiangalia pato la Taifa letu lote, utaona kwamba kilimo kinachangia takribani theluthi moja tu ya pato la Taifa, lakini nguvu kazi inayoenda kwenye kilimo ni zaidi ya theluthi mbili ya nguvu kazi yote hapa nchini. Maana yake ni kwamba, juhudi zinazozafanywa na mkulima, zinaleta kipato kidogo sana katika nchi yetu tija ipo chini sana na hatuwezi kuingia kwenye ushindani bila kutatua tatizo hili. Kwa hiyo, changamoto kubwa kabisa ya kilimo ni kuhakikisha kwamba gharama ya uzalishaji zinashuka, maana yake ni kwamba na bei ya mazao ishuke, lakini kipato cha mkulima kiongezeke. Hiyo inawezekana tu endapo tunaweza kuzalisha zaidi kwa hekta moja na gharama zikishuka zitatusaidia kujenga viwanda na kuleta ushindani kwenye uzalishaji wa mafuta ya kula na kwenye kuuza kwa nchi za jirani ambazo tunashughulika nazo.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachukua maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameyatoa hapa ambayo ni mengi sana na tumeya-*summarize*. Mengine

mazuri sana, tutayafanyia kazi, lakini niwape matumaini Waheshimiwa Wabunge baadhi ya vitu ambavyo tayari viko kwenye mchakato na tunaomba tutakapokuja hapa na hotuba ya bajeti na maombi ya fedha mtupitishie kwanza.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la utafiti. Tunaongeza fedha kwenye utafiti wa kilimo, kwa sababu bila utafiti hatuwezi kupata mbegu bora na hatuwezi kuwa na kilimo bora katika mazingira yetu. Kwa hilo moja tunaongeza na wataona na tunafanya hivyo kwa kuanzisha Mfuko wa Utafiti ambao tutaulezea hapa na vile ambavyo tutafanya.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti tutalenga sana vitu viwili; kwanza mbegu, kupata mbegu bora zinazokidhi mahitaji ya nchi yetu; na pili kilimo bora katika mazingira yetu. Katika suala la mbegu, tutajitahidi sasa kuzalisha mbegu nyingi kwa sababu kilimo cha mbegu hata humu ndani ya Bunge lako Tukufu tumekisikia sana. Tunafanyaje? Mashamba yote ya ASA yaliyopo hapa tunayatengea fedha kwa ajili ya kufanya kilimo cha mbegu cha umwagiliaji ili tuhakikishe kwamba tutakuwa tunazalisha mbegu sio kwa kutegemea msimu wa kilimo, kwamba tunaendana na wakulima tunazalisha mbegu wakati tunazalisha chakula halafu zile mbegu tunasubiri mpaka mwaka ujao, lakini tuweze kuzalisha mbegu kwa mwaka mzima na kuzalisha mbegu za kutosha na hizo mbegu ziwe ni matokeo ya utafiti ambao utakuwa unafanywa na taasisi yetu ya utafiti kwa fedha ambazo tutaziongeza kama Waheshimiwa Wabunge watakavyosikia katika bajeti. Hilo tutalifanya pamoja na mambo mengine ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine hata tukifanya utafiti, hasa upande wa *agronomy*, kilimo bora tunahitaji kufikisha matokeo ya utafiti kwa mkulima. Kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyozungumza ni muhimu sana kuimarisha shughuli za ugani hapa nchini, tuna kazi kubwa sana, kwa sababu namna fulani tumerudi nyuma katika eneo hilo. Maafisa Ugani wengi hawana usafiri, wanahitaji kutoa huduma kwa wakulima na namna ya kufuatilia utendaji wao

haujawa mzuri sana, kwa hiyo tunafanya nini? Kwanza, tutanunua, tutakapoomba fedha hapa tunaomba mtukubalie, pikipiki 1500 kwa kuanzia, kwa ajili ya kuwagawia Maafisa Ugani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatenga mikoa mitatu ya kielelezo ya namna ya kufanya huduma za ugani kwa namna ambayo inaleta tija. Mikoa hiyo tunahitaja wakati tutakapo wasilisha hapo Bungeni. Tunaongeza juhudi za ufuatiliaji, kwa sasa hivi tuna kitu tayari kinachoitwa *mobile* kilimo. Kila Afisa Ugani ambaye tumemuunganisha naye anakuwa na simu anapomtembelea mkulima, anatoa taarifa na anatuwekea namba ya mkulima. Kwa hiyo tunaweza tukakaa ofisini hapa au kwenye halmashauri unampigia mkulima kumuuliza Afisa Ugani alivyokuja kulikuwa na shughuli gani na amekushauri nini.

Mheshimwa Spika, kwa hiyo tutalifuatilia hilo, tutaongeza sana hasa kwa hiyo mikoa mitatu ambayo tutaitaja siku hiyo kuhakikisha kwamba kweli tunafuatilia shughuli za ugani zinakwenda vizuri. Tutafufua na kuimarisha zile *farmers' fields schools*, mashamba ya mfano, lakini kila Afisa Ugani hasa kwenye hii mikoa mitatu tutahakikisha na yeye ana shamba na tutamhudumia, tutamwezesha. Wakati tunamkagua utendaji wake tutaenda kuangalia na shamba lake likoje. Wakati kuna shamba la kielelezo katika eneo lake, tunataka kuhakikisha kwamba na yeye analima, anatuonesha anajua kitu ambacho anataka kwenda kuwashauri wakulima.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni pamoja na kuongeza huduma za kupima udongo kama zilivyosema hapa, kwa sababu matumizi ya pembejeo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, yapo mengi ya kusema, lakini kwa sababu ya muda, nashukuru sana na

kama nilivyosema naunga mkono hoja. Tunaomba tukija kuomba fedha Bungeni zipitishwe. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Profesa Adolf Faustine Mkenda kwa maneno haya ya kutia moyo sana sana hasa kwa upande wa watendaji wa kilimo. Nilikuwa nawauliza mahali fulani kwa nini ninyi mko hivi mlivyo, wakaniambia Mheshimiwa sisi ni Maafisa Kilimo, sisi sio wakulima, lakini sasa mtawafanya nao washiriki kwenye kilimo, litakuwa ni jambo jema. Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Medard Matogolo Kalemuni, tumalizie *session* hiyo.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mada hii muhimu ya Mpango uliopo mbele yetu. Kwanza napenda nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa kutuletea Mpango huu mzuri sana. Wapo wachangiaji takriban 10 waliochangia eneo hili, lakini kwa sababu ya muda, nitaeleza kwa ufupi maeneo machache sana.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla tumeamua kujenga uchumi wa viwanda. Ili tuelekee kwenye uchumi wa viwanda, jambo muhimu sana ni kuwa na umeme wa kutosha, unaotabirika na wa gharama nafuu. Nimeanza na jambo hili tuone ili tunapoelekea tuko namna gani. Nianze na suala la kuzalisha umeme mchanganyiko ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza kwa kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyoko mbele yetu hapa tunaweka kipaumbele gani. Mpango wa Serikali yetu ni kuzalisha umeme mchanganyiko na ndio mpango tulionao kwa kutumia vyanzo vyote tulivyonavyo ili kujiridhisha tunapata umeme wa kutosha, unaotabirika, wa uhakika na wa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuzalisha umeme hapa nchi toka mwaka 1964 katika mtambo uliopo Hale-Tanga wa

megawatts 21.5. Tukaja Mradi wa Nyumba ya Mungu, nao bahati nzuri upo Tanga, maporomoko ya maji wa *megawatts* nane; baadaye tukaja Mtera karibu na hapa Dodoma, *megawatts* 80 mwaka 1980. Kwa hiyo, toka miaka hiyo, toka ukoloni mpaka mwaka wa 2000 tulikuwa tunatumia umeme wa maji. Baadaye miaka ya 2000 tulianza kutumia umeme wa rasilimali ya gesi asilia. Hapo kwa umeme tulionao hapa nchi ambao ni zaidi ya *megawatts* zaidi ya 1,601 asilimia 62 ya umeme tulionao kwa sasa unatokana na rasilimali ya gesi. Kwa hiyo tunaitumia gesi kwa sasa kwa kiasi kikubwa kuzalisha umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hoja ya kwamba pengine hatufuati sana vyanzo vingine haipo. Tunazingatia vyanzo vyote kuzalisha umeme ilimradi uwe umeme wa uhakika, unaotabirika na wa gharama nafuu. Kwenye rekodi tulizonazo umeme wa gharama nafuu kabisa kuliko vyote ni wa rasilimali ya maji. Ili uzalishe *megawatts* moja ya umeme wa maji unahitaji Shilingi 36 tu basi, fedha ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umeme wa pili unaofuata kwa gharama nafuu, ni umeme wa nyuklia Shilingi 65 peke yake unapata *unit* moja ya umeme. Unaofuata kwa bei ya chini ni umeme wa *solar* pamoja na upepo unaohitaji Shilingi 103 kuzalisha *unit* moja. Umeme unaofuata kwa bei ya chini naomba mnifuatilie vizuri unafuata pia umeme makaa ya mawe ambao ni Shilingi 118 kwa *unit*. Umeme unaofuata ni umeme wa joto ardhi ni Shilingi 119 hadi 120. Umeme unafuata ni Shilingi 147, umeme wa rasilimali ya gesi Shilingi 147 kwa *unit*; na umeme wa mwisho ni wa mafuta mazito Shilingi 546 kwa *unit*. Nimalizie kusema, lazima mwisho wa siku umlegezee mzigo mwananchi wa kawaida na huu ni umeme wa maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nilipongeze Bunge lako Tukufu, mwaka jana, mwaka juzi na mwaka huu kwa kukubali kutekeleza Mradi mkubwa wa Julius Nyerere utakaozalisha *megawatts* 2,115. Hata hivyo, haina maana kwamba hatuzalishi miradi mingine, tunaendelea kuzalisha umeme wa

gesi na hivi sasa tuna mpango wa kuzalisha *megawatts* 300 kule Mtwara; *megawatts* 330 kule Somanga Fungu na tunaendelea kuzalisha *megawatts* 185 Kinyerezi *one extension* na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, kwa Mradi huu wa Julius Nyerere ambao utatupa *megawatts* 2,115 ambao kama nilivyoeleza gharama yake ya kuujenga ni nafuu kuliko miradi mingine, maana yake tunakwenda kupunguza gharama ya umeme kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze jambo moja; kwanza napenda nitoe taarifa, mradi unaendelea vizuri na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alitembelea, nisingependa kumsema lakini aliona mradi unakwenda vizuri na sisi tutaendelea kutembelea hadi ukamilike.

Mheshimiwa Spika, China ambayo ndio anaongoza kuwa na mradi wa kuzalisha umeme duniani, kuna mradi mkubwa wa maji unaozalisha *megawatts* 22,160, mradi mmoja. Kwa hiyo naomba nisisitize kwamba pamoja na mambo mengine, pamoja na kuzingatia umeme mchanganyiko, lakini pia twende kwa vipaumbele vinavyolenga kweli kujenga uchumi wa viwanda wenye gharama nafuu. Bado narudia, tunatumia vyanzo vyote ndio maana nimesema kwamba rasilimali ya gesi tutaendelea kuzalisha miradi mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo matumizi mengine mazuri sana kwa miradi ya gesi pamoja na kuzalisha umeme katika mradi wa gesi, gesi pia inaweza ikatumika kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vingine; kutengeneza mbolea, kujenga viwanda vya Ngozi, viwanda vya vyuma na kadhalika. Kwa hiyo matumizi ya rasilimali ya gesi bado yapo palepale. Sio rasilimali ya gesi tu nimetaja vyanzo vingine ndio maana tunakwenda kuzalisha umeme wa upepo na jua na uko mpango wa kukamilisha mradi huo mwakani Julai utakaozalisha *megawatts* 1,100 kwa hiyo vyanzo vingine tutaendelea kuvitumia. Langu la msingi hapo kutoa taarifa hii Bungeni, nitaeleza kwenye mpango na bajeti yetu muda

utakapofika, lakini leo nimeona niliweke jambo hili sawa ili Watanzania tujue tunakoelekea.

Mheshimiwa Spika, katika miradi hii ambayo nimeitaja hapa, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, vyanzo vyote ambavyo viko kwenye mpango wetu vinatumika kuzalisha umeme kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, tutakapozalisha mradi huu wa Julius Nyerere tutakuwa na takribani *megawatts* 4,887 hapo mwakani mwezi Juni. Kwa hiyo umeme utakaobaki mahitaji yetu, mwakani tutahitaji umeme takribani *megawatts* 2,001. Kwa hiyo umeme utakaobaki takribani 2,102 tutaweza kuwauzia majirani zetu pia na kuingiza fedha nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe taarifa, kwa sababu mradi huu na naomba nisali mbele yako, mradi huu ukamilike na nina uhakika utakamilika. Tarehe 15 Novemba, 2021, kabla ya saa kumi na mbili jioni tunaanza kujaza maji kwenye bwawa letu ili tuanze kupata umeme wa kutosha. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nilieleze vile jambo hili.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Spika hajakusikia bado umesemaje?

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, Tarehe 15 Novemba, 2021, kabla ya saa kumi na mbili jioni tunaanza kujaza maji kwenye bwawa letu, kuelekea kwenye kupata umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwenye suala hilo. Naomba niishukuru sana Serikali, hadi sasa katika mradi huo tumeshalipa trilioni 2.04, ambayo ni sawa na asilimia mia moja ya mahitaji ya malipo yanayotakiwa kulipwa kwa Mkandarasi. Naipongeza Serikali kwa sababu hatujachelewa kulipa na tunayo matumaini tutaendelea kumlipa fedha ipo na mradi utakamilika kwa wakati. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la matumizi ya gesi Mtwara, jambo ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli napenda kwa hekima ya pekee niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara na Lindi kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rasilimali ya gesi tuliyonayo kwa sasa tunazaidi ya trilioni 57.54 na maeneo makubwa sana tunayotumia ni kwenye kuzalisha umeme lakini tumeanza kutumia pia kwa matumizi ya nyumbani. Kwa Mtwara peke yake, kama nilivyowapongeza Waheshimiwa Wabunge, Mtwara tuna mitambo 13 ya kuzalisha umeme wa gesi. Na umeme wa gesi kwa Mtwara ambao ni megawati 30.45 wakati mahitaji yao ni megawati 15, tunayo ziada ya umeme kwa Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara na Lindi kwasababu wametuhamasisha sana kwamba umeme wa gesi unatumika. Lakini gesi hii inatumika kwa sababu suala la msingi ni hii gesi inatumikaje kwa Mtwara. Tumeanza kutumia gesi, na mpaka sasa tumetumia trilioni 0.053 kwa ajili ya kuwasambazia gesi nyumbani wnanachi wa Mtwara na maeneo ya Lindi.

SPIKA: Ahsante sana.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwamba tutaendelea kutenga gesi kwa ajili ya kutumia nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kwasababu ya muda, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, umetupa moyo sana, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Sasa tunakuja kwa watoa hoja, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Eng. Hamad Masauni Yussuf, naomba utumie kama dakika saba hivi, lakini uje hapo mbele; karibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya, lakini nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu kwa kunichagua kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite katika hoja kama mbili ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumzia katika Bunge lako Tukufu kwenye mchango wa mjadala wa Mpango.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ninataka kulizungumzia ni kuhusu maoni ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu jinsi gani ambavyo kasi ya ukuaji wa uchumi wetu haiakisi hali halisi ya maisha ya wnanachi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa utangulizi kwa kunukuu *equation* moja ya uchumi ambayo inasema $Y=C+I+G+X-M$. Ukiangalia *equation* hii inaweza ikatoa tafsiri nyingi lakini kwa haraka haraka na kwa sababu ya muda nimezichukua kama tafsiri tatu. Ta kwanza inaonesha kwamba kipato na matumizi ni vitu ambavyo vinakwenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano leo hii mtu ambaye anafanya biashara anashindwa kupata sehemu nzuri ya kuweka biashara zake na mtu ambaye anaishi katika mazingira duni akiweza kupata uwezo wa kujenga nyumba bora, akiweza kupata uwezo labda wa kukodi sehemu nzuri ya kufanya biashara zake zikawa rasmi zaidi, maana yake ni nini; maana yake ni kwamba ameweza kuboresha maisha yake na hivyo basi kipato chake kimeongezeka.

Mheshimiwa Spika, leo hii tafsiri nyingine ambayo tunaweza tukaiona moja kwa moja hapa ni kwamba uwekezaji wetu katika nchi hii unakwenda sambamba pamoja na kipato chetu. Sekta hii ya uwekezaji na kipato huwa ni muhimu katika msingi wa kuongeza kipato. Ni jambo ambalo haliepukiki na ndiyo maana leo hii tukiangalia sekta ambazo zinaajiri watu wengi kabisa ni kwenye uwekezaji. Hivyo basi, itasaidia kuweza kufanya viwanda vyetu vihamasike, hasa viwanda vile ambavyo vinatumia rasilimali za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, tafsiri nyingine ya mwisho ambayo nimeipata katika *equation* hii ni kwamba mwelekeo wa matumizi ya Serikali yanachangia vilevile kipato cha wnanachi. Kwa mfano leo Serikali ikiamua kuwekeza katika umeme vijijini au katika miradi ya maji wakandarasi wa ndani wanapata uwezo na wanaweza kuajiri watu wengine na fedha inazunguka.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ambayo iko Mezani ni kwamba je, ni kwa kiasi gani mpango wetu huu wa miaka mitano umeweza kuzingatia tafsiri hizi tatu. Wakati huohuo tukiendelea kuhakikisha kwamba tunadhibiti mfumuko wetu wa bei, lakini wakati huohuo tunaendelea kudhibiti fedha haramu isiweze kuzunguka katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mpango wetu una maeneo makubwa matano. Eneo la kwanza linazungumzia kuhusu kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Lingine linazungumzia kuimarisha uzalishaji viwandani, kukuza biashara na uwekezaji, kuchochea maendeleo ya watu pamoja na kuendeleza rasilimali watu. Maeneo haya matano ukiangalia kimsingi na ukiangalia nafasi ya sekta binafsi katika kushiriki katika kufanikisha malengo haya ni jambo ambalo haliepukiki. Iwe sekta binafsi kupitia uwekezaji wa ndani, iwe sekta binagfsi kupitia uwekezaji wa nje ambao watatuletea *Foreign Direct Investment*, iwe uwekezaji wa ubia katika sekta binafsi na sekta ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii sasa kueleza kwa kifupi kwamba ni kwa vipi Mpango wetu wa Miaka Mitano tumejikita katika kuhakikisha kwamba tunaisaidia sekta binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi hii pamoja na kuhakikisha kwamba inasaidia kuongeza mzunguko wa fedha katika jamii.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ni la msingi ni kwamba tutahakikisha tunafanya maboresho ya kisera, kisheria, kitaasisi na kimfumo pale itakapohitajika ili kuondoa vikwazo na kuvutia uwekezaji ikiwemo kwenye masuala ya kodi ili kuimarisha weledi na ufanisi katika kukusanya kodi na kudhibiti ukwepaji kodi bila kutumia mabavu yasiyostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; tutaendelea kupanua wigo wa vyanzo vya kodi na wigo wa walipa kodi. Sasa hivi nchi yetu ambayo ina takribani watu milioni 55 ukiangalia *tax base* yake ya watu wenye *TIN Number* hawazidi watu milioni nne. Kwa hiyo, jambo hili ni jambo ambalo ni la msingi kabisa kuliangalia katika miaka mitano ambayo tunakuja.

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha tunakamilisha miradi yote ya kimkakati ikiwemo mradi wa umeme kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wa Nishati akiwa anamalizia hoja yake kwa Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo amezungumza Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kwamba suluhisho la kuweza kuhakikisha kwamba tunapata umeme wa uhakika na umeme wa bei nafuu ili viwanda vyetu viweze kupunguza gharama ya uzalishaji, ni kwa kutumia vyanzo mchanganyiko. Kwa hiyo, vyanzo vyote ambavyo vimeainishwa katika mpango huu, ikiwemo vyanzo vya makaa ya mawe, vyanzo vya gesi, vyanzo vya *hydro* na kadhalika, vitatumika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kujenga mazingira wezeshi kwa wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa ili

waweze kurasimisha biashara zao na kukuza mitaji yao, uwezo wao, ujuzi wao pamoja na uzoefu wao.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano ni kuongeza matumizi ya maarifa na ujuzi wa teknolojia madhubuti katika sekta ikiwemo sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na shughuli mbalimbali zinazojihusisha na usindikaji wa bidhaa nchini ili kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha kwamba tunajenga mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuendelea kuendesha shughuli za uzalishaji na uuzaji nje wa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi zilizoachakatwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati hii yote ambayo nimeieleza ambayo iko kwenye mpango huu...

SPIKA: Ahsante sana. Malizia kwa dakika moja.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: ...wa miaka mitano inahakikisha kama nilivyozungumza, kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua, nchi yetu inapiga hatua kimaendeleo lakini wakati huohuo tunaimarisha upatikanaji na mzunguko wa fedha katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer*. Hamad Masauni Yussuf, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

Sasa nimuite mtoa hoja mwenyewe, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, tafadhali. Sasa ujitahidi tu dakika nilizobaki nazo hapa kama 12 au 13, jitahidi uzitumie hizohizo kwasababu Waheshimiwa Mawaziri wamekusaidia kidogo, basi karibu sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja, nikushukuru wewe mwenyewe kwa fursa hii pamoja na Naibu Spika kwa kuendesha vizuri mjadala huu na niishukuru Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na wajumbe wake kwa michango waliyoitoa kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge waliochangia ni 111 wakiwemo 94 waliochangia kwa kuongea na 17 waliochangia kwa kuandika. Na niseme michango ya Wabunge wote kwa kweli imekuwa ya Kibunge kwelikweli na ninaamini itatusaidia katika kutekeleza mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda, kabla sijaenda kwenye hoja moja moja, nianze kwanza kwa kuisemea hoja ya jumla ile ambayo ilikuwa inahusisha kama wasiwasi kidogo hivi kuhusu utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, dira aliyoitoa Mheshimiwa Rais tangia ameapishwa na ambayo ameendelea kutoa katika maelekezo mbalimbali, katika matukio mbalimbali ya kitaifa ni dira tosha ambayo inatutosha kutupa uhakika wa utekelezaji wa mpango huu unaofuata, Mpango wa Tatu.

Mheshimiwa Spika, niwakumbushie tu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania ni maelekezo yapi yale yanayotoa dira ambayo yanatosha kutupa matumaini makubwa kwamba mpango huu tunakwenda kuutekeleza ili wote tuyazingatie.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kauli moja tu ya kwanza Mheshimiwa Rais aliyoitoa ni ile iliyokuwa inahimiza mshikamano katika Taifa letu. Alisema huu ni wakati wa kushikamana kuliko wakati mwingine wowote ule, tukishikamana mtu mmoja mmoja, viongozi, Serikali, sekta binafsi, ni dhahiri kwamba tunakwenda kuutekeleza mpango hii kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Rais alisema atasimama imara kwenye masuala ya mapato na matumizi. Na sisi viongozi tukiondoka na dira hiyo, sisi kwenye ngazi ya Wizara tumeshajipanga kwenda kuhakikisha kwamba tunatekeleza maelekezo hayo ya kusimama imara kwenye masuala ya mapato na matumizi. Tukisimama imara kwenye masuala ya mapato na matumizi ni dhahiri kwamba tunakwenda kutekeleza mpango huu kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Rais alisema atasimama imara, alisema atasimama imara kwenye masuala ya rushwa, *zero tolerance on corruption*. Jambo hili tukitembea nalo Watanzania wote kama dira ni dhahiri kwamba tunakwenda kuutekeleza mpango huu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Rais alilisema kwa nguvu kubwa, tena waziwazi, ni kwamba kodi za dhuluma, *no!* Akasema nendeni mkakusanye kodi kwa kutumia akili zaidi badala ya nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni nadra sana kusikia kauli za aina hiyo katika viongozi wengi sana wa Kiafrika. Dhamira ya aina hiyo ni jambo ambalo litafungua ushiriki wa hiari na wa kizalendo wa Watanzania wote kwenda kutekeleza mpango huu wa maendeleo. Na ni sifa moja ambayo naamini itatusaidia pia kwenda kuhakikisha kwamba tunatekeleza mpango huu kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, alisema Mkaguzi Mkuu (*CAG*) usiwe na kigugumizi. Maana yake ni nini; maana yake anachofanya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kujenga taasisi katika utendaji wa kazi. Ameelekeza hilo na maana yake kila sekta na kila taasisi ziwajibike katika kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo na Mawaziri wengine wamelisemea ni miradi mikubwa yakielelezo yote iendelee. Na tumeona hatua ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, mengine ni masuala ya haki. Amesema kesi za uonevu zote zifutwe, zile ambazo hazina base, zile ambazo hazina msingi, zifutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hakuishia hapo, akasema wananchi hawana fedha mifukoni, madeni yalipwe na vitu vingine ambavyo vinaweza kuchochea mzunguko wa fedha kwenye uchumi, na punde mzunguko wa fedha unapokuwa mkubwa maana yake tutakuwa na makusanyo na tunapopata makusanyo maana yake tunakwenda kutekeleza miradi hii ambayo tumeiainisha katika Mpango huu wa Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania, kwa hiyo dira ya aina hii sote tunatakiwa tuiunge mkono, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais ili tuweze kutekeleza mpango huu. Na naamini ni jambo ambalo litaleta tija.

Mheshimiwa Spika, tuache chachandu chachandu zingine. Maana yake kauli zenye dira zimetolewa halafu kunatoa vimaneno vimaneno vingine; tuache chachandu chachandu zingine, kauli aliyotoa Mheshimiwa Rais na maelekezo aliyoyotoa yanatutosha kutupeleka kutupeleka mbele, yanatosha kutupeleka mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wanasema tumesikia kauli lakini hatuna imani, tunataka tuone vitendo. Kazi ya Urais si kama tofali useme utamuona siku moja anabeba tofali hivi uone ndiyo kitendo kile pale amekifanya; haya maelekezo aliyoyotoa ndiyo yameshaanza kufanyiwa kazi na wengine wameshaanza kutoa ushahidi kwamba akaunti zimefunguliwa, wengine wameshatoa ushahidi kwamba kesi imefutwa, kati ya yale ambayo alikuwa ameyatolea maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na sisi wasaidizi wake tayari tunaendelea kuyafanyia kazi na kila taasisi ambayo inaguswa na maelekeo imeingia kazini kuyafanyia kazi. Mheshimiwa Askofu Gwajima yuko hapa angeweza kutuambia,

walikuwepo wale waliokuwa na mashaka, wasaidizi wa Yohana, akawatuma, nendeni mkamuulize hivi yule ni yule tuliye kuwa tunamngojea au tuendeleo kumngojea mwingine? Wala hakuwajibu kuwa ni mimi, akawaambia tu vipofu wanaona, viwete wanatembea, wakoma wanatakaswa na akasema heri mtu yule ambaye hana mashaka nami. Sasa na wale ambao wana mashaka tuwaambie ni huyu huyu, hakuna tunayemngojea. 2025 tunaweka *comma* tu lakini safari inaendelea, nukta ni mpaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wanadiriki kuruisha mishale mpaka kwa Hayati. Nilisikia mahali hivi wengine wanarusha mishale; mwacheni mzee apumzike. *(Makofi)*

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangalia sana)

SPIKA: Nakuongezea Mheshimiwa Waziri wa Fedha; tena apumzike kwa amani. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru; tena apumzike kwa amani. Amemaliza kazi yake Serikalini, amemaliza kazi yake duniani, tuliosalia ndio tuna kazi, tuna wajibu sisi tunalifanyia nini Taifa letu. Si utaratibu wa Kiuchamungu kumrushia mishale mtu ambaye ametangulia mbele za haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa dira hii ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa, nitoe rai na nirudie tena; twendeni, tuchape kazi, kazi iendeleo na twendeni kila mmoja awajibike katika eneo lake ambalo anawajibika kufanya kazi ili tuweze kuutekeleza ipasavyo mpango wetu.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye hoja moja moja; Kamati ilikuwa inapendekeza kwamba tuone umuhimu wa mikopo yote kuelekezwa katika kukamilisha miradi ya maendeleo, hasa ile ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yamezingatiwa na yanakwenda sambamba kabisa na

sheria, sura ya 5 kipengele Na. 5.7 na sehemu ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa pamoja na kifungu cha tathmini na uhimilivu wa deni la Taifa katika Knauni ya 38 ya Sheria ya Mikopo, Dhamana pamoja na Misaada. Kwa hiyo, haya yamezingatiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wallisemea.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo kamati ilitolea maoni, iliona kuna umuhimu wa malengo kwenda sanjari na hatua stahiki zinazochukuliwa katika mpango wa utekelezaji ukiwa umekwenda sambamba na mikakati ya utekelezaji wa mpango, mkakati wa ugharamiaji wa mpango, mkakati wa ufuatiliaji pamoja na tathmini wa mpango pamoja na mapitio na mikakati ya mawasiliano ndani ya Wizara zetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitoa maoni kuhusu wakandarasi wa ndani, jambo hili pia limezingatiwa na matumizi mbalimbali ya fursa pamoja na ugharamiaji wa mpango; jambo hili pia limezingatiwa. Jambo lingine ambalo limeongelewa na Wabunge wengi kuhusu tathimini pamoja na ufuatiliaji, jambo hili tumezingatia taratibu ambazo zinatumika katika nchi nyingi, lakini pia zinazotumia utaratibu wa tathimini ambao wametungua sheria na zile ambazo wanatumia utaratibu wa ufuatiliaji wa ndani ya taasisi husika.

Kwa msingi huo na kwa kutambua umuhimu wa kuwa na nyenzo za ufuatiliaji na tathimini Serikali imechukua hatua ya kuandaa mwongozo na ufuatiliaji wa tathimini ili kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza kuhusiana na masuala haya ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisemea kwa kiwango kikubwa ni lile lililokuwa linasema bajeti za maendeleo zitekelezwe kama ambavyo zilikuwa zimepangwa na kupitishwa na Bunge; jambo hili linazingatiwa. Jambo lingine ni uwepo wa uwajibikaji wa kina katika matumizi ya fedha; jambo hili litazingatiwa na Mheshimiwa Rais tayari alishalitolea kauli na kauli hiyo ni mwongozo kwa taasisi zote, Wizara pamoja na idara zote huku Serikalini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilitolewa maoni na Wabunge wengi ni kuongeza wigo wa kodi na mahsusi ilikuwa Serikali ipunguze kiwango cha kodi ya makampuni ili kuvutia uwekezaji wa ndani na kampuni za nje ili kuongeza *multiplier effect* katika kuimarisha ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limekuwa likifanyiwa kazi. Ukiangalia katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilipunguza kiwango cha kodi hiyo kutoka asilimia 30 hadi 20 kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2018/2019 hadi 2022/2023 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya madawa ya binadamu pamoja na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi. Sambamba na hilo mwaka 2019/2020 Serikali ilipunguza kiwango cha kodi ya mapato ya kampuni kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2020/2021 kwa wawekezaji wapya wanaotengeneza taulo za kike.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo makampuni mapya yaliosajiliwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam yalitozwa kodi ya mapato ya kampuni ya asilimia 25 kwa kipindi miaka mitatu mfululizo kuanzia tarehe iliposajiliwa. Kwa maana hiyo Serikali itaendelea kuyaangalia masuala ya haya ambayo yalitolewa hoja na Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo nimesema. Yale masuala mengine ambayo yametolewa na Wabunge yanayoashiria, ambayo yamebeba maudhui ya kikodi tutayaelezea kwa kina tutakapokuja kwenye Bajeti Kuu pamoja na Muswada ule wa sheria, yaani *Finance Bill*. Yale mengine ambayo yanawahusu sekta, sekta zinazohusika zitaendelea kuyaelezea punde tu tutakapokuwa tunaenda kwenye mawasilisho yale ya kissekta.

Mheshimiwa Spika, *concern* nyingine ya Wabunge wengi ilikuwa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo pamoja na kutekeleza masuala mengine. Ni vyema ukaweka viwango vya maisha tofauti ikiwa ni busara mpango huu uweze...

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nitalisemea hili kwa kuwa naelekea dakika za mwisho za wasilisho.

Kwa kuhitimisha nirudie tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya mapendekezo wa Mpango huu wa Taifa. Nichukue fursa hii kuzitakia Wizara, Idara zinazojitegemea Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza ipasavyo falsala yetu ya kazi iendelee, na hivyo wajielekeze katika kusimamia utekelezaji wa mpango huu ili tuweze kufikia azma yetu ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sana kabisa, nawashukuru sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa wasilisho lako la hitimisho zuri kabisa; japo muda ulikuwa hautoshi kupitia hoja zote lakini umejitahidi. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama ilivyowajibu naomba niwahoji kwamba Bunge limejalidili na kuidhinisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026. Wanao afiki waseme ndiyo, wasioafiki wasema sio. Nadhani walioafiki wameshinda,

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha
Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2021/2022 – 2025/2026
ulipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Nawashukuruni sana Waheshiwa Wabunge kwa ushirikiano, nawashukuru zaidi Serikali kwa kazi kubwa

sana ya kuja na mpango huu na michakato yake yote mpaka tumefika leo. Watu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara nyingine zote ambazo zimeshiriki katika kutengeneza mpango huu *comprehensive* kabisa, tunasema ahsanteni sana. Tunaamini tumepata kiongozi sasa kwa maana ya mpango huu cha kuweza kutupeleka mbele zaidi na zaidi. Tunashukuru sana.

Kesho tutakuwa na, tunaanza ile *budget session* yenyewe. Kama ilivyo ada kanuni zetu zinatutaka tuanze na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, huwa ndio inayoanza ya kwanza kabisa. Kwa hiyo tuwepo ili tusikilize hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na baada ya hapo tujipange kuchangia kwa siku zile zilizopangwa, nafikiri kuanzia kesho mpaka Ijumaa tutahitimisha.

Kwa hiyo kama ambavyo huwa nawasisitiza wale ambao mngenda kuchangia kwa dakika ambazo angalau zinatoshwa muanze mapema, msisubiri kule mwishoni tunaanza mbio mbio inakuwa tena, mawazo yako pia yanaweza yasifanyiwe vizuri kama yametolewa mwishoni sana, yakitolewa mapema ni jambo la kushukuru.

Sasa Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaweza ukaanza wakati wowote hivi karibuni. Kwa utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Bunge ambalo huwa Bunge limejiwekea nyakati kama hizo za kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani vikao vya Bunge hukutana kama kawaida saa 3:00 asubuhi mpaka saa saba mchana na kusitishwa. Jioni huwa tunaanza saa 10:00 alasiri na baada ya hapo huwa tumaliza saa 12:00 jioni. Kipindi cha jioni ni saa 10:00 jioni hadi saa 12:00, *two hours*.

Kwa hiyo nashauri mkiridhia Waheshimiwa Wabunge tumuombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu atutolee hoja ya kutengua kanuni.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi karibu.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI YA MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:
Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kwa unyenyekevu kwa maelekezo yako ili nitoe maelezo ya hoja ya kutengua kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kKwa kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 34 (2), (4) Bunge lako linakutana hadi saa 7:00 mchana na kusitishwa mpaka saa 11:00 jioni; na baada ya hapo Bunge lako huendelea kukaa mpaka saa 1:45 usiku ambapo Spika husitisha shughuli na kuliahirisha hadi siku nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni ndani ya kipindi cha Mkutano wa Tatu wa Bunge unaoendelea, waumini wa Dini ya Kiislamu wataanza mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo katika kipindi hicho waumini wote wa kiislamu watakaofunga hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa 12:30 jioni.

Na kwa kuwa ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge ambao ni Waumini wa Dini ya Kiislamu waweze kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini yao, na vile vile kutoa muda wa kutosha kwa wachangiaji wa bajeti za Wizara na shughuli nyingine za Bunge zitakazopangwa inabidi Bunge litengue kanuni ya 34 (2) na kanuni ya 34 (4) ya kanuni za kudumu za Bunge kwa mujibu wa kanuni 174 (1).

Mheshimiwa Spika, hivyo basi Bunge linaazimia ya kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge wakati huu wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani;

(i) Kanuni 34(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa saba mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yeyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni itenguliwe; na badala yake Bunge linaposisitishwa

saa saba mchana liendelee na shughuli zake ifikapo saa kumi jioni badala ya saa kumi na moja jioni.

(ii) Kanuni ya 34(4) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litaendelea hadi saa moja na dakika arobaini tano usiku ambao Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake itenguliwe na badala yake Bunge liahirishwe ifikapo saa kumi na mbili jioni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utanza kutumika mara tu Mfungo Mtukufu wa Ramadhani utakapoanza na baada ya mfungo huo kukamilika Bunge litarejea katika utaratibu wake wa kawaida. Kwa heshima kubwa na taadhima ya mwezi mtukufu wa Ramadhani ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono, lakini sasa ni wajibu wangu kuwahoji. Naomba make. Wanaoafiki hoja hiyo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, waseme ndio, wasioafiki waseme sio. Wote wameafiki hoja hii. Kwa hiyo tutakwenda kwa utaribu huo mara tu mfungo utakapoanza rasmi. *(Makofi)*

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Ninamatangazo mawili ya mwisho, moja Wabunge kutoka chama cha waliowengi, kikao Msekwa baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, la kwanza. Tangazo la pili ni kwa wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa maana ya wenyeviti wetu wote wa kamati natumaini mmeshapa ujumbe kupitia sms zenu kuhusiana na kikao kesho saa saba mchana kwenye ukumbi wa Spika, na mmeshaambiwa Ajenda ni kupitia masuala yanayohusiana na bima ya afya ya Wabunge, tayari kazi kubwa imeshafika kwa hiyo mtapokea na kutoa maoni yenu kuhusiana na mapendekezo yatakayokuwepo kutoka kwa watoa bima wetu na

Management ya Bunge. Na tukumbuke Waheshimiwa Wabunge bima ya afya ya Wabunge pia inawahusu Waheshimiwa Mawaziri wote. Bima ya Wabunge ndio Bima ya Waziri inafanana kwa kila kipengele kwa kila jambo, na hilo ndio jambo ambalo linafanyiwa kazi liko mikono salama.

Kesho saa saba basi Kamati ya Uongozi tukutane na kupitia kama ya uongozi kama kutakuwa na umuhimu basi kesho kutwa mchana tunaweza kufanya kikao cha Wabunge wote kuhusiana na jambo hilo, kama itaonekana ni vizuri ni kufanya hivyo kufuatana na ushauri tukaopata kwenye Kamati ya Uongozi ya Waheshimiwa Wabunge.

Basi kwa hatua hiyo naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 07.54 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 13 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*